Tume iliwahoji wadau wengi. Wadau hao walikuwa ni pamoja na wanataaluma; wanasheria; viongozi wa kidini; wabunge; viongozi na wanachama wa vyama vya siasa; wanachama wa vyama visivyo vya kiserikali (NGOs), pamoja na wale wanaojishughulisha na masuala ya haki za binadamu na utawala, pamoja na wanaojishughulisha na masuala ya wanawake na vijana; vyama vya kidini (FBOs); vyombo vya habari; sekta binafsi; vyombo vya kiuledi, kikiwemo chama cha wanasheria; wanachama wa vyama vya wafanyakazi; Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC); na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG). Zaidi ya watu kutoka katika makundi haya, huko Pemba wajumbe wa tume walifanya mazungumzo na watu wa kawaida kutoka katika makundi mbali mbali na wanaofanya shughuli mbali mbali, pamoja na wavuvi, wakulima wa karafuu, wakulima na wafugaji.

Zaidi ya mahojiano na watu mmoja mmoja, tume ilifanya mahojiano na Makundi ya Walengwa Mahasusi (FGDs). Makundi hayo yalikuwa ni ya vijana na wanawake kisiwani Unguja. Makundi ya Walengwa Mahasusi yaligawiwa katika jinsia na sehemu wanzotoka (mjini na vijijini), na kujumuishwa pamoja bila ya kujali vyama vyao vya siasa.

Kasoro chache ziliathiri kazi ya tume. Tume haikuweza kukutana na viongozi muhimu kutoka serikalini, chama tawala, viongozi na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibara (HoR). Wengi wao walikataa kuizungumzia mada husika au walionekana kuwa na shughuli nyingi na kushindwa kuifuata ratiba yetu iliyojaa shughuli.

## Usuli: Historia Fupi ya Ukoloni na Katiba

---

Visiwa vya Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa viwili, Pemba na Unguja. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### Utawala wa Waarabu na Ukoloni

Wabantu waliweka maskani yao katika visiwa hivi tokea karne ya 2 Baada ya Kuzaliwa Nabii Issa.<sup>1</sup> Wakati wa karne ya 11 na 12, Mabaharia wa Kiajemi walijenga kituo chao katika visiwa hivi na kuoana na wenyeji. Walifuatiwa na Wareno mnamo mwisho wa karne ya 15 na walividhibiti visiwa hivi mpaka walivyotimuliwa na Waarabu kutoka Omani mwaka 1698. Mwaka 1832, mtawala wa Omani, Sultan Seyyid Said, alihamia Zanzibar. Alianzisha utawala wa mamwinyi wa Kiarabu uliotegemea nguvukazi ya watumwa na kujenga uchumi madhubuti wa biashara ya viungo. Kwa msaada wa fedha kutoka kwa Wahindi, Sultani alijihusisha vile vile na biashara ya watumwa na madini. Matokeo yake ni kuwa idadi ya Wahindi ilizidi, na baadaye Wazungu walianzisha mahusiano ya kidiplomasia,<sup>2</sup>

---

1 Jjuuko Frederick & Muriuki Godfrey, *Federation within Federation, The Tanzania Union Experience and the East African Integration Process*, Ripoti ya Tume ya Kutafuta Ukweli wa Mambo Tanzania ya Kituo cha Katiba, uk.2.

2 Ibid., uk.3

Marekani (USA) ikiwa ndiyo ya kwanza kufungua ofisi yake ya ubalozi mwaka 1836, ikifuatiwa na Wingereza na Ufaransa mwaka 1844.<sup>3</sup> Hivi sasa, Zanzibar in mchanganyiko wa makabila mbali mbali, wawakilishi wa wageni wake wa hapo kale<sup>4</sup>– miongoni mwao ni watu wenye asili ya Afrika, Waarabu, Wahindi na Wachina.

Ijapokuwa Waarabu wa Oman walikuwa ni wateja wa Waingereza katika kipindi chote cha karne ya 19, Waingereza wakiwasaidia katika kuwashughulikia raia wake wakorofi, hii ilibadilika pale Zanzibar ilipotangazwa kuwa himaya ya Wingereza mwezi Juni mwaka 1890. Kuanzia hapo, Zanzibar ilitawaliwa na sultani aliyelelewa na Wingereza, huku madaraka kamili yakiwa ni ya Waingereza. Mwaka 1913 Waingereza waliweka Zanzibar chini ya Ofisi ya Makoloni na kuteua Balozi Mkaazi ambaye alikuwa na madara kamili mpaka Zanzibar ilipopata uhuru mwaka 1963.<sup>5</sup> Kuanzia mwaka 1914 hadi 1925, liliundwa Baraza la Mahamia likiwa ni chombo cha ushauri kwa sultani. Mwaka 1925 liliundwa Baraza la Utendaji (EXco) na Baraza la Kutunga Sheria (Legco). Nafasi ya Baraza la Mahamia ilichukuliwa na Baraza la Utendaji (EXco) na Baraza la Kutunga Sheria likiongozwa na Balozi Mkaazi wa Wingereza likawa ndiyo chombo cha kutunga sheria cha mahamia hiyo. Sheria yoyote ya sultan iliweza kupitishwa tu baada ya ushauri na ridhaa ya Baraza la Kutunga Sheria. Kwa ufupi, madaraka ya sultan yalipunguzwa. Kwa miongo miwili ya kuwepo kwake, Baraza la Kutunga Sheria

3 Yahya Khamis Hamad & Peter Maina Chris, 'Elections in Zanzibar and their consequences: ZEMOG na Miafaka', katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), in *Zanzibar, The Development of the Constitution*, 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3, uk.122

4 *Zanzibar: A Giant cultural Melting Pot at the East African Coast*, accessed at <https://www.africantravelhub.com/zanzibar-a-giant-cultural-melting-pot-at-the-east-africa-coast/>; see also William Cunningham Bissell & Marie -Ande Fouéré (ed.), *Social Memory, Silenced Voices, and Political Struggle: Remembering the Revolution in Zanzibar*, uk.328, imepatikana katika <https://books.google.co.ug/books?id=oEZbDwAAQBAJ&pg=PA328&lpg=PA328&dq=Social+Memory,+Silenced+Voices,+na+Political+Struggle.+Remembering+the+Revolution+in+Zanzibar,+melting+post+of+races&source=bl&ots=1qRCAfXQ2d&sig=>

5 Jjuuko & Muriuki, op.cit., uk.2-4

halikuwa na wajumbe ‘Waafrika Wazawa’ hadi mwaka 1946, ambapo kutokana na mabadiliko ya hali ya kisiasa katika Ulaya ya Magharibi, ikiwa ni pamoja na kuingia madarakani kwa Chama cha Labour huko Wingereza, Mwafrika, Sheikh Ameir Tajo, alijiunga na Baraza hilo. Mwafrika wa pili alijiunga na Baraza hilo miaka mitatu baadaye mwaka 1949.<sup>6</sup>

## Kuelekea uhuru

### **Baraza la Kutunga Sheria**

Kwa ahadi ya kupata serikali ya ndani, Baraza la Kutunga Sheria lilibadilishwa muundo wake mwaka 1955 kwa kuwa na wajumbe sawa walio rasmi na wasiokua rasmi, kumi na mbili kila upande. Kwa wajumbe wasio rasmi idadi ya Waafrika na Waarabu ilikuwa ni sawa – wane kila upande – pamoja na Waasia watatu na Mzungu mmoja. Wakati huo, Waarabu walikuwa na chama kimoja; Wahindi walikuwa na vyama viwili: the Indian Association na Muslim Association; na Waafrika walikuwa na vyama viwili vile vile: the African Association kikiongozwa na Sheikh Abeid Karume, na the Shirazi Association, kikiongozwa na Sheikh Ameir Tajo na Sheikh Thabit Kombo.<sup>7</sup>

Mwanzoni mwa mwaka 1954, Balozi Mkaazi wa Wingereza, wakati huo akiwa, John Rankine alipendekeza kuwepo kwa wajumbe 12 wa kuteuliwa – wanne kila upande, kwa Waafrika na Waarabu, Wahindi watatu na Mzungu mmoja. Pendekezo hili lingeliimarisha uwakilishi wa wananchi lakini bado liliheshimu uteuzi wa wajumbe kwa mujibu wa makabila yao. Chama cha African Association kililikubali pendekezo hili lakini Waarabu wasomi, vijana kutoka chama cha Arab Association walilikataa.<sup>8</sup> Waarabu walikuwa na madai kadha, ikiwa ni pamoja na uchaguzi wa mtu mmoja kura

---

6 Hamad & Peter, op.cit., uk.122-125

7 Ibid., uk.126

8 Glassman, Jonathan, *War of Words, War of Stones: Racial Thought and Violence in Colonial Zanzibar*, 2011, Indiana: Indiana University Press, uk.60

moja, uchaguzi mkuu, uwakilishi rasmi wa wachaguliwa walio wengi katika Baraza la Kutunga Sheria na kuwepo kwa mawaziri.<sup>9</sup>

Glassman anaelezea kwa kina:

Mapema mwaka 1954, balozi mkaazi, John Rankine, alipendekeza kuwepo kwa mabadiliko ya katiba yatakayoengeza uwakilishi wa wananchi katika Baraza la Kutunga Sheria (Waarfrika na Waarabu wawe na idadi sawa ya viti) lakini yaendeleo kuheshimu kanuni ya kuteua wajumbe kwa mujibu wa makabila yao. Tajo na African Association waliliunga mkono pendekezo hilo. Lakini pendekezo hili lilisababisha mgawanyiko mkubwa miongoni mwa wananchi wakereketwa, Waarabu wasomi katika Arab Association. Wakati wazee ambao walikuwa wengi katika Kamati ya Utendaji ya Arab Association walipiga kura ya kuiunga mkono katiba ya Rankine, walipingwa na wajumbe vijana, wasomi ambao walishawishiwa sana na siasa za Kairo. Miongoni mwao alikuwa Ahmed Lemke, mhariri wa gazeti la kila wiki la Arab Association, Al-Falaq. Makala ya mhariri yaliyoandikwa na Lemke yalidai kuwa wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria wachaguliwe moja kwa moja na wapiga kura watakaorodheshwa katika daftari la wapiga kura bila ya kujali makabila yao; alitoa madai haya kwa lugha kali ya kupinga ukoloni iliyokuwa na nia ya kuwaaibisha wale wanaofuata siasa za mrengo wa kati ambao walikuwa ndiyo wachapishaji wa gazeti hilo. Mwezi Juni 1954, makala yake ya mhariri yaliwalazimisha Waingereza wamkamate yeye na wajumbe wote wa kamati ya utendaji kwa makosa ya uchochezi.

...Kwa kupinga ukamataji huo na kwa kiasi fulani kuunga mkono madai ya Al-Falaq ya kuwepo kwa uchaguzi wa Baraza la Kutunga Sheria bila ya kujali makabikla ya wapiga kura, Arab Association ilitangaza mgomo katika vyombo vyote vya ushauri vya serikali na wajumbe wake kujitoa kutoka katika Baraza la Kutunga Sheria. Mjumbe pekee ambaye hakujitoa alikuwa Ali Sultan Mugheiry, mjumbe wa Kamati ya Utendaji, ambaye baada ya kumwomba radhi Rankine, hakukamatwa. Mwezi Novemba 1955, hata haikutimia wiki moja tokea aingie katika Baraza la

---

9 Hamad & Peter, op.cit., uk.127

Kutungua Sheria, Mugheiry aliuawa kwa kuchomwa kisu. Kuuawa kwake kumekuwa na athari kubwa miaka mingi baadaye.<sup>10</sup>

Juu ya yote hayo yalioelezwa hapo juu, Waingereza waliendelea na pendekezo lao. Waarabu waligoma kuingia katika Baraza la Kutungua Sheria kwa miezi 18.<sup>11</sup>

Mwaka 1956, Tume ya the Coutts iliyoundwa ili kupendekeza namna ya kuwapata wajumbe wasiokuwa rasmi wa Baraza la Kutungua Sheria ilipendekeza kuwepo kwa uchaguzi kwa viti sita kati ya viti 12 vya wajumbe rasmi, na kupendekeza kuwa mgombea wa Baraza la Kutungua Sheria awe raia wa Zanzibar, na mpiga kura awe raia aliye chini ya himaya ya Wingereza. Utaratibu wa kuwachagua wajumbe sita wasiokuwa rasmi wa Baraza la Kutungua Sheria kwa kutumia daftari la orodha ya wapiga kura ulianzishwa mwaka 1957 likiwa ni badiliko kubwa la katiba. Kipindi hiki kilisadifu kuwa ndicho baadhi vyama vya siasa viliundwa, Zanzibar Nationalist Party (ZNP), kiliundwa Desemba 1955, kutokana na chama cha the Nationalist Party of the subjects of the sultan ( Hizbu), na Afro-Shirazi Union (ASU), kilichotokana na muungano wa haraka wa African Association na Shirazi Association mwaka 1957. Chama hiki baadaye kilitwa Afro-Shirazi Party (ASP).<sup>12</sup>

## **Uchaguzi wa 1957**

Ijapokuwa chaguzi za mwanzo za kikoloni za mwaka 1957 zilikuwa na wagombea kutoka vyama mbali mbali vya siasa, vyama vya kikabila na kidini, wagombea hasa walikuwa ni vyama vya ASP na ZNP.<sup>13</sup> Katika uchaguzi huu wa 1957 ASP ilishinda majimbo matano kati ya majimbo sita. Mshindi wa Kiti cha Mji Mkongwe alikuwa ni mgombea kutoka Muslim Association, kimoja kati ya vyama viwili vya Wahindi wakati ZNP haikupata hata kiti kimoja.

---

10 Glassman, *op.cit.*, uk. 60

11 Hamad & Peter, *op.cit.*, uk. 127

12 *Ibid.*, uk.127-8

13 *Ibid.*, uk. 128

Ijapokuwa Waafrika walikuwa wachache katika Baraza la Kutunga Sheria, kwa mara ya kwanza idadi yao iliwashinda Waarabu katika Baraza la Kutunga Sheria la mwaka 1957.

Tume ya Blood ya 1960 iliteuliwa ili kutoa mapendekezo ya hatua za kikatiba visiwani humo ikiwa ni pamoja na kuwa na wadhifa wa mawaziri, watakaoongozwa na waziri kiongozi, Baraza la Kutunga Sheria lenye wajumbe 22, kugawa majimbo ya uchaguzi, kuhlalisha ushiriki wa wanawake katika uchaguzi na kupunguza masharti ya kumiliki mali na kiwango cha elimu kwa wanaume.<sup>14</sup> Kukubaliwa kwa mapendekezo hayo kumepelekea kufanyika kwa uchaguzi wa Januari 1961.

### **Uchaguzi wa 1961**

Katika uchaguzi wa 1961 idadi ya wapiga kura walioandikishwa ilikuwa marudufu ya ile ya walioandikishwa mwaka 1957. Majimbo zaidi yalianzishwa na kuyafanya yafikie 22 (13 Unguja na tisa Pemba). Chama cha ASP kilishinda viti 10 na ZNP viti tisa; na Zanzibar Pemba People's Party (ZPPP), ambacho kilijitoka kutoka katika ASP mwaka 1959, kilipata viti vitatu. Ule muungano uliotarajiwe kuwepo kati ya ZPPP na ASP au ZNP na ASP haukutokea kwa sababu ZPPP yenyewe ilikuwa imegawika. Mjumbe wake mmoja alijiunga na ASP na wawili walijiunga na ZNP. Hii ilisababisha kutokea kwa mdororo uliosababisha kuitishwa kwa uchaguzi mwengine. Iliundwa serikali ya mseto ilioyoongozwa na Waziri Kiongozi na na mawaziri kutoka vyama vyote. Serikali hiyo ilidumu kwa muda wa mieazi sita.<sup>15</sup> Ili kuepuka mdororo mwengine, lilianzishwa jimbo jipya la uchaguzi huko Pemba kabla ya uchaguzi mwengine wa mwezi Juni 1961. Vyama vya ZNP na ZPPP viliunda umoja wao. Ijapokuwa uchaguzi huo ulivurugwa kwa kutokea fujo, hatimaye ASP ilishinda viti 10 na kura zake kuongezeka, ZNP ilishinda viti 10, na ZPPP ilidhibiti

<sup>14</sup> Ibid., uk.129-130

<sup>15</sup> Ibid., uk.131

viti vyake vitatu lakini kura za vyama hivyo viwili zilipungua.<sup>16</sup> Kwa hivyo, iliundwa serikali ya mseto kati ya ZNP na ZPPP.

### **Mkutano wa katiba, uchaguzi na uhuru**

Mkutano wa katiba wa kuzungumzia uhuru wa Zanzibar ulifanyika London kati ya tarehe 19 Machi na tarehe 6 April 1962 na ulihudhuriwa na vyama vyote vya siasa. Hata hivyo, kwa sababu ya tofauti zilizokuwepo kati ya chama cha ASP na muungano wa ZNP-ZPPP, mkutano huo ulimalizika bila ya mafanikio yoyote. Wakati chama cha ASP na ZNP-ZPPP waliahidi utiifu wao kwa Sultan na kutaka utawala wake uendelee, maoni yao kuhusu programu ya kuipeleka Zanzibar kwenye serikali ya ndani hadi kufikia uhuru yalitofautiana.<sup>17</sup> Chama cha ASP kilitaka kuondolewa kabisa suala la uwezo wa kiuchumi na kiwango cha elimu katika uchaguzi, kupunguzwa kwa umri wa kuweza kupiga kura na kuwa miaka 18, kuongezwa kwa idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa kutoka 23 hadi 31, na kufanyika uchaguzi mwengine. Lakini muungano wa ZNP/ZPPP uliyakubali mashari ya kuondoa uwezo wa kiuchumi na kiwango cha elimu tu na kuyakataa madai mengine yote.<sup>18</sup>

Tarehe 24 Juni 1963, Zanzibar ilipata uhuru wa kuwa na serikali ya ndani na uchaguzi mwengine ulifanyika kuanzia tarehe 8 hadi tarehe 15 Julai. Muungano wa ZNP-ZPPP ulishinda viti 18 na ASP viti 13, lakini ikiwa na wingi wa kura. Mkutano wa mwisho wa katiba ulifanyika London mwezi Septemba 1963. Ulikuwa juu ya Katiba ya Uhuru. Mkutano ulikubaliana kuwa tarehe rasmi ya uhuru ni tarehe 10 Desemba 1963 sultani akiwa mkuu wa serikali na akipewa madaraka zaidi ikiwa ni pamoja na madaraka ya kumteua mrithi

---

16 Ibid.

17 Othman Haroub, *Yes, in My Lifetime: Selected Works of Haroub Othman*, Saida Yahya-Othman (ed.), 2014, Mkuki na Nyota, uk.158. Kwa taarifa zaidi angalia Colonial Office, report of the Zanzibar Constitutional Conference, 1962, London

18 Ibid, uk.3

wake. Tarehe 10 Desemba 1963, Zanzibar ilipata uhuru na kumaliza miaka 73 ya utawala wa wakoloni wa Kiingereza.

## Mapinduzi na Kuundwa kwa Muungano

Tarehe 12 Januari 1964 yalitokea mapinduzi Zanzibar ambayo yaliipindua serikali ya mseto ya ZNP/ZPPP, yaliondoa ufalme na kuifuta Katiba ya Uhuru. Baraza la Mapinduzi lilitangaza utawala wa amri. Tarehe 26 April 1964, Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika ziliungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.<sup>19</sup>

Tarehe 29 Oktoba 1964, nchi hiyo ilibadilishwa jina na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<sup>20</sup> Muungano uliendeshwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Muungano na kuridhiwa mara baada ya hapo. Katiba ya Tanganyika ilikubaliwa kuwa ndiyo katiba ya kwanza na ya muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania URT na ilitarajiwa kutumika kwa mwaka mmoja hadi 1965. Hata baada ya Muungano, Zanzibar iliendelea kuwa na uhuru wa kiasi fulani na hadi sasa bado ina serikali yake, chombo chake cha kutunga sheria na mahakama.

Hapo mwanzo Mkataba wa Makubaliano ya Muungano ulikuwa na mambo 11 lakini baada ya muda yameongezeka sana. Chini ya utaratibu huu kuna yale yanayoitwa ‘Mambo ya Muungano’, ambayo yanazihuzu zote, Tanzania Bara na Zanzibar, na ‘Mambo Yasiyokuwa ya Muungano’ yanayoihusu Zanzibar tu. Serikali ya Muungano ina madaraka ya kushughulikia mambo ya Muungano na mambo yasiyokuwa ya Muungano kwa Tanzania Bara wakati Serikali ya Zanzibar ina madaraka ya kushughulikia mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Zanzibar. Hakuna serikali ya Tanganyika na hakuna serikali na chombo cha kutunga sheria kwa ajili ya serikali hiyo.

---

<sup>19</sup> Hamad & Peter, op.cit, uk.135

<sup>20</sup> Jjuuko & Muriuki, op. cit., uk.6

## Kuelekea Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU)

---

Zanzibar imekuwa na majaribio matatu ya kuleta muafaka na mawili yalimalizika kwa mafanikio. Kabla ya suluhisho la tatu – *Muafaka III*, palikuwepo na *Miafaka* miwili – *Muafaka I* wa 1999 na *Muafaka II* wa 2001. *Miafaka* yote miwili ilikuwa na nia ya kushughulikia vurugu za baada ya uchaguzi zilizotokea Zanzibar na hali ya kutoelewana kati ya serikali na upinzani. Matatizo hayo yaliendelea na *Miafaka* miwili haikutekelezeka kwa hivyo ukawepo Muafaka III. Hata hivyo, Muafaka III haukutiwa saini na hii ilisababisha kuwepo kwa jaribio jingine yaani *Maridhiano*. Asili ya upatanishi huu ni siasa za ubishani na vurugu za Zanzibar.

### Usuli wa *Miafaka*: Historia Fupi ya Uchaguzi Zanzibar

Hali ya sasa ya kisiasa na ya kikatiba ya Zanzibar haiwezi kueleweka bila ya kusoma historia yake ya uchaguzi ambao ndiyo kiini cha juhudi zote za upatanishi – *Miafaka*, na baadaye *Maridhiano*.

Vyanzo vyote vinadhihirisha kuwa kihistoria, tokea wakati wa ukoloni, chaguzi zote za Zanzibar zimekuwa za utata na kutawaliwa na machafuko ya baada ya uchaguz. Machafuko hayo yalianza tokea

wakati wa uchaguzi wa kwanza mwaka 1957. Jazba zilipanda na siasa ziliathiri kila familia.<sup>21</sup>

Ripori ya Idara ya Utawala kwa mwaka 1958 inaielezea hali hiyo:

Mwaka huu umeshuhudia namna siasa zilivyoathiri kila sehemu ya maisha ya Zanzibar na wafanyabiashara, wakulima, vibarua, wavuvi na hata wake wa majumbani waliathirika. Wanavijiji mashambani walibishana. Mazishi na sherehe za kidini ziligomewa na vyama vinvyopingana! Wanawake waliweka rahani nguo zao ili kupata pesa za nauli ya kuwafikisha kwenye mikutano ya kisiasa. Hayo yalikuwa ndiyo matokeo ya uchaguzi mkuu wa kwanza katika visiwa ambavyo hapo zamani vilikuwa na amani.<sup>22</sup>

Hali hiyo iliendelea. Uchaguzi wa mwaka 1961 ulikumbwa na mapigano kwa siku kadha, na idadi rasmi ilionesha kuwa waliokufa walikuwa 68, waliojeruhiwa 381 na zaidi ya 1,000 walikamatwa: nyumba nyingi ziliharihiwa na iliripotiwa kuwepo kwa uporaji mkubwa.<sup>23</sup>

Uchaguzi wa 1995, wa kwanza baada kurudishwa tena mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, nao pia ulikuwa na vurugu na kwa wakati huo ulielezewa kuwa ndiyo kilele cha vurugu za kisiasa Zanzibar.<sup>24</sup>

Mabishano kuhusiana na uchaguzi wa mwaka 1995 yalianza wakati wa uandikishaji, kwa kumtaka Mzanzibari mpiga kura kuwa mkazi katika eneo lake kwa kipindi cha miaka mitano. Wote CCM na CUF walijaribu kuwapinga wasiandikishwe wapiga kura waliodhaniwa kuwa ni wa chama pinzani.<sup>25</sup> Matatizo mengine yalijitokeza wakati wa kupiga kura. Juu ya malalamiko yaliyotolewa kwa maandishi kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) na vyama vyote viwili kuhusiana na kasoro zilizojitokeza,<sup>26</sup> ZEC

---

21 Ibid., uk.130

22 Ibid., uk.129-130

23 Ibid., uk.132

24 Ibid., uk.157

25 Ibid., uk.148

26 Ibid., uk.149

ilikitangaza CCM kuwa mshindi kikiwa na viti 26 na kufuatiwa na CUF kikiwa na viti 24 katika Baraza la Wawakilishi (HoR), na kwa uchaguzi wa Rais, Dk. Salmin Amour wa CCM alipata asilimia 50.2 % akifuatiwa na Seif Hamad wa (CUF) aliyepata asilimia 49.8%, tofauti finyu ya asilimia 0.4%. CCM aliunga mkono uamuzi wa ZEC. Matokeo hayo yalipingwa kila upande. Waangalizi wa uchaguzi wa kujitegemea walielezea uchaguzi huo kuwa na dosari<sup>27</sup> na wafadhili walilalamika kuhusu dosari zilizokuwepo kati ya tarakimu za ZEC na zile za katika vituo vya kupigia kura.<sup>28</sup> CUF kiliyapinga matokeo hayo ya uchaguzi kwa sabu ya matokeo hayo kuchezeza na ‘Tume ya Uchaguzi iliyochukua msimamo wa kichama’ kwa kukipendelea CCM. Baada ya uchaguzi pametokea ukatili na uhasama mkubwa kati ya vyama viwili hivyo. Mwezi Oktoba, hali ilikuwa tete, ikiambatana na vitendo vya vurugu na wapinzani kunyanyaswa. Hali ilizidi kuwa mbaya kwa kukamatwa na kushtakiwa kwa uhaini wanaharakati 18 wa CUF, pamoja na wajumbe wanne wa Baraza la Wawakilishi mwezi Novemba 1995.<sup>29</sup> Matokeo yake ni kuwa nyumba zilichomwa moto, watu walifukuzwa kizini kinyume cha sheria, wanafunzi walizuliwa kwenda shule na vyuoni, watu wakichapwa viboko ovyo na polisi barabarani, na vyombo vya dola viliwanyanyasa watu walioaminika kuwa ni wapinzani.<sup>30</sup> Hali hii ya kikatili na ya ukandamizaji dhidi ya upinzani ililalamikiwa kitaifa na kimataifa, na kulazimisha kuwepo kwa usulihisi wa mgogoro huu na matokeo yake ni *Muafaka I*.<sup>31</sup>

---

27 Ibid., uk.150, 156-7

28 Ibid., uk.150

29 Ibid., uk.157

30 Ibid., uk.152

31 Ibid., uk.157

## **Muafaka I na II: Muhtarasi**

### **Muafaka I**

Makubaliano kati ya CCM na CUF yalifikiwa baada ya uchaguzi wa 1995 na yalisimamiwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Chifu Emeka Anyaoku, ambaye alimkabidhi Dk. Moses Anafu kazi ya kuendesha mchakato wa kutafuta makubaliano hayo. Sababu yake ilikuwa ni vurugu na unyanyasaji uliofuatia upinzani dhidi ya ushindi wa CCM katika uchaguzi na uhasama mkubwa na hali ya wasiwasi iliyokuwepo kati ya CCM na CUF. Mchakato huo ulioanza mwezi Februari 1998 ulikuwa ni matokeo ya shinikizo la ndani na la kimataifa kumaliza hali ya ukatili na ukandamizaji.<sup>32</sup>

Kutokana na makubaliano hayo, pande mbili hizo zilikubaliana juu ya marekebisho kadha yakiwemo kuiimarisha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ili kuifanya iwe Tume huru isiyopendelea upande wowote; kuwepo kwa daftari la kudumu na kuaminika la orodha ya wapiga kura; kupitiwa tena kwa Katiba ya Zanzibar na sheria ya uchaguzi ilingane na hali ya sasa ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi; kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vinvyomilikiwa na serikali vinatenda haki kwa vyama vyote; kutengeneza mazingira huru kwa vyama vyote vya siasa kutangaza maoni yao na kutaka kuungwa mkono; mpango wa elimu kwa umma; kufanyiwa marekebisho mahakama ili kuifanya iwe huru na ya kiuledi; na kuwatendea sawa watumishi wa serikali kwa mujibu wa sheria.

Ijapokuwa pendekezo la awali liliridhiwa na CUF mwezi Julai 1998, CCM ilichelewa kufanya hivyo. Vile vile, mkataba ambao ulikuwa utiwe saini tarehe 15 Agosti 1998, ulitiwa saini mwaka mmoja baadaye tarehe 9 Juni 1999.<sup>33</sup>

---

32 Angalia J. Oloka Onyango na Maria Nassali, *Constitutionalism and Political Stability in Zanzibar: The Search for a New Vision*, Ripoti ya Tume ya Kutafuta Ukweli wa Mambo iliyoundwa chini ya usimamizi wa Kituo cha Katiba. Oktoba 2003, uk. 18

33 See Hamad & Peter, op. cit., uk.157

Hata hivyo, mkataba huo ulibaki kuwa ni wa maneno matupu. Hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa nia ya kisiasa. Sababu nyengine ya kutofanikiwa kwa mkataba huu ni kutokuwepo kwa utaratibu wa kuufwatilia na utekelezaji wake. Ilitolewa hoja vile vile kuwa haukuwa na nguvu ya kisheria na kutegemea nia njema ya vyama husika katika kuutekeleza – kamati ya vyama mbalimbali iliyoundwa kwa mujibu wa mkataba huu ilikuwa na hadhi ya kuwa mshauri tu na Jumiya ya Madola ni mdhamini wa huruma tu. Zaidi ya hayo, vyama vyote viwili CCM na CUF vilikuwa na wasiwasi na waendeshaji hao wa majadiliano.<sup>34</sup> Kwa hiyo Zanzibar iliingia katika uchaguzi wa mwaka 2000 bika ya ridhaa kamili ya vyama vikuu hivyo viwili. Kutofanikiwa kwa *Muafaka* 1 kulionekana wazi wazi kwa namna ya uchaguzi wa mwaka 2000 ulivyoendeshwa na matokeo yake ambayo kwa kiwango kikubwa yalionekana kuwa ni aibu pamoja na kuwepo kwa matukio kadha yaliyodhihirisha ukiukwaji wa matakwa ya usuluhishi ambayo *Muafaka* uliyataka.<sup>35</sup>

## **Muafaka II**

Kama ilivyoenezwa, machafuko ya kisiasa yaliendelea hadi uchaguzi wa mwaka 2000. Uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba 2000 ulionekana kuwa na dosari zaidi kuliko ule wa mwaka 1995. Ulielezwa kuwa ‘haukukamilika’ kwa kuwa haukufikia hatua yake ya mwisho kwa vile majimbo 16 hayakupiga kura kwa sababu ya tatizo la nyezo na vifaa. Kwa sababu hii, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ilitangaza kurudiwa kwa uchaguzi huo. Chama cha CUF kilikataa kushiriki katika kurudiwa huko kwa uchaguzi mpaka uchaguzi urudiwe katika majimbo yote ya Zanzibar na kutishia kuyakataa matokeo ya kurudiwa kwa uchaguzi ikiwa madai yao hayajakubaliwa.<sup>36</sup> Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliyapuuza madai hayo na uchaguzi ulirudiwa tarehe 5 Novemba 2000. CCM kilitangazwa kuwa mshindi na mara

<sup>34</sup> Oloka & Nassali, op. cit., uk. 19

<sup>35</sup> Ibid.

<sup>36</sup> Hamad & Peter, op. cit., uk.162

hii kwa asilimia kubwa Dk. Karume wa CCM akishinda kwa asilimia 67.04% na Seif Hamad wa CUF asilimia 32.96% kwa uchaguzi wa Rais na ushindi wa viti 34 kwa CCM na viti 16 kwa CUF kwa uchaguzi wa wabunge.<sup>37</sup> Matokeo ya CUF yalikuwa ni yale ya uchaguzi wa awali tu kabla ya kurudiwa kwa uchaguzi. CUF iliyakataa matokeo hayo na kukataa kuitambua serikali. Kiliitisha maandamano ya nchi nzima tarehe 26 na 27 Januari 2001, ili kupinga matokeo ya uchaguzi uliokuwa na kasoro na 'majimbo yaliyotengenezwa kwa kuipendelea CCM'. Serikali ilijibu matukio haya ya siku mbili kwa ukatili mkubwa. Kwa mujibu wa Tume ya Mbita iliyoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchunguza sababu na athari za matokeo ya tarehe 26 na 27 Januari. Katika matokeo hayo watu thalathini waliuliwa, ijapokuwa tarakimu zisizo rasmi ni marudufu ya idadi hiyo, mamia walijeruhiwa na kiasi cha watu 2,300 walikimbilia Shimoni, Kenya, hili likiwa ni wimbi la kwanza la Watanzania wengi kukimbilia nchi hiyo. Haya yalifuatiwa na wiki mbili za vipigo, ukamatwaji holele na aina mbali mbali za unyanyasaji dhidi ya raia wa kawaida.<sup>38</sup>

*Muafaka II* ulichochea na hayo yaliyoelezwa hapo juu. Mkataba huu ulikuwa ni matokeo ya sinikizo kwa CCM kutoka kwa wananchi wa kawaida, wasomi na wafadhili, Ni kutokana na uchaguzi wa mwaka 2000 na baada ya hapo.<sup>39</sup>

Masharti ya *Muafaka II* yalikuwa yanafanana na yale ya *Muafaka I* isipokuwa yale masuala yanayoihusu serikali. *Muafaka I* ulikuwa ni merekebisho ya ziada kwa *Muafaka II*. Kwa umahasusi hasa, *Muafaka II* ulitaka kufanyiwa marekebisho sheria ya uchaguzi ; kuundwa upya Tume ya Uchaguzi ya Zanzubar (ZEC) ili wawemo wajumbe wawili rasmi kutoka upande wa upinzani; kuanzishwa ofisi ya Mkurugenzi wa

37 Angalia *Zanzibar: 2000 Elections*, inayopatikana katika :<https://eisa.org.za/wep/zan2000election2.htm>

38 Oloka & Nassali, op. cit., uk.19

39 Ibid.

Kuendesha Mashtaka (DPP); kuwepo kwa mahusiano mema kati ya uongozi wa CCM na CUF; na kuzidisha fursa kwa vyama vya upinzani ya kuweza kuwafikia wanachama wake.<sup>40</sup> Kutokana na yale yaliyojiri katika kipindi cha *Muafaka I*, *Muafaka II* ulifanywa kuwa Sheria na Baraza la Wawakilishi (HoR) na kuigizwa katika Katiba ya Zanzibar ukiwa marekebisho ya 8 na 9 ya katiba.<sup>41</sup> Mara baada ya kutiwa saini, iliundwa Kamati ya Pamoja ya Usimamizi ya Rais (JPSC) ikiwa na wajumbe wa CUF na CCM ili kusimamia na kutekeleza makubaliano ya Muafaka huo. Ulipofika mwisho wa mwaka wa 2003, takriban asilimia 80% ya makubaliano hayo yalitekelezwa – ofisi huru ya Mkurugenzi wa Kuendesha Mashtaka ilianzishwa ili kuharakisha utoaji wa haki;<sup>42</sup> palikuwepo na mahusiano mazuri kati ya viongozi wa vyama hivyo viwili ambao waliwakilishwa kwa idadi sawa katika kamati ya vyama vyote na kuwa na utaratibu wa uwenyekiti wa pamoja; kadhalika, ilijengeka ari ya ujirani mwema miongoni mwa Wazanzibari walioelewa kuwa siasa za ushindani hazina maana ya kuchukiana; na ushabiki wa kisiasa na uonevu kwa wale walioaminika kuwa si watiifu kwa [chama tawala] na serikali ulipungua.<sup>43</sup>

Ijapokuwa Muafaka II ulitekelezwa vizuri zaidi ukilinganisha na *Muafaka I*, nao pia ulikuwa na matatizo yake. Lililo wazi ni kuwa haukushughulikia suala la kihistoria ambalo bado linaathiri hali ya kisiasa Zanzibar. Hayo ni masuala muhimu kama vile hadhi ya muungano, utawala, utawala wa sheria, uhusiano kati ya Unguja na Pemba, elimu pamoja na elimu ya uraia na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.<sup>44</sup> La muhimu kabisa ni kuwa haukujumuisha umma wote kwa jumla kwa kuwa

40 Ibid., p.xi, uk.20

41 Ibid., uk.20

42 Hamad & Peter, op. cit., uk.164

43 Oloka & Nassali, op. cit., uk, 21-22; na ibid.,uk.164-5

44 Hamad & Peter, op. cit., uk.164-5

ulihusisha vyama viwili tu CUF na CCM. Kwa jumla, watu wa Zanzibar hawakujumuishwa katika mijadala juu maelewano au jinsi ya kupatikana maelewano hayo; na Muafaka ulilenga kwenye mchakato wa uchaguzi na matokeo yake.<sup>45</sup>

Kwa kuwa hali ya kutoelewana kati ya serikali na upinzani Zanzibar iliendelea hata baada ya *Miafaka* miwili, hilo ndilo lililosababisha kuwepo kwa Muafaka III.

### ***Muafaka wa tatu***

Kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU) mwaka 2010 kulitanguliwa na mazungumzo kati ya CCM na CUF, ambayo yalianza tarehe 17 Januari 2007 Zanzibar. Kabla ya hapo, yalifanyika mashauriano yasiyokuwa rasmi kati ya washauri na wasaidizi wa Rais Kikwete na maafisa wa CUF kuanzia mwezi Desemba 2006, baada ya uchaguzi mkuu wa 2005, kwa madhumuni ya kuondoa mdororo wa kisiasa visiwani Zanzibar.

Mwezi April 2007, makatibu wakuu wa vyama hivyo viwili walikubaliana kumaliza mkutano huo tarehe 15 Agosti 2007. Hata hivyo, hilo halikuwa. Tarehe 14 Agositit 2007, Rais Kikwete alijitolea kuongoza mchakato huo yeye mwenyewe binafsi ili kuhakikisha kuwa unafanikiwa na mwisho wa mwezi Agosti, CCM iliwaomba CUF wawe na subira ili kutoa nafasi ya kufanyika kwa mkutano mkuu wa CCM na uchaguzi wa chama hicho mwezi November 2007 na umalizike kabla ya hatua ya mwisho ya mazungumzo kufanyika. Hii iliusukuma mbele mkutano wa mwisho kati ya vyama hivyo viwili ili ufanyike Bagamoyo tarehe 25 hadi 29 Februari 2008. Katika mkutano huu, vikundi vya kufanya mashauriano vya vyama vyote viwili vilikubaliana kuwasilishi yaliyokubaliwa kwenye vyombo vya kufanya maamuzi vya vyama vyao ili yaidhinishwe na kutiwa saini tarehe itakayokubaliwa.<sup>46</sup>

---

45 Oloka & Nassali, op. cit., uk.xi

46 Hamad na Peter, op. cit., uk.166-7

Mapendekezo ya mgawanyo wa madaraka yalikuwa ni pamoja na rais atoke kutoka chama kitakachoshinda; makamo wawili wa rais – makamo wa kwanza atoke kutoka katika chama kitakachoshika nafasi ya pili ya wingi wa viti na ambaye atakuwa msaidzi mkuu wa rais na makamo wa pili kutoka katika chama kitakachoshinda (chama cha rais), ambaye atakuwa na jukumu la kuratibi mawaziri wote na kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza la Wawakilishi. Kwa ufupi, makamo wa pili atachukua nafasi ya waziri kiongozi.<sup>47</sup> Ilipendekezwa pia kuwa liwepo baraza la mawaziri litakalokuwa na wajumbe kutoka chama kilichoshinda na vyama vilivyoshindwa kwa muiano wa wingi wao katika Baraza la Wawakilishi. Kwa kuwa muundo mpya wa serikali ulikuwa na madhumuni ya kuzuia matokeo ya vurugu baada ya kila uchaguai Zanzibar, CCM ilitaka mkataba uwe tayari na utiwe saina kabla ya uchaguzi wa 2010.<sup>48</sup>

Tarehe 17Machi 2008, Baraza la Utawala la CUF lilifanya kikao chake Zanzibar na kuuidhinisha mkataba. CUF pia kilitangaza hadharani matokeo ya mkutano katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kiwanja cha Demokrasia, Kibandamaiti. Hata hivyo, CCM ilikikosoa CUF kwa kutangaza hayo kabla ya muda na hivyo kukiuka taratibu kwa kuwa tangazo hilo lilitolewa kabla ya kikao cha Kamati ya Utendaji ya CCM (NEC) kukaa na kupokea ripoti kutoka kwa wawakilishi wa CCM. Pia, kauli hiyo iliyotolewa hadharani ilipasa itolewe na makatibu wakuu wote wawili baada ya vyama vyote kupokea na kuidhinisha ripoti za wajumbe wao.

Kufuatia matukio yaliyoelezwa hapo juu, mwezi huo huo CCM ilikutana Butiama. Iliyafanyia marekebisho mapendekezo yaliyotolewa na wawakilishi wa CUF na CCM na kupendekeza iwepo kura ya maoni ili watu wa Zanzibar waamue kuhusu muundo wa serikali unaopendekezwa. Sababu kubwa ya CCM kuwa na msimamo huu ni kuwa na mchakato shirikishi ambao utawajumuisha

---

47 Ibid., uk.171-2

48 Ibid., uk.171

Wazanzibari wenye mawazo na itikadi mbali mbali za kisiasa kushiriki katika mchakato huu wa kufanya maamuzi ya makubaliano mapya na kupata uungwaji mkono na wananchi wengi. Kiliamini kuwa kwa namna hii, yataepukwa makosa yaliyofanyika wakati wa *Muafaka II*<sup>49</sup> ambao ulivitenga vyama vingine vya siasa. CCM ilitilia mkazo pia haja ya mkataba mpya kulingana na katiba na sheria za Zanzibar na kwa hiyo ilitaka yafanyike marekebisho ya katiba kulingana na muundo mpya.

Chama cha CUF kiliyapinga kwa nguvu mapendekezo ya CCM ya kutaka iwepo kura ya maoni. CUF ilikituhumu chama cha CCM kwa kukiuka yale yaliyokubaliwa. Chama cha CUF kilitaka kuwa yale masuala waliyokubaliana na CCM yatekelezwe mara moja.<sup>50</sup> Chama hicho pia kilieleza kushitushwa kwake kwa kuwa katika kipindi chote cha miezi 14 ya majadiliano ambacho kilikuwa na vikao 21, CCM hakikuwahi kulitaja suala la kura ya maoni. Hata hivyo katika kipindi chote cha mchakato huu wawakilishi wa CCM walieleza kuwa si kama wamekuwa wakiwasiliana na Kamati Kuu (CEC) na Halmashauri Kuu NEC yao tu lakini wamekuwa pia na mawasiliano na maraisi wote wawili, Kikwete na Karume. CUF kilieleza kuwa hizo zilikuwa ni njama zilizoandaliwa mapema kabisa ili kukivuruga chama cha CUF na kitendo cha kulivuruga suala muhimu sana la kitaifa. Zaidi ya hayo CUF kilikituhumu CCM kwa kuingia katika makubaliano hayo bila ya nia thabiti ya kutatua mgogoro wa kisiasa na kuwepo kwa amani visiwani Zanzibar, ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwapotosha Watanzania na jumuiya ya kimtaifa. Walilichukulia hilo kuwa ni hila ya CCM ya kukishughulisha chama cha CUF na kurefusha mazungumzo hayo mpaka wakati wa uchaguzi ufike bila ya kulimaliza suala hilo. Kadhalika CUF kilishikilia kuwa CCM ingelilileta suala hilo wakati wa majadiliano na siyo kwa mlango wa nyuma. Hata hivyo, kwa

---

49 Huu haukuwa *Muafaka* wa kwanza Zanzibar. Mikataba miwili – *Muafaka I* na *Muafaka II* – ilitiwa saini kati ya CCM na CUF mwaka 1999 na 2001 mutawalia

50 Hamad & Peter, op. cit., uk.178

kuwa wote CUF na CCM walikubali kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na daftari la kudumu la wapiga kura vilikuwa na dosari zilizohitaji kurekebishwa, suala la nani angeliendesha kura hiyo ya maoni lilikuwa ni la wasiwasi kwa wote.<sup>51</sup> CUF kilieleza kukatishwa tama kwao kwa kile walichokiita udhaifu na utovu wa uaminifu wa Rais Kikwete akiwa kiongozi kwa kushindwa kukipinga chama chake juu ya kuwa alieleza hapo awali kwamba anakerwa na hali ya kutoelewana ya Zanzibar. Pia walimpinga vikali kwa kujishughulisha na juhudi za kuleta maelewano sehemu nyengine za Kenya na Cameroon huku akiyapuza ya Zanzibar.<sup>52</sup>

## Uchaguzi wa 2005

Wakati wa uchaguzi mkuu wa 2005 uliofuata *Muafaka II*, rais aliyekuwa madarakani, Amani Abeid Karume wa CCM, ilishinda uchaguzi kwa kura asilimia 53.2% , wakati Seif Hamad alipata asilimia 46.1%. Kwa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi, CCM kilishinda viti 30 wakati CUF kilishinda viti 19. CUF kilikataa kuutambua ushindi wa CCM na kutangaza mgomo usiokuwa na kikomo kwa Baraza la Wawakilishi.

## Maridhiano

Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliundwa baada ya mkataba wa masikilizano ambao uliitwa *Maridhiano* uliotiwa saini tarehe 5 Novemba 2009<sup>53</sup> kati ya aliyekuwa rais, Dk. Amani Abeid Karume, na katibu mkuu wa chama kikuu cha upinzani, CUF, Maalim Seif Sharif Hamad. Yaliyokuwemo katika makubaliano haya ya kistaarabu hayakutangazwa hadharani.<sup>54</sup> Matokeo ya kwanza ya makubaliano

51 Ibid., uk.172-4

52 Ibid., uk.175

53 Angalia Ali Uki, 'Maridhiano and the Government of National Unity, its impact on elections and constitutionalism in Tanzania', katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), katika *Zanzibar, The Development of the Constitution*, 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3, uk.235 ;

54 Angalia Yahya Khamis Hamad, 'The constitutional premises of the GNU in Zanzibar',

haya ambayo yaliwashangaza wengi yalikuwa ni CUF kumtambua Dk' Karume kuwa ni Rais wa Zanzibar, baada ya miaka tisa,<sup>55</sup> wakati baada ya uchaguzi wa 2005 CUF ilitoa tamko la kutomtambua kuwa ndiye mshindi wa uchaguzi huo.<sup>56</sup> Watu walikuwa na mawazo mchanganyiko kuhusu *Maridhiano*. Wote, wanachama wa CUF na wa CCM.<sup>57</sup> Matokeo yake yalikuwa ni kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mnamo kipindi cha mwaka mmoja, baada ya kazi kubwa ya kuwashawishi wanachama wa CCM na CUF kuwa serikali hiyo ilikuwa ni kwa maslahi yao.<sup>58</sup>

### **Marekebisho ya 10 ya katiba na kura ya maoni**

Kufuatia *Maridhiano*, iliwasilishwa hoja binafsi katika Baraza la Wawakilishi na Mhe. Abubakar Khamis Bakary iliyotaka kuridhiwa kwa mapendekezo ya *Maridhiano*, ambayo ni kuwa na kura ya maoni ili kuwaruhusu Wazanzibari waamue kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa; Sheria ya Uchaguzi Na. 11 ya 1984 ifanyiwe marekebisho ili kuipa madaraka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kusimamia kura ya maoni; na katiba ya Zanzibar ifanyiwe marekebisho ili kuruhusu marekebisho ya katiba yanayopendekezwa kuhusiana na Serikali ya Umoja wa Kataifa GNU.<sup>59</sup>

Bakary mwenyewe anaeleza kuwa mapendekezo hayo yalipitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja baada ya mjadala mkali katika Baraza hilo.<sup>60</sup> Anayaelezea marekebisho hayo kuwa ni pamoja na :

---

katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), katika *Zanzibar, The Development of the Constitution*, Ibid., uk.247

55 Chris Maina Peter, 'Recent developments in Zanzibar: From Miafaka to Maridhiano and Government of National Unity', katika *Zanzibar, The Development of the Constitution*, Ibid., uk.181

56 Hamad & Peter, op. cit., uk.171

57 Peter, 'Recent Developments in Zanzibar; op. cit., uk.181 na uk. 215

58 Ibid.

59 Ibid., uk.258

60 Abubaker Khamis Bakary, 'Challenges facing the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977 and the 10th Amendment to the Zanzibar Constitution 1984, katika

- Ibara ya 1 na ya 2 zinazoeleza kuwa Zanzibar ni nchi na ni moja ya nchi mbili huru zilizoungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Ibara ya 93 (3) inayoanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa;
- Kuanzishwa kwa vyeo vya makamo wa rais wawili kwa mujibu wa Ibara ya 39(2), na makamo wa kwanza wa rais akiwa mtu aliyependekezwa na chama kilichoshika nafasi ya pili katika uchaguzi wa rais;
- Ibara ya 42(2) inyoanzisha baraza la mawaziri la Baraza la Mapinduzi kulingana na uiano wa uwakilishi kwa idadi ya viti ambavyo kila chama imeshinda wakati wa uchaguzi mkuu ;
- Uteuzi wa wakuu wa mikoa (RCs) kufanywa na rais wa Zanzibar na siyo kama ilivyokuwa hapo kabla yaani kuteuliwa na rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushauriana na rais wa Zanzibar ; na Wakuu wa Mikoa (RCs) hawatakuwa tena wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa hivyo kuwa watumishi wa serikali tu bila ya kuwa na jukumu lolote la kisiasa kama ilivyokuwa hapo zamani.<sup>61</sup>
- Ibara ya 80 (A) (2) iliyotaka kuwepo kwa kura ya maoni.

Athari za marekebisho haya ni pamoja na kuingizwa katika katiba vipengele kadha kwa nia ya kuiimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa vipengele ‘ambavyo havitabadilishwa, havitapitiwa upya wala havitafutwa mpaka ifanyike kura ya maoni’. Athari nyengine ni kuwepo kwa Marekebisho 10 ya katiba ya Zanzibar na ulazima wa kuvifanyia marekebisho vipengele 14 vya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pamoja na kufutwa kwa baadhi ya vipengele huku vipengele vingine vikiwa havihitajiki, yote haya yakionesha haja ya ‘kuiandika upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ’ ‘ambayo imejaa viraka na mambo yenye utata’.<sup>62</sup>

---

*Zanzibar Yearbook of Law*, Juzuu ya 1, 2011, Zanzibar Legal Services Centre (ZLSC), Zanzibar, uk.296

61 Ibid.

62 Ibid., uk.297

Baada ya hapo, Sheria ya Kura ya Maoni ilipitishwa<sup>63</sup> ili kuwapa watu wa Zanzibar fursa ya kupiga kura na kuamua juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kura ya maoni ilifanyika tarehe 31 Julai 2010 na asilimia 66.4% ya wapiga kura waliikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa.<sup>64</sup> Utaratibu wa mgawanyo wa madaraka katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ulizungumzwa kwa upana na watu wa Zanzibar katika vyombo vya habari na katika semina mbali mbali kabla ya mswada haukujadiliwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi.<sup>65</sup> Mswada wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ulipitishwa tarehe 9 Agosti 2010<sup>66</sup> na kuridhiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi siku tatu baadaye tarehe 13 Agosti 2010, ukiwa Sheria Na. 9 ya 2010.<sup>67</sup> Kikao maalum cha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kilifanyika mwezi Agosti 2010 ili kuifanyia marekebisho katiba ya Zanzibar ya 1984 ili kuingiza Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa Rekebisho la Kumi.<sup>68</sup>

---

63 Sheria ya Kura ya Maoni Na. 6 ya 2010, Ibara ya 7(2)

64 Uki Ali, op. cit., uk.242

65 Ibid.

66 Gazeti Rasmi La Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *Gazetu Makhsusi, Sehemu ya CXIX Namba 6380*, 26 Agosti, 2010, uk.151 cited in Uki, Ibid., uk.243

67 Ibid, uk. 138, imechukuliwa katika Uki ibid.

68 Angalia Peter, ibid., uk.215-216

## Serikali Ya Umoja Wa Kitaifa 2010

---

### Maana, Ufafanuzi na Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa

Ikifafanuliwa, Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeelezwa kuwa ni serikali inayotokana na tukio ambalo vyama vikuu vyote vya siasa na wenye maslahi mbali mbali katika nchi kuwa ni sehemu ya mfumo wa serikali inayotawala. Serikali ya namna hii inasemekana kuwa hutokea pale penye mvutano wa kisiasa kuhusiana na chama kipi kiunde serikali baada ya uchaguzi kwa sababu ya matokeo ya uchaguzi yanayopingwa au kuwepo kwa upinzania wenye nguvu ambao hauwezi kuachwa nje ya serikali kama ilivyokuwa Afrika ya Kusini, au ikiwa ni njia ya kuwa na serikali inayojumuisha wote.<sup>69</sup>

Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar inaaminika kuwa ni ya aina ya pekee. Tofauti na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Kenya na ya Zimbabwe ambako kumetokea machafuko mara baada ya uchaguzi, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar ilitokana na mchakato wa kabla ya uchaguzi,<sup>70</sup> ijapokuwa si kwa maana ya kihistoria.

---

69 Hamad, op. cit., uk.247-248

70 Ibid. and Uki, op. cit., uk. 235

Uki anaifafanua Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa muktadha wa Zanzibar kuwa:

Ni serikali inayojumuisha wawakilishi wa vyama vya siasa vinavyoshinda kiti au viti katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni utaratibu wa kugawana madaraka wa vyama vya siasa vinvyopata viti katika chombo cha kutunga sheria. Chama cha siasa kisichokuwa na kiti katika chombo cha kutunga sheria hakiwezi kufurahia sehemu ya mkate huu.<sup>71</sup>

## Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa

### **Rais**

Kwa mujibu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, mtu anayeshinda kuwa Rais katika uchaguzi mkuu anakuwa kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mkuu wa serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.<sup>72</sup> Kwa mujibu wa sheria, rais hatolazimika kuchukua ushauri wa mtu yeyote katika kutekeleza kazi zake.<sup>73</sup>

### **Makamo wa kwanza na wa pili wa rais**

Chini ya rais wapo makamo wa rais wawili – makamo wa kwanza wa rais na makamo wa pili wa rais.<sup>74</sup> Hii imebadili muundo wa serikali iliyokuwepo kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ilikuwa na rais na waziri kiongozi. Makamo wa kwanza na makamo wa pili wa rais wanateuliwa na rais wa Zanzibar mnamo siku saba za kushika kwake madaraka.<sup>75</sup>

---

71 Uki, *ibid.*, uk.236

72 Angalia Ibara ya 26(1) ya Katiba ya Zanzibar ya 1980, kama ilivyofanyiwa marekebisha na Ibara ya 10 ya Sheria Na. 9 ya 2010

73 *Ibid.*, Ibara ya 52

74 Katiba ya Zanzibar ya 1984 kama ilivyofanyiwa marekebisha, Ibara ya 39 (1)

75 *Ibid.*, Ibara ya 39 (2)

### ***Makamo wa kwanza wa rais***

Makamo wa kwanza wa rais anateuliwa baada ya mashauriano na chama kinachoshika nafasi ya pili katika uchaguzi wa rais.<sup>76</sup> Ili kuweza kushika nafasi hiyo mtu lazima awe na sifa ya kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.<sup>77</sup>

Pale ambapo chama kinachoshika nafasi ya pili katika uchaguzi wa rais kitapata chini ya asilimia 10% ya kura zote katika uchaguzi wa rais au kama rais atagombea bila ya kupingwa, nafasi ya makamo wa kwanza wa rais itakwenda kwenye chama kitakachoshika nafasi ya pili kwa idadi ya viti vya majimbo yote ya uchaguzi katika Baraza la Wawakilishi.<sup>78</sup> Pale ambapo chama kitakachotakiwa kushika nafasi ya makamo wa kwanza wa rais kitashindwa kuwasilisha kwa rais jina la mtu atakayeteuliwa kushika nafasi hiyo mnamo siku saba za rais kushika madaraka, rais ataiwacha nafasi hiyo ibaki wazi na kuendelea kumchagua makamo wa pili wa rais.

Makamo wa kwanza wa rais ndiye mshauri mkuu wa rais<sup>79</sup> katika kutekeleza kazi zake na atafanya shughuli zote atakazopangiwa na rais.<sup>80</sup>

Ijapokuwa ni mjumbe wa baraza la mawaziri,<sup>81</sup> makamo wa kwanza wa rais si mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.<sup>82</sup>

### ***Makamo wa pili wa rais***

Makamo wa pili wa rais anateuliwa na rais miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika chama cha rais.<sup>83</sup> Kama makamo wa kwanza wa rais, makamo wa pili wa rais ni mshauri

---

76 Ibid., Ibara ya 39 (3).

77 Ibid.

78 Ibid.

79 Ibid., Ibara ya 39 (5)

80 Ibid.

81 Ibid., Ibara ya 43 (1)

82 Ibid., Ibara ya 39(4)

83 Ibid.

mkuu wa rais<sup>84</sup> katika utekelezaji wa kazi zake na ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Wote, makamo wa kwanza na makamo wa pili wa rais wanawajibika kwa rais kwa kipindi chote watakachokuwa madarakani.<sup>85</sup> Rais ana madaraka ya kuwafukuza makamo wa rais wote wawili<sup>86</sup> na kukitaka chama cha makamo wa kwanza rais kupendekeza mtu mwingine ili ateuliwe katika nafasi hiyo<sup>87</sup> mnamo siku 14 .

Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha azimio la kutokuwa na imani na makamo wa kwanza wa rais au makamo wa pili wa rais kama inavyoelezwa katika sheria.

Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa unaeleza ni nani wa kushika madaraka ya urais pindi nafasi hiyo inapokuwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu, maradhi au sababu nyengine ambayo itamfanya rais ashindwe kufanya kazi zake. Kwa hali kama iliyoelezwa hapo juu, makamo wa pili wa rais atashika nafasi ya urais, na kama atakuwa hayupo, Spika wa Baraza la Wawakilishi na kama atakuwa hayupo, basi ni Jaji Mkuu.

Pindi rais atakapokuwa hayupo Tanzania au kwa sababu nyengine yoyote ile, ataagiza kwa maandishi, yatakayo kuwa na maagizo mahasusi, kukabidhi kazi na shughuli za urais kwa makamo wa pili wa rais au, kama hayupo, kwa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi atakayeonekana anafaa. Ni wazi kuwa makamo wa kwanza wa rais hawezi kushika nafasi ya rais hata kwa muda.<sup>88</sup>

Ni dhahiri kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa inampa makamo wa pili wa rais madaka zaidi ukilinganisha na makamo wa kwanza wa rais.

---

84 Ibid., Ibara ya 39 (5)

85 Ibid., Ibara ya 39 (9)

86 Ibid., Ibara ya 40 (1) (c)

87 Ibid., Ibara ya 40 (2)

88 Uki Ali, op. cit., uk,241

## **Mawaziri**

Mnamo siku 14 za kuwateua makamo wa kwanza wa rais na makamo wa pili wa rais, rais kwa kushauriana na makamo wa rais wote wawili, atateua mawaziri miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kulingana na uiano wa viti ambavyo kila chama kimeshinda katika Baraza.<sup>89</sup> Hata hivyo, mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa haina mwongozo kuhusu mgawanyo wa wizara kwa chama tawala au upinzani. Hili hutegemea matakwa ya rais.<sup>90</sup>

Inapotokea kuwa makamo wa kwanza wa rais na au waziri kutoka upande wa upinzani atajiuzulu au itakuwepo nafasi iliyo wazi kwa zaidi ya siku 90 rais anaweza kuteua waziri mwingine ili kujaza nafasi hiyo.<sup>91</sup>

Inafaa izingatiwe kuwa utaratibu wa mgawanyo wa madaraka wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa uliishia kwa mawaziri na naibu mawaziri na mawaziri wasiokuwa na wizara maalum hawakuwemo.<sup>92</sup>

## **Uchaguzi Mkuu wa 2010 na Baraza la Mawaziri la Kwanza la Serikali ya Umoja wa Kitaifa**

Uchaguzi mkuu wa 2010 ulifanyika kwa amani tarehe 31 Oktoba. Kwa mara ya kwanza katika historia ya chaguzi za baada ya uhuru Zanzibar, chama cha CUF kiliyakubali matokeo na kukipongeza CCM kwa ushindi wake hata kama ulikuwa ushindi mwembamba – mgombea urais wa CCM Dk. Shein, alishinda asilimia 50.1% ya kura zote na mgombea wa CUF Seif Hamad alishinda asilimia 49.1%, wakati kwa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi, CCM ilishinda viti 28 na CUF viti 22. Kukubali matokeo kwa CUF kulitokana na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.<sup>93</sup>

89 Ibid., Ibara ya 42 (2)

90 Uki Ali, op. cit., uk.240

91 Ibid., Ibara ya 42 A

92 Hamad Khamis Yahya, op. cit., uk.265

93 Ripoti ya kikundi cha waangalizi cha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwenye uchaguzi mkuu wa Tanzania wa 2015. Uchaguzi mkuu wa Tanzania 18-29 Oktoba 2015. Ofisi ya

Baraza la Mawaziri la kwanza la Serikali ya Umoja wa Kitaifa lilikuwa na mawaziri 16 – tisa kutoka CCM na saba kutoka CUF. Katika mawaziri tisa hao, ni wawili tu ndio waliokuwa wanawake – mmoja kutoka kila chama. Walikuwemo manaibu waziri sita watano kutoka CCM na mmoja kutoka CUF. Miongoni mwa manaibu waziri sita, wanne walikuwa wanawake – watatu kutoka CCM na mmoja kutoka CUF. Walikuwemo vile vile mawaziri wasiokuwa na wizara maalum watatu, ambao wote walikuwa wanaume – wawili kutoka CCM na mmoja kutoka CUF.

Kama ilivyoielezwa hapo juu, Serikali ya Umoja wa Kitaifa imetoa madaraka kwa rais kuwateua makamo wa rais wote wawili na mawaziri wote. Baada ya uchaguzi wa 2010 rais na makamo wa pili wa rais walikuwa kutoka CCM, makamo wa kwanza wa rais kutoka CUF na baraza la mawaziri liligawiwa miongoni mwa vyama viwili hivyo. Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mara ya kwanza ilikifanya CUF, kuwa ndiyo chama kikuu cha upinzani, sehemu ya serikalit. CUF kilishiriki katika kufanya maamuzi ya serikali, tofauti na Bara ambako kilibakia kuwa kimoja ya vyama vikuu vya upinzani.<sup>94</sup> Juu ya haya inaaminika kuwa udhibiti wa CCM uliendelezwa chini ya Serikali ya kwanza ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu rais alitoka kutoka katika chama tawala. Yahya Hamad anaeleza kuwa, ijapokuwa baadhi ya mawaziri walitoka kutoka chama cha CUF, ‘kiutendaji walikuwa mawaziri wa serikali ya CCM’ – ‘ulikuwa ni mgawanyo wa “vyeo” tu na hivyo kuwafanya mawaziri kutoka upande wa upinzani kuwa ni vibaraka wa CCM’.<sup>95</sup>

Kuna hoja kubwa inayotolewa kwamba ijapokuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilipunguza mvutano wa kisiasa Zanzibar, lakini ilishindwa kuushughulikia mgawanyiko mkubwa uliokuwepo.<sup>96</sup>

---

Jumuiya ya Afrika ya Masharuki, Tanzania, 18 Januari 2016, uk.11

94 Khamis Bakary, *op. cit.*, uk.297

95 Angalia Yahya Hamad, *op. cit.*, uk.266

96 Angalia Throup David W., ‘Commentary: The political crisis in Zanzibar’, March 2016, imepatikana katika <http://www.csis.org/analysis/political-crisis-zanzibar>

Kushindwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kushughulikia mahusiano ya kimadaraka yasiyokuwa sawa kati ya Pemba na Unguja imeelezwa kuwa ni upungufu mmojawapo. Upungufu wa pili ni kutowaingiza watumishi wa serikali kuanzia ngazi ya katibu mkuu na kuteremka chini,<sup>97</sup> watu ambao labda wangelisababisha kuleta mabadiliko yaliyotarajiwa na kuimarisha ari ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Zaidi ya hayo ni ilani ya uchaguzi ya CCM ndiyo iliyotekelezwa chini ya Serikali ya awali ya Umoja wa Kitaifa; ilani ya uchaguzi ya CUF haikuwa na nafasi.<sup>98</sup>

Kwa kuwa ili awe na sifa ya kuwa makamo wa rais mtu ilimbidi apate si chini ya asilimia 10% ya kura zote katika uchaguzi wa rais, na kwa kuwa hakuna chama chochote isipokuwa CCM na CUF kilichoweza kufikia kiwango hicho, basi faida za Serikali ya Umoja wa Kitaifa zitakuwa ni kwa vyama vikuu viwili hivyo tu.<sup>99</sup> Kadhalika, imetolewa hoja kuwa kwa kuwa nafasi za uwaziri zinategemea uiano wa viti ambavyo kila chama kitashinda katika majimbo ya uchaguzi, ina maana kuwa vyama vingine vya siasa vimetengwa kabisa katika kupata uwaziri katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. La muhimu zaidi, imeelezwa kuwa ijapokuwa wananchi walishiriki katika kura ya maoni ya 2010 ili kuamua juu ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni CCM na CUF tu ndio waliopata fursa ya kuzungumzia muundo wake kufuatia mswada ulioletwa kwa hati ya dharura katika Baraza la Wawakilishi, na kwa hivyo kupunguza ushiriki wa wananchi. Ilipendekezwa kuwa katiba ipitiwe upya ili kuupanua muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa wadau wengi zaidi na siyo CCM na CUF tu, na hivyo kuruhusu ushiriki wa wananchi zaidi.<sup>100</sup>

97 YahyaHamad, op. cit., uk.267

98 Uki, op. cit., uk.245

99 Mussa Bakari Kombo, 'The state of constitutionalism in Zanzibar 2015', katika Mwesiga Baregu, *Annual State of Constitutionalism in East Africa 2015, 2016*, Kampala, Fountain Publishers, uk.255

100 Ibid., uk.256

## Kwa nini iwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa?

Wakati Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya 2010 inatokana na *Maridhiano* ya 1999, wakati tume ikifanyakazi, baadhi ya watu wameihusisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kipindi cha mapema zaidi. Hoja moja ni kuwa ijapokuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliundwa mwaka 2010, wazo la kuwa na serikali kama hiyo lilijitokeza katika ilani ya uchaguzi ya CUF ya mwaka 1995. Maoni mengine yanaihusisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kipindi cha kabla ya Mapinduzi. Maoni haya yanaeleza kuwa 'Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mjukuu', ambaye mizizi yake hasa ni *Muafaka* wa 1958 uliotiwa saina Ghana. Vyama viwili vilishiriki katika *Muafaka*, huu ambao ulishuhudiwa na mtu aliyetitwa Francis Khamis, Mkenya, na Karume Chume ??, mwenye asili ya Malawi. Mkutano wa Mbale uliofanyika mwezi April 1963 na kuandaliwa na Umoja wa Kupigania Uhuru wa Nchi za Afrika Mashariki na ya Kati (PAFMEACA) nchini Uganda, moja ya mambo yaliyokuwemo katika ajenda yake, pamoja na Shirikisho la Afrika ya Mashariki, lilikuwa ni suala la Zanzibar, ulizisuluhisha pande mbili hizo.

Wakati tume ikiwa kazini, wajumbe wa tume walisikia maoni mengi yanayokubaliana kuhusu sababu ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwanza, kwa wapiga kura ni historia ya vurugu na wasiwasi wa kisiasa uliokuwepo wakati wa uchaguzi Zanzibar. Waliohojiwa wengi wanakumbuka historia ya vurugu za uchaguzi Zanzibar tokea siku za ukoloni. Wamebainisha kuwa Wazanzibari walipigwa, waliwekwa ndani na kuuliwa katika mfululizo wa chaguzi. Vurugu za uchaguzi zilikuwepo tokea wakati wa uchaguzi wa mwaka 1961 na kufuatiwa na mvutano kati ya ASP na ZNP, uliosababisha kuundwa kwa serikali ya muda na marudio ya uchaguzi uliofanyika mwezi Juni. Tume ilielezwa juu ya matokeo sawa ya uchaguzi na uchaguzi uliporudiwa watu zaidi ya 1,000 walikamatwa na wengine kadha

waliuliwa. Machafuko haya yanaaminiwa kuwa ‘ndiyo mwisho wa fungate ya kisiasa kwa Zanzibar’.

Zaidi ya hayo, vurugu za uchaguzi zingeliendelea katika kila kipindi cha baada ya uchaguzi hadi cha uchaguzi mwengine kuhusiana na uchaguzi zote za 1995, 2000 na 2005. Uchaguzi wa 2000 ulionekana kuwa ni wa aina yake katika historia ya vurugu za uchaguzi za Zanzibar. Wakati wa uchaguzi huu iliripotiwa kuwa watu 35 waliuliwa na wananchi walifanyiwa vurugu kubwa. Lililokuwa la wazi kabisa ni kuwa kwa mara ya kwanza katika historia, Wazanzibari waliikimbia nchi yao wakiwa wakimbizi huko Shimoni, Mombasa. Inasemekana kuwa ulikuwepo wasiwasi mkubwa wa kisiasa na watu waligawanyika. Inaaminika pia kuwa hapo zamani vurugu za uchaguzi za Zanzibar zilisababishwa na udanganyifu katika uchaguzi ambao CCM kilidai ushindi. Waliohojiwa wengi waliamini kuwa historia yao ya vurugu zilizooneka katika fujo za wakati wa uchaguzi zilisababisha maafa yasiyokuwa na mwisho kwa Wazanzibari na hayo ndiyo yaliyowafanya viongozi wawili hao, aliyekuwa rais Abeid Karume na Maalim Seif Hamad Sheriff, kiongozi wa chama kikuu cha upinzani CUF, kuingia katika makubaliano yaliyozaa – *Maridhiano* na baadaye Serikali ya Umoja wa Kitaifa – ili kujaribu kumaliza hali hiyo ya kuhuzunisha. Zaidi ya hayo, tume ilielezwa kuwa, ‘hakuna kilichoandikwa lakini Maridhiano yalikuwa ni makubaliano ya kistaarabu yaliyotokana na miaka mingi ya mateso’.

Katika ngazi ya maandalizi ya kisiasa ya vyama, mvutano mkali wa kisiasa kati ya vyama vikuu viwili Zanzibar – CCM na CUF – ulikuwa na nafasi yake. Tume ilielezwa kuwa wananchi wa Zanzibar wamegawika nusu kwa nusu kuhusiana na ushabiki wa kisiasa, nusu wakikiunga mkono chama tawala cha CCM na nusu wakikiunga mkono chama cha upinzani CUF. Ushawishi wa CUF na CCM umethibitishwa kwa (kuangalia matokeo ya uchaguzi wa mwaka 1995 ambao vyama viwili hivyo viligawana baina yao asilimia 97%

ya kura na vyama vingine vikipata asilimia 3% tu), hii ikiwa ni sababu nyengine ya kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa hivyo, wakati wote pamekuwepo na tofauti finyu katika matokeo ya uchaguzi ya vyama viwili hivyo, tofauti ya asilimia – 1% kwa wingi, ambayo kwa mujibu wa baadhi ya waliohojiwa, imesababisha mgawanyo wa madaraka. Ule ushabiki ulio sawa kati ya CCM na CUF umekuwa ndiyo taswira ya kila wakati wa chaguzi za Zanzibar, taswira ambayo waumini wa maoni haya wanasema kuwa haiwezi kudharauliwa. Tofauti finyu kama hiyo inaweza kuwa ni sababu ya kutosha kwa aliyeshindwa kulalamika na kuyakataa matokeo. Baadhi ya watu ambao tume imewahoji, vile vile wamezihusisha vurugu za uchaguzi ambazo zimekuwa za kawaida visiwani na hali ya ushindani wa siasa zake. Kadhalika, Wazanzibari, katika kutafuta utulivu na amani wameamua kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuliko kuwa na serikali ya chama kimoja.

Zaidi ya hayo, kuna madai kuwa ‘Maridhiano yalikusisha CCM na CUF – Karume na Seif na vyama viwili ambavyo kihistoria vimetia mizizi’. Pamoja na hayo, CUF kimetambuliwa kuwa ni chama cha Zanzibar na ni chama pekee cha Tanzania ambacho makao makuu yake yapo Zanzibar. Hii inakifanya chama cha CUF kiwe juu katika jukwaa la siasa za Zanzibar. Historia ya vyama vyote viwili hivi imelazimisha kuwepo kwa mgawanyo wa madaraka na ndiyo maana imekuwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa undani zaidi, kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kumehusishwa na hali isiyokuwa ya kawaida ya mfumo wa jamii ya watu wa Zanzibar. Maoni haya yanadhani kuwa mchanganyiko wa watu wenye asili ya nchi mbali mbali wa visiwani lakini muhimu zaidi pia mgawanyiko wa kikabila miongoni mwa watu wa Zanzibar umelazimisha kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tofauti za kijamii kwa watu wa Zanzibar ni za kihistoria na kisiasa chini ya utawala wa Waarabu. Tume iliarifiwa kuwa chini ya utawala wa Waarabu Wazanzibari ‘wazawa’ walikandamizwa na kufanywa kama

watumwa. Ardhi kubwa ilimilikiwa na Wahindi wakati Waafrika hawakuwa na ardhi bali wakifanya kazi kwenye ardhi hiyo kwa ujira mdogo. Ilizidi kuelezwa kuwa wakati wa mdororo wa uchumi wa miaka ya 1930, wahindi wengi waliyakodisha mashamba yao kwa Waarabu ili kupata faida kubwa zaidi na hivyo kujenga dhana potofu kuwa ardhi hiyo ni yao. Waafrika walikuwa katika hali duni kabisa, wakifanyakazi ya kuwa (*vibarua*) kwa malipo ya chini kabisa. Inaelezwa kuwa huu ulikuwa ndiyo mwanzo wa kuibuka kwa matabaka katika jamii ya Zanzibar. Kama ilivyoielezwa kwa tume wakati ikiwa kazini: *Chini ya utawala wa kisultani, pamekuwepo na mgawanyiko kati ya mabwana na watwana tokea mwanzo*. Baada ya hapo mgawanyiko wa kikabila kati wa Waarabu na Waafrika ulianza. Inasemekana kuwa mgawanyiko wa kikabila ulizidishwa na sera za utawala usiokuwa wa moja kwa moja wa Wingereza, ambao waliutumia muundo wa madaraka uliokuwepo wa kuwapa uwezo Waarabu kuwabagua Waafrika. Vyama vya siasa vilianzishwa katika miaka ya 1950 kwa misingi ya kikabila. Mfano uliotolewa ulikuwa ni ASP, kilichoundwa na Waafrika na Washirazi kutoka Uajemi, na ZNP, kilichojumuisha Washirazi wenye asili ya Zanzibar na Waafrika. Kwa tofauti hizi mmoja miongoni mwa waliohojiwa alisema kuwa ‘ ZNP na ASP vilikuwa na sura ya kikabila’.

Mapinduzi ya 1964 yaliyoongozwa na Mwafrika aliyetitwa Okello mwenye asili ya Uganda, akisaidiwa na Wazanzibari wazawa, yaliwapindua Waarabu na kumwondoa Sultani. Inasemekana kuwa mapinduzi hayo yaliuzidisha mpasuko wa kijamii. Mgawanyiko wa kijamii ulizidi baada ya kurudishwa tena mfumo wa siasa ya vyama vingi mwaka 1992. Kuna hoja kubwa inayotolewa kuwa mgawanyiko wa kikabila bado unaendelea mpaka sasa na una athari kubwa kwa siasa za hivi sasa za Zanzibar. Kwa mantiki hii imeelezwa kuwa Wazanzibari ‘waliochanganya damu’ yaani Wazanzibari wenye asili wa Uarabu hivi sasa wanahusishwa na wakoloni wa Kiarabu na wanabaguliwa sana. Imeelezwa kuwa ubaguzi huu unatokana na imani

kuwa visiwa hivi vilimilikiwa na Wazanzibari wenye asili ya Afrika hapo awali. Kwa muktadha huu, baadhi ya waliohojiwa wameiona Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa ni mfumo utakaowajumuisha wote na kuwakusanya pamoja Wazanzibari wote bila ya kujali rangi au asili ya makabila yao.

Kwa misingi hiyo hiyo, yaliibuliwa masuala ya mfarakano mkubwa na hali ya kutokuwepo kwa usawa katika ngazi ya kimkoa kati ya Pemba na Unguja. Tume ilielezwa kuwa, hili pia ni la kihistoria. Tofauti zilielezwa katika pande mbali mbali. Kwanza, ni ukweli kuwa mapinduzi ya kihistoria ya mwaka 1964 yalitokea Unguja na la pili ni kwamba Unguja kwa desturi imekuwa ndiyo makao makuu ya serikali. Mambo haya mawili yanaaminika kuwa ndiyo yaliyotoa madaraka na kuzidisha kasi ya maendeleo kwa kuipendelea Unguja. Imeelezwa kuwa kuanzia wakati huo, watu wa Unguja wamekuwa na hisia za ukubwa na kujiona bora kuliko wale wa Pemba, na hili limesababisha ubaguzi wa aina fulani. Waliohojiwa walielezea kuhusu vitendo vya wazi vya kibaguzi kwa sababu za maeneo kati ya watu wa Unguja na Pemba. Yalitolewa malalamiko kuhusiana na matukio ya chuki katika sehemu za kazi dhidi ya wafuasi wa CCM huko Pemba. Taarifa zilizopatikana zinaeleza pia kuhusu ubaguzi mkubwa dhidi ya Wapemba katika ofisi za serikali. Tume ilielezwa kuwa kwa jumla Wapemba walijiririwa kwa kazi za ukarani. Ilielezwa kuwa *kivango cha elimu cha mtu hakikutiliwa maanani. Zaidi ya hayo ili mtu apate kazi ilimlazimu atoe kadi ya unanachama ya CCM.* Muhojiwa mmoja alielezea hali hiyo kuwa ni *aina ya ukaburu.* Walio vijana miongoni mwa waliohojiwa walieleza kuwa ubaguzi huu haukuwa kwa mujibu wa ushiriki binafsi ya kisiasa wa muhusika bali kwa mujibu wa historia ya kisiasa ya familia zao.

Inaelezwa vile vile kuwa ubaguzi dhidi ya Pemba uliwalazimisha wananchi wa Pemba kujijimarisha kisiasa ili kuepukana na kutengwa kwao kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa mujibu wa wahojiwa hao hao sababu hii hii ndiyo iliyowafanya Wapemba kukiunga mkono chama

cha CUF. Kwa mujibu wa hoja hii, tume imebaini juu ya imani ya wananchi wa Pemba kuwa chama cha CUF kimekuwa kikishinda katika chaguzi zote. Muhojiwa mmoja alieleza kuwa ‘ukiacha uchaguzi wa mwaka 2000 ambao chama cha CCM kilishinda viti viwili katika kata, tokea mwaka 1995 viti vyote vya Pemba vimekuwa vikichukuliwa na CUF’. Kwa mujibu wa baadhi ya wahojiwa, mpasuko mkubwa uliopo kati ya Pemba na Unguja, na hasa nafasi ya Pemba kuwa ndiyo ngome ya upinzani, ndiyo uliosababisha kuwepo kwa fujo zaidi za uchaguzi huko Pemba kwa miaka mingi ukilinganisha na Unguja.

Kwa upande mwengine, kuna jambo muhimu lililobainika kuwa Zanzibar imegawanyika katika makundi, siyo ya kisiasa bali ya – wale wanaounga mkono Mapinduzi na wale wanaopinga Mapinduzi, la kwanza likiyaunga mkono Mapinduzi ya mwaka 1964 na jingine likiyapinga na mpasuko huu umesadifu kuwa ni kati ya Pemba-Unguja na CCM-CUF. Inaaminika kuwa hii ndiyo sababu ya uhasama wa kudumu na siyo uhasama wa muda; na kuwa ‘hapajakuwepo na dalili ya mabadiliko ya mgawanyiko huu kabla, wakati wa au baada ya Mapinduzi; au kabla, wakati wa na baada ya utawala wa chama kimoja’. Hilo, kwa mujibu wa maoni haya ndilo lililoisababisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kujenga maelewano kati ya makundi mawili haya.

Tume imebaini kuwa Serikali ya Umoja wa Kitafa imebidi iwepo kwa sababu mvutano wa kisiasa, uhasama na kutoelewana kwa jamii miongoni mwa Wazanzibari kutoka pande zote mbili – CCM na CUF – umefikia mahali pabaya. Watu wamekosa subira. Juhudi za kuleta amani, ambazo ni *Muafaka I* uliosimamiwa na Jumuiya ya Madola tarehe 9 Juni 1999 na *Muafaka II* wa tarehe 10 Octoba 2001, ijapokuwa imeingizwa katika katiba ikiwa ni marekebisho ya 8 na ya 9 zimeonekana kuwa ni makaratasi matupu.

Katika nchi ambayo asilimia 95% ya wananchi wake ni Waisilamu na dini ambayo inahubiri umoja, wafuasi wa vyama mbali mbali

vya siasa hawasali pamoja ndani ya msikiti mmoja. Waumini wamekuwa wakiwaheshimu mashekhe waliokuwa na mawazo ya kisiasa kama yao tu – hawakuwa pamoja katika shughuli za kijamii. Tume imeelezwa kuwa katika kipindi hiki viongozi wa dini wamekuwa wakishambuliwa kwa tindikali kwa sababu za kisiasa. Biashara za wafuasi wa vyama kinzani ziligomewa. Wafuasi wa CUF hawakwenda kwenye maduka ya wafuasi wa CCM na kinyume yake. Muhojiwa mmoja alieleza kuwa: ‘Hawakuwa wakisafiri katika *dalla dalla* moja. Hawakuwa wakikaa pamoja, au kuhudhuria sherehe ya mfuasi wa chama kinzani au hata maziko ya mfuasi wa chama kingine.’ Pamekuwepo na habari za familia kutengana kwa sababu ya siasa. Ndugu wamekuwa hawasemeshani. Zaidi ya hayo, rangi za vyama ndizo zilizobainisha ufuasi wa vyama na hii ilikuwa hata kwa mavazi ya kawaida. Katika mikutano iliyoandaliwa na jumuiya za kiraia, washiriki walikataa kutumia makaratasi yenye rangi ambazo hazihusiani na vyama vyao. Huko Pemba mashamba ya mikarafuu yalichomwa moto.

Kutokana na hayo yalioelezwa hapo juu, tume ilibaini juu ya kuwepo kwa tofauti kubwa za hapa na pale za kijamii na kisiasa kati ya Wazanzibari, tofauti ambazo zinatofautiana na yale mawazo yaliyopo kuwa *tatizo la vurugu na utulivu Zanzibar lilijitokeza miezi michache tu kabla na baada ya uchaguzi, na linachochewa na vyama vya siasa siyo wananchi.*

Kwa maoni ya baadhi ya wahojiwa, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikiwa ni njia ya kuelekea kwenye usuluhishi wa tofauti za kisiasa na kijamii ziliopo, ulikuwepo ulazima wa kujumuisha wote. Kadhalika, baadhi ya wahojiwa walieleza kuwa baadhi ya makundi ya Wazanzibari walidhani kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaondoa mgawanyiko kati ya Pemba na Unguja. Ubaguzi na chuki za watu wa Unguja dhidi ya watu wa Pemba huenda zikasita. Kwa maneno mengine, palikuwa na matumaini kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itawaunganisha wananchi wa Zanzibar na kujenga mazingira ya

amani yatakayowawezesha kufanyakazi na kuishi pamoja. Msimamo huu umechukuliwa kutokana na dhana ya kile kilichodhaniwa kuwa ni mfumo bandia wa siasa ya vyama vingi ambao kwa ukweli ulikuwa ni utawala wa chama kimoja cha CCM – ambao umewanyima wapinzani nafasi ya kuchangia katika utawala wa nchi. Watetezi wa maoni haya waliambia tume kuwa baadhi ya Wazanzibari waliamini kuwa kwa kupitia Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ile siasa ya kuwa *mshindi huchukua kila kitu* itamalizika na upinzani ambao siku zote haukujiona kuwa ni sehemu ya mchakato wa maendeleo utakuwa na nafasi ya kushiriki katika serikali.

Kwa maoni ya wengine, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mchakato wa kimaumbile unaotokana na historia ya Zanzibar. Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilionekana kuwa ni matokeo yasiyoepukika ya hadhi ya Zanzibar kuwa ni nchi huru ambayo imekuwa sehemu ya Muungano baada ya mapinduzi ya 1964 – mapinduzi yaliyofanywa na wananchi na siyo watu wa kutoka nje, yaani Wabara na wageni. Kwa hali hiyo, Zanzibar ambayo ikijitawala wenyewe, wakati wote ingeliweza kufanya maamuzi huru kuhusu utawala wake nje ya mfumo wa Muungano. Kadhalika, watetezi wa maoni haya wanaiona Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa ni tukio la kihistoria linaloonyesha nafasi adimu kwa watu wa Zanzibar kufanya chaguo lao. Wanaitofautisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Muungano ambao Wazanzibari hawakupata nafasi ya kutoa maoni yao kama waliutaka au la. Kama baadhi yao walivyosema : ‘Hatukuulizwa ikiwa tunautaka Muungano.’

## **Nani na Nini Kilichowezesha Kuwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa**

Kuna maoni yaliyotolewa wakati tume ikifanyakazi yakidai kuwa ‘maoni ya kuwa na mtazamo wa namna moja yalitoka Washington’. Hata hivyo, waliohojiwa wengi wametoa shukrani zao kwa kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa uongozi na nia njema za wawu

wawili, aliyekuwa rais Abeid Karume na Seif Sharif Hamad wa CUF, ambao mapenzi yao ya kuwepo kwa Zanzibar ya amani, yenye utulivu na iliyobariki yaliwalazimisha kupatana na kufikia *Maridhiano*.

Viongozi wote hawa walikuwa na jukumu kubwa katika kuifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa itokee. Viongozi wawili hawa walikutana na vikwazo na iliwabidi wajitolee. Baadhi ya waliohojiwa waliisifu hasa nia njema ya Seif Hamad ambaye walisema kuwa alikubaliana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ijapokuwa iliegemea upande mmoja na kukipendelea CCM. Maoni kama hayo yalikuwa ni kwamba *Seif alijali sana, alielewa historia na wananchi, na alifanya juhudi ya kijasiri kuifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ifanye kazi*. Maoni mengine yanaeleza juu ya kujitolea kwa Seif juu ya kushinda uchaguzi wa 2010 kwa masharti kuwa awe rais wakati wa uchaguzi ujao: *Majadiliano kati ya Karume na Maalim Seif yalikuwa ya siri, hapana anayejua nini kilitokea. Kwa kuwa yalikuwepo makubaliano kwa mujibu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Seif alikubali asing'ang'anie ushindi wake na kilichokubalwa ni kuwa akubalwe kushinda mwaka 2015*.

Hata hivyo, wengine wanatambua jukumu na mchango wa Rais Karume. Akiwa ndiye Rais aliyekuwa madarakani, Rais Karume alionekana kuwa na kazi kubwa ya kuwashawishi watu wake katika serikali na katika CCM kuikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kazi ya Kamati ya Watu Sita wajumbe wake wakiwa Mhe. Hassan Moyo, Mhe. Mansour Yusuf Himid na Mhe. Eddy Riyami kutoka CCM na Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Salim Bimani na Mhe. Ismail Jussa kutoka CUF nayo pia ilitajwa. 'Kamati ya Waanzishaji', kama wengine walivyoita, pia ilipongezwa. Tume ilielezwa kuwa kamati hii ilifanyakazi chini kwa chini, ilifanya mikutano na kupambana na taratibu zilizokuwepo ili kuifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ifanyekazi.

Baada ya mazungumzo ya upatanishi na makubaliano ya kistaarabu kati ya Karume na Seif Hamad, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilibidi iwasilishwe kwa wananchi. Hili, kwa maoni ya watu

mbali mbali ambao tume ilikutana nao, lilifnywa liwezekane na watu mbali mbali. Baadhi ya waliohojiwa waliipongeza kazi iliyofanywa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, ambalo lilifanyia marekebisho katiba na kuwaruhusu wananchi wa Zanzibar kupiga kura katika kura ya maoni juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wengine wameyaeleza mafanikio ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa yanatokana na nia njema ya wananchi wa Zanzibar ambao kwa kupitia kura ya maoni –*kura za maoni*– waliuridhia mchakato huo. Kwa mujibu wa maoni ya mtu mmoja, wale asilimia ‘33% walioipinga Serikali ya Umoja wa Kitaifa wanaichukulia siasa kuwa ni kazi.’ Viongozi wa kidini na jumuiya za kiraia nao pia walipongezwa kwa kazi waliyoifanya. Inasemekana kuwa Mashekhe waliwaandaa na kuwashajiisha wafuasi wao kuipigia kura na kuiunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Waliandaa semina na makongamano mengi na kuyatumia majukwaa ya kidini vile vile ili kuwasilisha ujumbe, Unguja na Pemba. Kwa upande wao Jumuiya Zisizokuwa za Kiserikali za vijana zilipongezwa kwa kuitangaza Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa ni mradi wa kizazi kijacho.

Nia ya kisiasa ya aliyekuwa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, inasemekani kuwa ndiyo iliyokuwa muhimili katika uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Akiwa hafurahishwi na hali ya kisiasa ya Zanzibar – (*Mpasuko wa kisiasa ya Zanzibar*) – Kikwete alinukuliwa akiisema hali hiyo katika hotuba yake ya ufunguzi na kuahidi kuwa angeliishughulikia. Ni wazi kuwa ilikuwa wakati wa utawala wake ndipo ambapo *Maridbiano*, kura ya maoni na marekebisho ya katiba yaliyofuatia yalitokea bila ya kikwazo hapo Zanzibar. Mawazo hayo hayo kuhusu Kikwete ndiyo yaliyotolewa kuhusiana na mchakato wa kuifanyia marekebisho katiba. Mtu mmoja aliyehojiwa alitilia mkazo kuwa *watu walijua kuwa Kikwete alitaka kuipa uhuru Zanzibar*.

Hata hivyo, muhojiwa huyo huyo alieleza huku akiwa amevunjika moyo kwa kile walichokiona kuwa ni hali ya kushangaza kwa upande

wa Rais Kikwete kushindwa kusimama imara na kukamilisha mchakato wa kuipitia upya katiba mchakato ambao tume iliamini kuwa Wazanzibari wengi walitegemea kuwa ungeliyasuluhisha masuala muhimu ya demokrasia na utawala Zanzibar.

Ijapokuwa wananchi wa Zanzibar, kwa kupitia kura ya maoni waliikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Serikali ya Umoja wa Kitaifa imekuwa na maisha mafupi.

## Mafanikio na Changamoto za Serikali ya Umoja wa Kitaifa

### Mafanikio

Wanataaluma mbali mbali waliyaelezea mafanikio yaliyopatikana kwa haraka ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ya wazi kabisa yalikuwa ni amani na utulivu.<sup>101</sup> Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miongo miwili, uchaguzi wa mwaka 2010 ulifanyika katika mazingira ya amani na tokea wakati huo amani imekuwa ni kitu cha uhakika. Inasemekana pia kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliwaunganisha Wazanzibari ambao wakati wote walikuwa wamegawika kwa misingi ya kisiasa na kikanda.<sup>102</sup> Katika kusherehekea mwaka wa pili wa kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa tarehe 3Novemba 2012, viongozi wakuu watatu wa Zanzibar – Rais Ali Mohamed Shein, Seif Sharif Hamad na Seif Ali Iddi – waliungana na wananchi wa Zanzibar kuadhimisha amani na utulivu yakiwa ndiyo mafanikio makubwa ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.<sup>103</sup> Kukua kwa sekta ya utalii tokea kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa;<sup>104</sup> kuboreka

101 Angalia Yusuf Issa, 'Tanzania: Concerns over Zanzibar's Govt of National Unity', *Tanzania Daily News*, 31 October 2012, imepatikana katika <http://allafrica.com/stories/201210310157.html>

102 Hamad Khamis Mohamed, 'The state of constitutionalism in Zanzibar 2011', katika Makulilo B. Alexander (ed.), *Annual State of Constitutionalism in East Africa 2011*, Kampala, Uganda, Fountain Publishers, 2013, uk.201.

103 Yussuf Issa, op. cit.

104 'Zanzibar: Power-sharing mechanism proves successful', *The Citizen*, 21 January 2013,

kwa ustawi wa wananchi kwa sababu ya bei nzuri ya karafuu na mwani; kuongezwa mishahara watumishi wa serikali; kuzinduliwa kwa Mkakati wa Zanzibar wa Maendeleo na Kupunguza Umasikini (MKUZA 11); na kuongezeka kwa pato la mtu binafsi mwaka 2011 yote haya ni mafanikio ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.<sup>105</sup> Mafanikio mengine yaliyoletwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni pamoja na ruzuku ya Dola za Kimarekani milioni US\$40 kutoka Benki ya Dunia kwa Zanzibar ili kuendeleza upatikanaji na ubora wa elimu; kupitishwa kwa sheria ya kupambana na rushwa; kuundwa kwa Shirika la Viwango la Zanzibar; kuongezwa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu; na kuendeleza kilimo.<sup>106</sup>

Zaidi ya mafanikio yaliyoelezwa hapo juu ambayo yameandikwa ndani ya machapisho, tume ilielezwa manufaa mengine yaliyopatikana kutokana na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Baadhi ya munufaa yaliyoelezwa na waandishi mbali mbali yalithibitishwa kwenye mahojiano.

Ile kuwa wazo la Serikali ya Umoja wa Kitaifa halikuwa wazo la kutoka nje, hilo lilipongezwa kwa kuleta hisia za umiliki wa mchakato uliotoa fursa ya utekelezwaji wake. *Serikali ya Umoja wa Kitaifa halikuwa wazo lililopandikiwa kutoka nje na hii imesaidia katika utekelezwaji wake.* Mwamko mkubwa wa wananchi kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa tokea ‘wananchi walipoelimishwa juu ya serikali hiyo’ hilo pia lilishangiliwa. Baadhi ya wanawake wamekuwa na mawazo kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeinua ari ya ushiriki wa wanawake, vijana na Watu Wenye Ulemavu (PWDs) katika michakato mbali mbali ya kisiasa kwa kuanzishwa kwa viti maalum.

Hisia za jumla za wengi miongoni mwa wale ambao tume imezungumza nao zimethibitisha kuwa miaka mitano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kuanzia 2010 hadi 2015 ilikwenda vizuri. Wengi

---

imepatikana katika <http://unpo.org/article/15390>

105 Angalia Hamad Khamis, op. cit., uk. 202

106 Angalia UNPO news reports, inapatikana katika <http://www.unpo.org/article/15390>

wameeleza kuwa amani na utulivu ndiyo mafanikio makubwa ya Serikali hiyo. Wananchi wameeleza kuhusu utulivu serikalini na kuwepo kwa amani katika visiwa vyote viwili, na hasa wametilia mkazo kuwa pamekuwepo na utulivu Pemba, ngome ya CUF.

Wakielezea juu ya hali ya usalama, imethibitishwa kuwa *hapajakuwepo na kipigo kutoka kwa polisi, wala hapajakuwepo kamatakamata wala hapajakuwepo ubakaji. Haijakuwepo hofu. Ilikuwepo hali ya kuwepo kwa haki.*

Wengine wameeleza:

Chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapajakuwepo na kamata kamata, kutiwa ndani au kupigwa kwa wapinzani.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwa nzuri sana; kabla ya hapo watu wakiuliwa na nyumba zikichomwa moto.

Watu hawakuogopa hata pale waliposusia kitu; hapajakuwepo na vurugu.

Pamekuwepo na amani na usalama hata wakati wa uchaguzi – wakati ambao hapo zamani umekuwa na fujo na vurugu kubwa. Mtu mmoja aliyehojiwa alisema kuwa *watu walipiga kura na kwenda zao nyumbani kwa amani.*

Kwa jumla, watu walikuwa na utulivu na kujenga matumaini mema ya hali ya mambo. Kama mtu mmoja aliyehojiwa alivyosema: *Palikuwepo na hisia kuwa mambo buenda yakawa mazuri zaidi.* Kwa baadhi ya wanawake ambao tume ilikutana nao, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilileta matumaini kwa wanawake na walikuwa na mategemeo kuwa ingelikuwepo amani ya kudumu na utulivu.

Wengi walieleza kuwa uchaguzi wa kwanza kufanyika katika kipindi cha Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2010 ulikuwa ndiyo uchaguzi pekee katika kipindi cha muda mrefu ambao haukuwa na vurugu na ulifanyika kwa amani. Baadhi ya watu walithibitisha kuwa, juu ya kuwepo mambo fulani fulani wakati wa uchaguzi wa mwaka 2010, viongozi wa CUF waliyapuuza ili kutoa nafasi kwa mara ya

kwanza kufanyika uchaguzi ambao haukulalamikiwa na CUF na baadaye kuwepo kwa serikali iliyoongozwa na CCM-CUF. Tuhuma ya wazi iliyotolewa na idadi kubwa ya waliohojiwa ni kuwa Rais Shein alishindwa katika uchaguzi wa 2010 lakini kamati ya watu sita ilimbembeleza na kuweza kumshawishi Maalim Seif Hamad asiyapinge matokeo ya uchaguzi ili kuinusuru Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuepukana na kutokea kwa vurugu. Tume ilielezwa kuwa hapajakuwepo na unyanyaswaji wa wanasiasa wa upinzani na chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamekuwepo na mazingira mazuri ya kuendesha siasa. Maoni haya yalielezwa wakati mhojiwa akitoa maoni yake kwa tume: *Mtu aliveza kushabikia imani yake ya kisiasa kwa uhuru na kwa haki. Watu walijibisi kuwa wako sawa. Palikuwepo na hisia za umiliki.*

Maoni kadha yalitolewa kuhusiana na mazingira ya amani na urafiki yaliyokuwepo wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Moja miongoni mwa mambo yaliyoelezwa ni kuwa chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamekuwepo na mshikamani zaidi wa kijamii miongoni mwa wananchi. Wasiwasi na chuki miongoni mwa Wazanzibari kwa sababu ya tofauti zao za kisiasa vilitoweka. Mara baada ya kuundwa kwa Serukali ya Umoja wa Kitaifa mmoja wa waliohojiwa alieleza kuwa:

Pamekuwepo na sherehe mjini na mitaani. Sherehe hizo zilichukua mwezi mzima baada ya viongozi kukubali kungumza. Katika hali ya msisimko kama hiyo, inasemekana mtu mmoja alifariki katika mkanyagano. Wakimbizi wa Kizazibari kutoka Mombasa na wengine wengi kutoka Ughaibuni walirudi nyumbani baada ya muda mrefu.

Muhojiwe mwengine aliiambia tume kuwa sherehe za kusherehekea Mapinduzi ambazo zilifanyika mara baada ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa – ambazo huko nyuma zilikuwa zimetawaliwa na CCM – ziliwaleta pamoja watu wa aina mbali mbali kutoka vyama vya siasa mbali mbali. Ilisemekana kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilileta hisia za umoja na udugu kati ya watu wa Pemba na Unguja.

Mvutano kati ya vyama viwili vya siasa ulipungua vile vile. Ilisemekana kuwa vyama hivyo viliishi pamoja kwa amani. Tume ilibaini kuwa vikundi vya upinzani vya CCM dhidi ya CUF, vikundi ambavyo vilijitokeza mara baada ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, vilipotea taratibu. Zaidi ya hilo, pamekuwepo na kauli kuwa asasi za serikali zilifanya kazi vizuri zaidi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ilielezwa kuwa bila ya kuwepo kwa upinzani katika Baraza la Wawakilishi pamekuwepo na mvutano mdogo ndani ya Baraza hilo. Shughuli kati ya Serikali na wawakilishi wa upinzani ndani ya Baraza zilikwenda vizuri na kwa maendeleo. Kadhalika, ile kuwepo kwa idadi sawa ya nafasi za uwaziri kati ya CCM na CUF – saba na sita mutawalia – kumesababisha kuwepo kwa mahusiano mazuri katika kufanyakazi. Inasemekana kuwa yamekuwepo maridhiano mengi.

Nukuu za hapo chini zinajieleza:

Shughuli zilikwenda vizuri, kila mtu aliwakilishwa ndani ya serikali. Hapajakuwepo na uhasama. Baraza la Wawakilishi lilifanyakazi vizuri zaidi wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hali ilikuwa nzuri kwa vile watu walikuwa wakisemeshana.

Pamekuwepo na ushabiki mdogo wa kisiasa, upande wa upinzani na CCM walifanyakazi pamoja ndani ya Baraza la Wawakilishi, hapajakuwepo na mgawanyiko kati ya CCM na CUF . Hata Baraza la Mawaziri limekuwa likikaa pamoja bila ya kujali upande wa CCM au CUF.

Shughuli za Baraza la Wawakilishi zilikuwa bora zaidi, pamekuwepo na majadiliano yaliyochangamka na watu walinufaika kwa hayo. Kwa mfano, bajeti zilizoongezwa zilishughulikiwa; zilichambuliwa ndani ya Baraza la Wawakilishi bila ya kujali chama. Waziri kutoka CUF huhojiwa na Wawakilishi kutoka CCM na kinyume yake.

Hata wahojiwa waliohisi kuwa kutokuwepo kwa upinzani rasmi ndani ya Baraza la Wawakilishi kulidhoofisha ubora wa sheria na sera zilizopitishwa wakati huo, kwa jumla waliikubali hali hiyo ya ufanisi

kwa maslahi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kusema kweli, baadhi yao, waliipongeza hali ya usuhuba kwa misingi ya vyama ndani ya Baraza la Wawakilishi. Akielezea hisia za umoja zilizojitokeza wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, mhojiwa mmoja alizihusisha hisia hizo na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na msimamo wa pamoja wa Zanzibar wakati wa kuipitia upya katiba ya Muungano.

Jambo jingine lililodhihirika lilikuwa ni kupungua kuhusishwa na vyama vya siasa shughuli za utumishi serikalini wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Muhojiwa mmoja alieleza kuwa *wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ulikuwa ni wakati mzuri; hata polisi wakifanyakazi ya polisi na siyo kazi ya CCM; usalama wakifanya kazi yao na siyo CCM kufanyakazi ya usalama*. Iliaminika kuwa usawa kazini uliboreka sana. Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilionekana kuwa iliwapa fursa watu wa Pemba kuingia katika utumishi wa serikali tofauti na zamani walipokuwa wakibaguliwa sana.

Wahojiwa hao walieleza vile vile juu ya kuonekana waziwazi kwa hali ya kufufuka kwa uchumi visiwani. Walieleza juu ya kuongezeka kwa uwekezaji nchini wa wageni na Wazanzibari walio Ughaibuni, Ulaya na katika nchi za Kiarabu. Tume ilielezwa kuwa watu walilipa kodi na kwa hiari yao walichangia katika michango na shughuli za maendeleo. Muhojiwa mmoja alieleza kuwa kuwemo kwa CUF serikalini kulimaliza hujuma dhidi ya miradi ya serikali na kupungua kwa vitendo vya kuvunja sheria kwa upande wa wafuasi wa CUF. Baadhi ya wahojiwa, hasa wale wa Pemba, walieleza kuwa tofauti na wakati wa utawala wa chama kimoja cha CCM pale huduma za serikali zilipoelekezwa kwa wafuasi wa CCM, chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapajakuwepo na ubaguzi. Ilielezwa kuwa ilikuwepo miradi mingi ya kimaendeleo ya serikali, pamoja na miradi ya miundombinu ambayo ilipelekwa Pemba wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wafuasi wa vyama vyote CCM na CUF, walinnufaika na miradi ya serikali. Ilielezwa vile vile kuwa miradi iliyokuwa ikimilikiwa na wafanyabiashara wafuasi wa CCM Pemba ilibariki wakati wa Serikali

ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu wafanyabiashara wafuasi wa CUF ambao ndio wengi, walianza kufanyabiashara na wenzao wa CCM.

## Changamoto

Baadhi ya wanazuoni walieleza kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilianza kupata msukosuka muda mrefu kabla ya uchaguzi wa 2015. Inatolewa mifano miwili: Wa kwanza ni Kongamano la Vijana wa CCM lililofanyika tarehe 11 Januari likiwa ni moja ya shughuli za kuadhimisha Mapinduzi, ambapo mtoa mada mmoja aliipinga vibaya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Inasemekana kuwa kauli hiyo ilishangiliwa sana na vijana. Tukio la pili ni lile la wanachama wa CCM kukataa kumruhusu Makamo wa Kwanza wa Rais, Seif Sharif Hamad, kuingia katika Baraza la Wawakilishi wakati wa kulivunja Baraza la 8.<sup>107</sup> Kwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais si mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa mujibu wa kanuni za Baraza, wajumbe walitakiwa kuridhia kuhudhuria kwake katika shughuli za Baraza hilo kwa kupiga kura na wajumbe wa CCM walipiga kura dhidi ya hilo.

Zaidi ya changamoto zilizoelezwa na waandishi mbali mbali, baadhi ya pingamizi dhidi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa zilielezwa kwa wajumbe wa tume. Yalikuwepo madai kuwa tokea mwanzo zilikuwepo pingamizi dhidi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Palikuwepo na wasiwasi kuwa kuyakubali *Maridhiano* haukuwa mchakato rahisi. Lakini vile vile, inasemekana kuwa Rais Karume mwenyewe alikutana na vikwazo. Kwa kuwa alikuwa akimaliza awamu yake ya pili na ya mwisho akiwa madarakani na alikuwa yumo katika kutaka kuachia madaraka, hili, kwa maoni ya baadhi ya waliohojiwa lilimzuia asishiriki kikamilifu katika mchakato wa uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

La muhimu zaidi ni kuwa CCM Bara haikukubaliana na wazo la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Zaidi ya hilo, upinzani wa CCM dhidi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ulikuwa ni wa wazi na wa kuendelea.

---

107 Angalia Kombo, op. cit., uk. 254-5

Kwa mujibu wa mhojiwa mmoja, upinzani dhidi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa baadhi ya watu ndani ya CCM ulikuwa ni kwa sababu wapinzani hao hawakutaka kabisa mgawano wa madaraka. *Walitaka madaraka kamili. Ni wale wanachama wa CCM waliokuwa na msimamo wa wastaan tu ndio walioikaribisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa.* Kwa maoni ya wengine, kukataa kugawana madaraka kwa CCM kuko wazi kwa ile kutokuwepo na madaraka yoyote ya maana katika ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais waliyopewa wapinzani.

Kwa kuendeleza hoja hiyo hiyo, tume imeelezwa kuwa baadhi ya *masheba* (viongozi wa serikali za mitaa) na maafisa wa serikali walionesha upinzani wa waziwazi dhidi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, jambo lililomlazimisha Rais Karume awafukuze. Kusema kweli, baadhi ya waliohojiwa waliieleza tume kuwa viongozi hao walioipinga Serikali ya Umoja wa Kitaifa tokea mwanzo waliendelea kufanyakazi dhidi ya serikali hiyo. Jaribio la 2014 lililofanywa na kiongozi wa wakilishi wa CCM marehemu Salim Ujuzo, la kuleta hoja Katika Baraza la Wawakilishi kuikataa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lilishindwa. Mawazo mengine ni kuwa nyufa zilianza kuonekana ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa mara kabla ya Mkutano wa Katiba pale wajumbe wa CUF walipopendekeza kuwa wajumbe wa Zanzibar washiriki katika shughuli za Mkutano wa Katiba wakiwa Wazanzibari ili wazungumze kwa sauti moja badala ya kuwa wawakilishi wa chama kimoja kimoja, jambo lililotakiwa na CCM. Inasemekana kuwa tofauti hiyo iliyachafua mahusiano ndani ya Baraza la Wawakilishi pale wawakilishi waliporudi kutoka katika Mkutano wa Katiba baada ya muungano wa wapinzani – Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) – kutoka nje ya Mkutano wa Katiba mwezi April 2014. Inaaminika kuwa wana CCM wanaoichukia Serikali ya Umoja wa Kitaifa wanaendelea kuipinga serikali hiyo hadi hivi sasa.

Yametolewa maoni kadha kuhusu hili. Baadhi ya wale wanaoipinga Serikali ya Umoja wa Kitaifa waliulaani mchakato uliopitiwa hadi kupatikana kwa serikali hiyo. Wanamkosoa aliyekuwa

Rais, Karume kwa mambo mbali mbali. Akiwa na hofu ya mgombea urais mwingine wa Zanzibar – Dr. Bilal ‘aliyekuwa tishio’ – tokea mwaka 2009, inasemekana kuwa Rais Karume aliyateka nyara majadiliano ya Butiama ya CCM-CUF na aliendelea kumwalika Seif kwa mazungumzo ya siri kile kilichoelezwa kuwa ni ‘kuizunguka CCM’. Katika hali hiyo hiyo, Karume alituhumiwa kwa yeye binafsi kuteua kamati ya watu sita (watatu kutoka CCM na watatu kutoka CUF) kamati ambayo ilifanya kampeni ya kuiunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa’ bila ya kukishirikisha chama. Kadhalika, iliaminika kuwa *wananchi hawakumwamini Karume wala hawakumwamini Seif wala hawakuuamini huo mchakato wenyewe*; na kuwa elimu kwa raia juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ingelichukua kiasi ya miaka minane na siyo miaka mitatu kama ilivyokuwa.

Wengine, ijapokuwa walidai kuiunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa, walipinga kuingizwa kwake katika katiba. Kinyume na imani kubwa ya kuilinda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuiingiza katika katiba, watetezi wa msimamo huu walipendekeza itungwe sheria ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu hakuna pahala popote duniani isipokuwa Zanzibar ambapo Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeingizwa katika katiba. Waliamini kuwa kuliko kuiingiza katika katiba sheria ingelileta mshikamano uliohitajika.

Maoni mengine yaliipinga moja kwa moja Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwa haikuwa na umuhimu na walipendekeza iondolewe moja kwa moja. Waliamini kuwa nia ya CUF chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kukiangusha CCM na siyo kufanya nacho kazi au kuwasaidia wananchi.

Hata ukiacha watu mmoja mmoja ndani ya CCM ambao hawakuipenda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tume ilibaini kuwa Serikali ya Muungano yenyewe haikuitaka Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *Hawakufurabishwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa*. Yalikuwepo malalamiko makubwa kuwa Serikali ya Muungano isingelipenda kuiona Zanzibar iliyoungana. Hoja iliyotolewa ni kuwa itakuwa

vigumu kuidhibiti Zanzibar iliyoungana. Kwa wahojiwa wengi, hii ndiyo sababu iliyoifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa isambaratike.

Udhaifu mwengine uliotajwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni utekelezwaji wake mdogo. Wengi walithibitisha kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilifanyakazi katika ngazi ya umakamo wa rais na uwaziri na katika Baraza la Wawakilishi. Kati ya nafasi za uwaziri 13 katika Serikali hiyo, saba zilikuwa ni kwa CCM na sita kwa CUF. Uiano huo huo ndio uliotumiwa kwa nafasi za naibu mawaziri. Isipokuwa kwa maoni ya watu wachache kuwa nafasi zilizokuwa chini ya kata, ikiwa ni pamoja na *masheba*, watumishi wake wengi walitoka upande wa upinzani, mawazo ya wengi ni kuwa, nafasi zote ambazo zilionekana kuwa ndiyo kiini cha shughuli za serikali, kama vile makatibu wakuu na wakurugenzi, ziliendelea kushikwa na watu wanaokiunga mkono chama tawala na wanazishikilia nafasi hizo hadi hivi sasa. Kwa hivyo, muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa haukutiririka hadi kwenye ngazi ya serikali ya mtaa wala haukufika chini kabisa kwenye mashina. Kwa mujibu wa maoni ya mtu mmoja, hii ni kwa sababu katiba inataja Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa jumla tu na haielezi kwa ufasaha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni nini. Maoni namna hayo hayo yalieleza kama ifuatavyo: *Serikali ya Umoja wa Kitaifa haikuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hasa kwa sababu ilijikita katika ngazi fulani tu. Kuna haja ya kufafanua kwa ufasaha zaidi katika katiba.* Kwa mujibu wa wale wenye maoni haya, Serikali ya Umoja wa Kitaifa 'lazima iwe ni pamoja na naibu mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu wakuu, masheha, wakurugenzi, spika na naibu spika'. Kusema kweli, jengine lililotegemewa ni kuwa CCM na CUF vilitakiwa vifanyekazi kwa ushirikiano hata katika ngazi ya jamii.

Kwa maoni ya baadhi ya wanachama wa chama cha upinzani CUF ambao walifanya mazungumzo na tume, maombi kadha ya CUF serikalini ya kuomba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ipanuliwe hadi kufika ngazi mbali mbali hayakusikilizwa, ijapokuwa kinatolewa kisingizio kuwa maombi hayo hayakuwa kwa maandishi.

Jambo jingine lililoonekana ni kuwa iliyokuwa ikitekelezwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwa ni ilani ya uchaguzi ya CCM. Ijapokuwa wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi, katika hotuba yake, Rais alieleza kuwa ilani za uchaguzi za CUF na CCM zitaoanishwa na ile iliyooanishwa ndiyo itakayotekelezwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa sababu hiyo, baadhi ya watu waliohojiwa na tume walieleza kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa isingeliweza kuyashughulikia masuala muhimu ya kijamii yanayowahusu Wazanzibari, kama vile kutengwa kwa Pemba na malalamiko ya jamii za Wazanzibari walio wachache kama vile Wahindi na Wakiristo ambao wanajihisi wametengwa. Kwa hivyo, kwa maoni ya wale wenye mtazamo huu Serikali ya Umoja wa Kitaifa ingelishughulikia matatizo mbali mbali ya kisiasa na kijamii. Kadhalika, imeelezwa kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa haikuwa na maslahi maalum yoyote kwa wanawake na vijana. Kusema kweli, kwa maoni ya wengi waliohojiwa, maslahi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa yalikuwa ni ya jumla tu. Ilisemekana kuwa badala yake, wanawake walitengwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwa hakuna hata mmoja aliyekuwa katika kilele cha madaraka. Kwa sababu hiyo, limekuwepo pendekezo kuwa zaidi ya marekebisha ya katiba na sheria kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lazima yawepo majadiliano ya wazi zaidi juu ya Serikali hiyo ili kujumuisha maoni yote, pamoja na yale ya makundi yaliyotengwa.

Wazo jingine ni kuwa ifanywe juhudi kubwa zaidi ya kuwaelimisha wale walio kwenye vyombo vya usalama juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili waelewe serikali hiyo vizuri zaidi na wasifanye yaliyo kinyume na serikali hiyo.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, utulivu wa kisiasa uliletwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ijapokuwa hilo lilipongezwa kuwa ni maendeleo chanya, kwa jumla pamekuwepo na malalamiko ya kutoridhika kwa baadhi ya Wazanzibari. Baadhi yao, hasa wale waliokitegemea CUF kuwa ni mkosoaji wa sheria na sera za serikali,

walihisi kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeviza hali ya kuwepo kwa upinzani uliochangamka. Walieleza juu ya kutoridhika kwao na namna sheria zilivyopitishwa wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wadau wakuu hawakuweza tena kuchangia katika sheria na sera. Vyama vya kiraia vya watu binafsi waliarifu tume kuwa wadau ambao si wa serikali hapo awali wakiutegemea upinzani wa CUF ambao kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa walichambua, walikosoa na kushinikiza kuwepo kwa sheria na sera pamoja na kuzifanyia marekebisho, sasa chama hicho kimekuwa sehemu ya serikali chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kufuata msimamo wa pamoja wa serikali hiyo. Mfano mzuri ni pale lilipotolewa pendekezo la kuboresha uuzaji wa karafuu. Tume ilibaini kuwa juu ya kuwa hapo awali kabka ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa chama cha CUF ndani ya ilani yake ya uchaguzi kilikuwa na pendekezo la kubadili sera ya serikali iliyokuwa na nia ya kuboresha uuzaji wa karafuu kwa kupitia watu binafsi, baada ya kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, CUF kiliungana na Wizara ya Biashara na Masoko, ambayo ililikataa pendekezo hilo kwa ari ya nipe nikupe. Katika hali hiyo hiyo, inasemekana kuwa Sheria ya Wafanyakazi wa Serikali na Sheria ya Haki za Wafanyakazi zilipitishwa bila ya mchango wowote kutoka katika vyama vya wafanyakazi. Kwa hivyo, kukosekana kwa upinzani katika Baraza la Wawakilishi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kilikuwa ni kitu cha kusikitisha kwa baadhi ya watu. Kwa wale wanaoikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hii ilikuwa ni fursa iliyopotea kwa CUF kuitumia nafasi ya kuwemo kwao serikalini ili kuimarisha sera zao pale ambapo ilani ya pamoja haikuwepo.

# Uchaguzi wa 2015 na Kurudiwa Kwa Uchaguzi wa 2016

---

## Uchaguzi wa 2015

Uchaguzi mkuuu ulifanyika Zanzibar tarehe 25 Oktoba 2015 na ilikuwa ni kwa mara ya tano tokea kurudishwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Uchaguzi huo ulitanguliwa na mchakato usiokamilika wa kuipitia upya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ulianza mwaka 2011 kwa kupitisha Sheria ya Kuipitia Upya Katiba na kuteuliwa Tume ya Kuipitia Upya Katiba (CRC) mwezi April 2012. Tume ya Kuipitia Upya Katiba ilitayarisha rasimu ya katiba kwa mujibu ya maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wadau mbali mbali kufuatia mchakato uliokuwa wa uwazi, jumishi na shirikishi. Rasimu ya katiba, iliyosifiwa kuwa ni ya maslahi kwa wananchi, iliwasilishwa kwa Rais mwezi Disemba 2013. Palitokea kutoelewana wakati wa Bunge la Katiba na kutoelewana huko kulisababisha upande wa upinzani chini ya Umoja wa Kuilinda Katiba ya Wananchi (UKAWA) ujioe katika mchakato huo mwezi April 2014 baada ya kukituhumu chama tawala cha CCM kuwa kimeuteka nyara mchakato huo na kudharau maoni ya wananchi. Katiba iliyopendekezwa ilipitishwa tarehe 2 Oktoba 2014 bila ya kuwepo kwa upinzani. Juu ya kuwa ilipitishwa, Katiba pendekezwa haikuridhiwa kwa kuwa kura ya maoni iliyokuwa ifanyike 2015

iliahirishwa na kufa kabisa. Tume ya Kupitiya Upya Katiba ilifuata kalenda ya uchaguzi na kusababisha kuwepo kwa muda mfupi zaidi wa kufanya kampeni wa siku 64 badala ya siku 90 zilizoelzwa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015.<sup>108</sup> Kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, uchaguzi wa 2015 uliendeshwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na ulikuwa wa kuzipigia kura nafasi tano: rais wa Zanzibar, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, madiwani, raisi wa Muungano na wajumbe wa Bunge la Muungano.

Waliandikishwa wapiga kura wapya 64,770, na kupita idadi iliyotarajiwa ya 50,000, na kufanya jumla ya wapiga kura kuwa 503,860.<sup>109</sup> Vyama vya siasa Kumi na nne viliveka wagombea kwa uchaguzi wa rais. Hata hivyo, ushindani mkubwa ulikuwa kati ya CCM na CUF.<sup>110</sup> Jumla ya wagombea 180 waligombea viti 54 vya Baraza la Wawakilishi na wagombea 354 waligombea nafasi katika Serikali za Mitaa ili kuwa madiwani.<sup>111</sup>

Juu ya kujitokeza wapiga kura wengi wakati wa kujiandikisha, ripoti zimeandika masuala machache kuhusiana na uchaguzi. Kwanza pamekuwepo na vurugu za hapa na pale zilizotokea Unguja Kusini, pamoja na wapiga kura wa CUF kukataliwa kupewa vitambulisho vya Zanzibar (ZAN IDs).<sup>112</sup> Hili liliilazimisha CUF kuwasilisha hoja ya mjumbe binafsi katika Baraza la Wawakilishi tarehe 30 Machi 2015 ili kudai haki ya kupatiwa vitambulisho. Hoja hii ilikataliwa kwa kauli moja na wajumbe wa CCM na kusababisha kuwepo kwa wasiwasi kati ya CUF na CCM; hoja hiyo ilipokataliwa tena pale ilipowasilishwa tena katika kikao kilichofuata. CUF kiligomea vikao

108 Angalia EAC Observer Mission Report, op. cit., uk.13-14

109 Angalia Kombo, op. cit., uk.241; Angalia vile vile *European Union Election Observation Mission, United Republic of Tanzania, Final Report, General Elections 2015*, p.5. Idadi hiyo hiyo ya wapiga kura inaelezwa kuwa ndiyo idadi rasmi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika *Election Observation Mission, Zanzibar 2015*, Friedrich Nauman Stiftung, imepatikana katika <http://www.scribd.com/document/289609067/Report-Zanzibar-2015>

110 Kombo, Ibid., uk.245; EU EOM Report, Ibid., uk.5

111 EU EOM, Ibid.

112 Kombo, op. cit., uk.242

vya mwisho vya Baraza, pamoja na kikao cha rais kulivunja Baraza tarehe 26 Juni 2015.<sup>113</sup>

Tume ilielezwa pia juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika kijiji cha Tumbatu wakati wa uchaguzi pale vikosi vya wanamgambo wa serikali na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) walipokivamia kijiji na kuwachukua wanakijiji siku ya usiku wa kuamkia uchaguzi. Hali hii ilielezwa ifuatavyo:

Watu walikuwa wakilia pale walipokuwa wakichukuliwa na kutelekezwa porini. Watu waliopigwa walikuwa ni wapinzani, nguvu kubwa ilitumika wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi. Chama tawala kilitumia nguvu na vitisho dhidi ya wapinzani.

Ugawaji wa majimbo mapya ya uchaguzi lilikuwa ni eneo jengine la ushindani. Zoezi hilo lilishuhudia kuongezeka kwa idadi ya majimbo ya uchaguzi kutoka 50 (28 Unguja na 22 Pemba) hadi kufikia 54, majimbo manne ya ziada yakiundwa Unguja tu.<sup>114</sup> Ijapokuwa zoezi hili lililingana na sheria, wasiwasi ulikuwa ni wakati lilipofanyika. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina madaraka ya kuipitia upya mipaka ya majimbo ya uchaguzi katika kipindi cha miaka minane hadi 10 na kuyaongeza hadi kufikia 55 na si chini ya 40 pale inapotokea kuhesabiwa watu au kuwepo kwa mabadiliko ya kiutawala kuhusiana na mipaka ya kiutawala. Hali zote mbili hizi zilitokea. Watu walihesabiwa mwaka 2012 na mipaka ya kiutawala ilirekebisha kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Tawala za Mikoa mwaka 2014. Hata hivyo, zoezi hili lilifanyika mwezi Julai, miezi michache kabla ya uchaguzi, pale baadhi ya vyama vilipokwisha maliza uchaguzi zao za ngazi za chini kulingana na katiba ya zamani. Chama cha CUF kilimaliza mchakato huu mwezi June lakini ilibidi kipate wagombea kwa majimbo mapya yaliyoundwa.<sup>115</sup> Lalamiko jengine ni kuwa mipaka mipya

---

113 Ibid., uk.243

114 Ibid., uk.244; EU EOM, uk.6

115 Kombo, ibid.

haikuzingania kanuni ya mgawanyo sawa ya wapiga kura.<sup>116</sup> Zaidi ya hayo, kuchelewa kuwekwa mipaka mipya, pamoja na kuwepo mipaka mipya yenye dosari kulivifanya vyama vya siasa vishindwe kuainisha wapiga kura wao waziwazi kwa sababu ya kampeni na wapiga kura kushindwa kutambua wamo katika jimbo gani la uchaguzi.<sup>117</sup>

Ripoti zinaeleza kuwa kampeni za uraisi kwa jumla zilikuwa za amani. Wagombea urais wa CCM na CUF walifanya kampeni za 'kistarabu'.<sup>118</sup> Siku ya Uchaguzi takriban vituo vyote vya kupigia kura vilifunguliwa kwa wakati, taratibu za ufunguaji vituo zilifuatwa na upigaji kura ulifanyika katika hali ya utulivu.<sup>119</sup>

Kwa jumla, uchaguzi mkuu ulifanyika kwa amani.<sup>120</sup> Waangalizi wa uchaguzi mbali mbali (wa kigeni na wa hapa nchini), wakiwa ni pamoja na Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) na Umoja wa Taasisi za Kiraia za Tanzania za Kuangalia Uchaguzi (TACCEO), walithibitisha kuwa uchaguzi ulikuwa huru na wa haki.<sup>121</sup>

Kura zilianza kuhesabiwa mara baada ya upigaji kura kumalizika. Wasimamizi wa uchaguzi walijumlisha matokeo ya uchaguzi na vyeti vya uchaguzi vilitolewa kwa wagombea wote waliochaguliwa kuingia katika Baraza la Wawakilishi. Hesabu ya mwisho ya matokeo ya uchaguzi wa rais ilifanywa mbele ya wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na wakala wa kuwakilisha kila chama kilichogombea uchaguzi.<sup>122</sup> Tume ya Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Ulaya (EU EOM) ilieleza kuwa matokeo yaliyothibitishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar yalitangazwa mfululizo katika vituo vya kuhesabu kura na fomu nyingi za matokeo walizokuwa nazo

116 Ibid.; angalia pia EU EOM Report, uk.6

117 EU EOM Report, ibid., uk.6

118 Ibid., uk.7; Kombo, op. cit., uk.245

119 EU EOM, ibid., uk.8

120 Ibid., uk. 7; angalia pia Kombo, op. cit., uk.246

121 Kombo, ibid., uk.247; angalia pia EU EOM Observer Report, EAC Observer Report, uk.21

122 EU EOM Report, uk.8

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar zililingana na zile walizokuwa nazo mawakala wa vyama.<sup>123</sup>

Hata hivyo, ilipofika jioni ya tarehe 27 Oktoba, vikosi vya usalama vya Jeshi la Wananchi la Tanzania (TPDF), pamoja na vile vya Idara za Usalama za Zanzibar, viliwazuia watu kuingi na kutoka katika kituo kikuu cha kuhesabu kura, na kuwazuia kuingia hata watazamaji na wajumbe wengine wa kimataifa. Ruhusa ya kuingia na kutoka ilitolewa baada ya saa tano bila ya maelezo yoyote kutoka katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar au maafisa wa usalama. Ilipofika magharibi ya tarehe 27 Oktoba, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitangaza matokeo kutoka majimbo ya uchaguzi 31 kati ya majimbo 54 ya uchaguzi wa rais, na hapakuwepo na matokeo kutoka Pemba.<sup>124</sup> Ripoti ya Tume ya Waangalizi wa Umoja wa Ulaya ilieleza kuwa mchakato wa kuhesabu kura katika kituo kikuu cha kuhesabu kura cha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ulikuwa ni wa wazi katika siku mbili za mwanzo pale waangalizi walipoweza kuingia na kutoka katika kituo hicho, mpaka pale mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar alipoamua kuufuta uchaguzi wa Zanzibar tarehe 28 Oktoba.<sup>125</sup>

Kabla matokeo hayakufutwa, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilifanya mkutano wake wa faragha tarehe 28 Oktoba kufuatia uahirishwaji wa kutangazwa matokeo zaidi ya uchaguzi. Kufuatia hili, mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar aliondoka katika kituo cha kuhesabu kura. Makamo wa mwenyekiti alijaribu kuendelea na kuhesabu kura lakini alizuiliwa na kusindikizwa nje ya kituo na vikosi vya usalama. Baadaye, mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar alitangaza kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kuwa uchaguzi wa Zanzibar umefutwa.<sup>126</sup> Ilielezwa kuwa, ukiangalia tabia ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya kuunyang'anya ushindi

---

123 Ibid., uk.41

124 Ibid.

125 Ibid., uk.8

126 Ibid., uk.41

upinzani siku zilizopita, tukio la tarehe 28 Oktoba 2015 liliashiria kuwa hakuna kilichobadilika.<sup>127</sup>

Taarifa ya mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Bwana Jecha Salim Jecha, ilitolewa siku ya mwisho ambayo kisheria Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitakiwa kutangaza matokeo ya uchaguzi.<sup>128</sup>

Sababu kubwa ya kuufuta uchaguzi ni kuwa uchaguzi haukuwa huru na wa haki. Sababu zilizotolewa na mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar za kuamua kuufuta uchaguzi ni, kupiga kura mara mbili, udanganyifu na vyama vya siasa kuingilia kati mchakato wa kupiga kura.<sup>129</sup> Na la muhimu hasa ni kwamba imetuhumiwa kuwa kura zilizopigwa katika baadhi ya majimbo ya uchaguzi, hasa Pemba, zilizidi idadi ya wale walioandikishwa na kuwa katika baadhi ya sehemu masanduku ya kura yaliyokuwa na kura zilizokwishapigwa yalitolewa nje ya vituo vya kupigia kura, kinyume na Ibara ya 42(1) ya Sheria ya Uchaguzi Na. 11 ya 1984. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar pia alitangaza kuwa utakuwepo uchaguzi mwengine tarehe itakayoamuliwa.<sup>130</sup>

Ripoti ya Tume ya Waangalizi wa Uchaguzi ya Umoja wa Ulaya ilieleza kuwa sababu nyengine za kuufuta uchaguzi ambazo zilitolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni: kutokubaliana kati ya wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar; wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kushindwa kufanya kazi zao na badala yake kujifanya kama wawakilishi wa vyama; ukweli kuwa baadhi ya vyama havikuwakilishwa katika vituo vya kupigia kura vya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, hasa Pemba ambako idadi ya kura ilizidi ile ya wapiga kura walioandikishwa; masanduku ya kura kuondolewa vituoni na kura kuhesabiwa nje ya vituo; mawakala wa vyama, hasa wale wa chama cha TADEA, kuondolewa kutoka katika vituo vya kupigia kura na kupigwa; vituo vya kupigia kura kuvamiwa

127 Throup, op. cit.

128 Kombo, uk.246

129 EAC Observer Report, uk.33

130 Kombo, op. cit., uk.246

na vijana; kuzuiliwa kuingia na kutoka katika vituo vya kupigia kura; vyama vya siasa kuingilia shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kutangaza ushindi; malalamiko ya vyama mbali mbali vya siasa, vilivyoeleza kutoridhika na matokeo ya uchaguzi; na kuchezea tarakimu kwenye fomu za matokeo katika baadhi ya vituo vya kupigia kura, hasa Pemba.<sup>131</sup>

Juu ya kuwepo kwa shaka kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilipokea maagizo kutoka kwa Rais Shein na wakereketwa wa CCM Zanzibar au ilifanya hivyo kwa makubaliano na Serikali ya Muungano, ukimya wa Dares Salaam na Rais mpya Magufuli kukataa kuingilia kati hakukusaidia kitu.<sup>132</sup>

## **Yaliyotokea Kufuatia Kufutwa kwa Matokeo ya Uchaguzi**

### **Hisia za wadau mbali mbali**

Tarehe 29 Oktoba, waangalizi wa uchaguzi wa hapa nchini na wa kimataifa, pamoja na Tume ya Waangalizi wa Uchaguzi ya Umoja wa Ulaya, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Madola, walitoa taarifa ya pamoja ambayo walieleza wasiwasi wao juu ya kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi na kuiomba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kueleza kinaganaga ni katika vituo gani kulikotokea dosari na kuiomba iwe wazi kwa uamuzi wake wa kufuta uchaguzi.<sup>133</sup> Siku hiyo hiyo, mabalozi wa Umoja wa Ulaya na wa nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya waliopo Tanzania, Norway, Uswizi, Canada na Marekani walitoa taarifa ya pamoja wakisisitiza imani yao kuwa mgogoro wa kisiasa Zanzibar unaweza kusuluhishwa vizuri zaidi kwa suluhisho lililokubaliwa na wote na kumwomba Rais Magufuli kutumia nafasi

---

131 EU EOM Report, op. cit., uk. 41

132 Throup, op. cit.

133 EU EOM Report, op. cit., uk.8

yake ya uongozi ili kuhakikisha kuwepo kwa matukio ya amani na heshima kwa mchakato wa uchaguzi.<sup>134</sup>

Chama cha CUF na vyama vingine sita vidogo – Demokrasia Makini, Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMM), Sauti ya Umma (SAU), National Reconstruction Alliance (NRA), Jahazi Asili na Democratic Party (DP) – walizipinga sababu za kufuta uchaguzi na kueleza kuwa hazikuwa za msingi huku wakisisitiza kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ingelikuwa katika hali ya kuyashughulikia matatizo badala ya kuamua kuufuta uchaguzi.<sup>135</sup>

Mgombea urais wa chama cha CUF, Maalim Seif alitangaza kuwa chama chake hakitoshiriki katika marudio ya uchaguzi na kutoa muda wa saa 48- hadi kufikia tarehe 2 Novemba 2015 – mgogoro huo uwe umesuluhishwa. Hata hivyo, muda huo ulipita bila ya maendeleo yoyote.<sup>136</sup> Aliwataka wanachama wa CUF watulie na kuwasihi wasubiri matokeo ya mazungumzo kati ya wagombea urais wa CUF and CCM uliokuwa na nia ya kutatua suala hilo.<sup>137</sup> Msimamo wa CUF uliungwa mkono na UKAWA wakati CCM waliunga mkono uamuzi wa mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuufuta uchaguzi.<sup>138</sup>

Hatua iliyochukuliwa na mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilikuwa ni mada ya mjadiliano ya haraka na ya kufanyiwa uchambuzi kwa wanasheria na jumuiya za kiraia ndani na nje ya Zanzibar, na hasa uhalai wa kisheria wa uamuzi huo.<sup>139</sup> Chama cha Wanasheria cha Zanzibar (ZLS) na Chama cha Wanasheria cha Tanganyika (TIS) vilipinga kufutwa kwa uchaguzi kwa sababu hakuna sheria inayompa madaraka mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kufanya hivyo.<sup>140</sup> Hoja nyengine ni kuwa

134 Ibid., uk.9; EAC Observer Report, op. cit., uk.33

135 Kombo, op. cit., uk.247

136 Ibid.; na EU EOM Report, op. cit. uk,8

137 Kombo, ibid.

138 Ibid.

139 Ibid.; na EU EOM Report, uk.8

140 Kombo, ibid., uk.248

kauli hiyo ilikuwa ni ya mtu mmoja bila ya kuwepo kikao au azimio la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kinyume na Ibara ya 119 (10) ya katiba inayotaka kuwa uamuzi wowote wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar lazima uungwe mkono na mwenyekiti au makamo mwenyekiti na wajumbe wanne; na hata kama Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ingeliheshimu ibara hiyo, chombo hicho hakina uwezo wa kisheria wa kufuta uchaguzi kwani kura zilikwishapigwa, baadhi yake kuhesabiwa na kutangazwa, na njia pekee ya kusuluhisha hilo ikiwa ni kutoa siku tatu zaidi ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza na kutangaza matokeo.<sup>141</sup> Vyanzo vingine vilieleza kutokuwepo kwa kipengele chochote cha sheria kinachohalalisha kufuta uchaguzi wote.<sup>142</sup> Ijapokuwa ripoti ya Tume ya Kuangalia Uchaguzi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inanukuu Ibara ya 51(2) ya Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya 1984 kama ilivyofanyiwa marekebisha, kuwa inaipa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar uwezo wa kuahirisha uchaguzi pindi vikiwepo vikwazo vyovyote katika kufanya uchaguzi huo, inaifafanua ibara hiyo kwa kueleza kuwa madaraka hayo ni ya Mahakama Kuu kwa mujibu wa Ibara ya 117 na 118 za Sheria hiyo.<sup>143</sup>

## **Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuidhinisha kufutwa uchaguzi**

Tarehe 1Novemba, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilifanya mkutano na wajumbe wote wa tume na hatua ya kufuta uchaguzi iliidhinishwa kinyumenyume. Inasemekana kuwa mkutano huo uligawanyika sana kwa misingi ya vyama vya siasa – wajumbe wa CCM na mjumbe mmoja mwingine na mwenyekiti wakiunga mkono hatua hiyo kwa

141 Ibid., uk.248-9

142 EU EOM, op. cit., uk. 42

143 Angalia 'Election Observation Mission to the 20th March 2016 Re-Run General Elections in Zanzibar Statement, Zanzibar 21st March, 2016', imeambatanishwa na the *Report of the EAC Observer Mission to the 2015 Tanzania General Elections, 18-25 October 2015*, op. cit.

wingi wa kura nne huku wawakilishi wa CUF na makamo mwenyekiti wakipiga kura ya kuipinga hatua hiyo.<sup>144</sup>

Kwa tangazo la tarehe 6 Novemba 2015, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilichapisha taarifa ya kufutwa matokeo ya uchaguzi katika gazeti la serikali la tarehe 11 Novemba 2015. Uamuzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ulifanywa kwa mujibu wa Ibara ya 119 (10) ya Katiba, inayotaka kuwepo kwa akidi katika kuidhinisha uamuzi wowote wa tume hiyo; na Ibara ya 3(1) na 5(a) zinazoeleza kuwa kanuni zote, maagizo na matangazo ambayo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina madaraka ya kufanya itakuwa zimefanyika kihalali kwa idhini ya mwenyekiti au mkurugenzi wa uchaguzi na kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina madaraka ya kusimamia mchakato wote wa uchaguzi.<sup>145</sup> Tangazo hilo halikufafanua sababu za kufutwa kwa uchaguzi au madaraka ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya kufuta uchaguzi.<sup>146</sup>

### **Majadiliano kati ya CCM na CUF**

Tarehe 9 Novemba, yalianza majadiliano kati ya wagombea wakuu wa nafasi ya urais wa CUF na CCM, Maalim Seif Sharif Hamad na Dk Shein. Haya yalikuwa ni majadiliano ya kwanza ya mfululizo wa mikutano tisa juu ya uhalali wa uamuzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mikutano hiyo ilihudhuriwa vile vile na waliokuwa marais wa Zanzibar, Alhaji Ali Hassan Mwinyi na Dk Amani Abeid Karume, na makamo wa pili wa rais, Seif Ali Iddi. Ombi la CUF la kutaka mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar aitwe kwenye mkutano huo lilikataliwa na CCM kwa sababu hawakuwa na madaraka ya kumwita. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, ijapokuwa ndiyo msimamizi na mwendeshaji wa uchaguzi haikuhusika na

---

144 EU EOM, op. cit., uk.42

145 Ibid.

146 Ibid.

mikutano hii. Mikutano hii ilitanguliwa na mkutano kati ya Rais Kikwete na Seif Sharif Hamad tarehe 4 Novemba.<sup>147</sup>

Hata baada ya mikutano kadha, vyama viwili hivyo vilishikilia misimamo yao – CCM kikitaka uchaguzi mpya ufanyike, huku CUF kikishikilia kuwa kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi hakukuwa halali, kilipinga pendekezo la kufanya uchaguzi mpya na kutaka kura za uchaguzi wa rais zihesabiwe tena na matokeo kutangazwa.<sup>148</sup> Ijapokuwa mazungumzo haya yalitoa matumaini ya kufufuliwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2015, hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa kati ya vyama viwili hivi vya siasa.<sup>149</sup> Mikutano hii iliendelea hadi Januari 2016, lakini hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa. Tarehe 22 Januari, kabla ya mazungumzo kati ya pande mbili hizo hayakuhitimishwa rasmi, mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar alitangaza kuwa uchaguzi wa marudio utafanyika tarehe 20 Machi 2016. Makubaliano ya mikutano hii yalikuwa ni siri. Kusema kweli Tume ya Kuangalia Uchaguzi ya Umoja wa Ulaya ilieleza kuwa hili lilifanywa makusudi.<sup>150</sup> Tarehe 28 Januari, CUF kilitangaza rasmi kuwa hakitashiriki katika uchaguzi wa marudio.<sup>151</sup>

Ijapokuwa baadhi ya watu ambao tume hii ilizungumza nao waliitaja mikutano hii na kueleza kuwa haikuzaa lolote lakini ukweli kuwa hapana yeyote aliyeweza kueleza ni nini hasa kilichotokea kumethibitishia madai ya tume kuhusu siri ya mikutano hii. Baadhi ya waliohojiwa walieleza kuwa hizo zilikuwa ni juhudi za Maalim Seif. Hata hivyo, walilalamika kuwa Seif alikuwa ndiye mwanachama pekee wa CUF aliyehudhuria mikutano hiyo na kwa kuwa alikuwa peke yake ni wazi kuwa alizidiwa.

---

147 Ibid., uk.43

148 Ibid., uk.9

149 Kombo, op. cit., uk.255

150 EU EOM Report, op. cit., uk.9, uk.45

151 Ibid., uk.45

## Matokeo a Kufutwa Uchaguzi

Taarifa zinaeleza kuwa kufutwa kwa uchaguzi kumekuwa na athari za kijamii, kiuchumi, kisiasana <sup>152</sup> pamoja na athari za kikatiba.

### Masuala ya kikatiba

Kufuatia kufutwa kwa uchaguzi, masuala kuhusu uhalali wa kikatiba wa rais kuendelea kuwa madarakani yalianza kuibuka. Chama cha Wanasheria cha Zanzibar kilitoa taarifa na kueleza kuwa, kwa mujibu wa Ibara ya 28 (1) (b) ya Katiba inayotoa muda wa miaka mitano kwa rais kuanzia siku anayoapishwa, muda wa rais kubaki madarakani ungelimalizika tarehe 2 Novemba 2015, kwa kuwa aliapishwa tarehe 3 Novemba 2010. Kwa kujibu hilo, serikali ilinukuu Ibara ya 28(1) ya Katiba inayoeleza kuwa rais aliye madarakani ataendelea kubaki madarakani mpaka hapo rais mwingine atakapoapishwa.

Suala jengine lilihusu uhai wa Baraza la Wawakilishi – Baraza la Wawakilishi la 8 na la 11. Kwa mujibu wa Ibara ya 92 ya Katiba, uhai wa Baraza la Wawakilishi ni miaka mitano kuanzia siku ya mkutano wake wa kwanza, ijapokuwa Baraza linaweza kuvunjwa kati ya muda huo. Baada ya uchaguzi wa 2010, Baraza la 8 lilikutana tarehe 11 Novemba 2010 na lingelimaliza muda wake tarehe 9 Novemba 2015. Hata hivyo, lilivunjwa kabla ya kumaliza muda wake wa miaka mitano, tarehe 13 Agosti 2015. Na kwa kufutwa kwa uchaguzi wa mwaka 2015 hapajakuwepo na Baraza la Wawakilishi ilipofika mwisho wa mwaka 2015 ijapokuwa Spika na Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 73 na ya 74, walibakia madarakani.<sup>153</sup> Wakati huo huo, suala la uhalali wa Baraza la Wawakilishi la 11 lilijitokeza vile vile. Kwa mujibu wa Ibara ya 90 (1), Baraza lilitakiwa likutane si baada ya siku 90 kuanzia siku ambayo Baraza lililokuwepo lilipovunjwa, siku ambayo ingelikuwa tarehe 11 Novemba 2017, lakini hili halikutokea

---

152 Kombo, op. cit., uk.248

153 Ibid., uk.250-1

kwa sababu ya kufutwa kwa uchaguzi.<sup>154</sup> Baraza jipya lilikutana baada ya kurudiwa kwa uchaguzi mwezi Machi 2016, zaidi ya miezi mitatu baadaye.

Kwa kuwa uchaguzi wa Zanzibar uliofanyika sambamba na ule wa Muungano ulifutwa, uhalali wa matokeo ya uchaguzi wa Muungano, uhalali wa Bunge la Muungano bila ya kuwemo wajumbe kutoka Zanzibar na muda wa Rais Shein kuwa madarakani, yote haya yalijitokeza wakati wa kufunguliwa rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba 2015. Vyama vya CUF, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na The National Convention for Construction and Reform–Mageuzi (NCCR) vilipinga kuhudhuria kwa Rais Shein kwa sababu muda wake wa kuwa madarakani ulimalizika, na walishinikiza kuwepo kwa Maalim Seif, ambaye walidai kuwa ndiye aliyekuwa mshindi halali wa uchaguzi wa 2015. Hili lilisababisha kufukuzwa kwao Bungeni na kuongezeka kwa mvutano kati ya CCM na upinzani.<sup>155</sup> Zaidi ya hayo uhalali wa uchaguzi wa rais na wabunge nao pia ulihojiwa kwa sababu chaguzi mbili hizo, kama ulivyokuwa uchaguzi wa Zanzibar ziliendeshwa sambamba na ziliendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na zisingeliweza kuwa halali wakati uchaguzi wa Zanzibar ulifutwa.<sup>156</sup> Kwa kuwa hadi kufikia mwisho wa mwaka 2015 Bunge la Muungano limekuwa likiendesha vikao bila ya kuwepo kwa Wabunge wa Bunge la Muungano kutoka Zanzibar, uhalali wake umekuwa ni suala lenye utata. Hoja iliyotolewa ni kuwa ili liwe limetimia kamili, Bunge la Muungano lilipaswa liwe na wajumbe watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambao uwakilishi wao ni wa lazima na kuwa hili lingelifanyika wakati Baraza la Wawakilishi lipo na kwa hali hii hilo halikutokea.<sup>157</sup>

---

154 Ibid. uk.252

155 Ibid.

156 Ibid., uk.253

157 Ibid., uk.254

Juu ya taarifa na kauli za kupinga kufutwa kwa uchaguzi zilizotolewa na vyombo na taasisi mbali mbali, pamoja na Jumuiya za Kiraia, vyama vya siasa, asasi za kidini na vyama vingine, hakuna hata mmoja aliyetumia vipengele vya katiba kuomba tafsiri sahihi kutoka mahakamani. Yamefunguliwa mashtaka ya kutaka usuluhishi wa kisheria wa uchaguzi wa 2015/16. Ilielezwa kuwa ligeliweza kupatikana suluhisho kwa mujibu wa Ibara ya 25 A ya Katiba, inayoeleza kuwa mtu yeyote anaweza kufungua mashtaka kwa sababu ya ukiukwaji au ukiukwaji unaotarajiwa wa katiba.<sup>158</sup> Imeelezwa vile vile kuwa ile hoja ya au kisingizio cha kukosa imani na mfumo wa kisheria, hasa kwa chama kama Chama cha Wanasheria cha Zanzibar ambacho kina uwezo wa kisheria wa kushughulikia masuala ya kikatiba na kufungua madai kwa maslahi ya uma haina mantiki yoyote. Zaidi ya hilo, kwa Chama cha Wanasheria wa Zanzibar, ambacho hakikuwahi kufungua mashtaka kwa maslahi ya umma, dai la kudhalilishwa kwa hatua kama hiyo haliweza kukubalika.<sup>159</sup> Kuhusu Chama cha Wanasheria cha Zanzibar, Chama cha sheria Kisichokuwa cha Kiserikali kinachoongoza cha utetezi wa Kisheria na haki za binadamu, huu ungelikuwa ni wakati mwafaka wa kujaribu uwezo wao wa kutetea maslahi ya umma. Zaidi ya hilo, hata kama haki haikupatikana katika Mahakama Kuu ya Zanzibar, suluhisho lingelitafutwa katika mahakama za kanda kama vile Mahakama ya Afrika ya Mashariki (EACJ) na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Wananchi.<sup>160</sup> Kushindwa kufungua mashtaka kwa maslahi ya umma kwa Chama cha Wanasheria cha Zanzibar baada ya uchaguzi wa 2015/16 kulipingwa kwa nguvu zote, juu ya kuwa chama hicho hakina uzoefu na uwezo katika kutetea maslahi ya umma. Imetolewa hoja vile vile kuwa kufungua mashtaka ya

---

158 Ibid., uk.261

159 Ibid.

160 Ibid., uk.261-2

kutetetea maslahi ya umma kwa suala hilo kungeliendeleza na kuimarisha mfumo wa sheria kwa masuala ya kikatiba.<sup>161</sup>

Kwa upande mwingine, kuna hoja kuwa uingiliaji wa kisheria katika kutatua migogoro inayotokana na kufutwa kwa uchaguzi usingelikuwa na tija yoyote kwa hisia kuwa mahakama hazina uhuru. Maoni haya yanaonesha imani ndogo waliyonayo wananchi wa Zanzibar kwa mahakama na uwezekano wa mahakama hizo kusinikizwa zisifute uhaguzi. Maoni haya yamezidi kuchochewa kwa ile namna makamo mwenyekiti, ambaye ni jaji wa mahakama kuu alivyotendewa na vikosi vya usalama. Ilidhaniwa vile vile kuwa zingelifanywa mbinu na mahakama, kwa makusudi kuchelewesha matoke ya changamoto za kisheria kuhusu suala hilo na kwa hivyo kulifanya suluhisho la kisheria lisiweze kupatikana.<sup>162</sup>

## **Matokeo ya kiusalama**

Tarehe 28 Oktoba, kufuatia tangazo la kufutwa uchaguzi, zimekuwepo taarifa za kufanyiwa fujo wale waliodhaniwa kuwa wafuasi wa CUF katika kisiwa cha Tumbatu na mabomu mawili yalionekana karibu na Mji Mkongwe.<sup>163</sup> Taarifa nyengine zimeelezea juu ya kuripuka kwa mabomi ya kienyeji bila ya kuwepo kwa majeruhi.<sup>164</sup> Zaidi ya matukio haya, visiwani pamekuwepo na ulinzi mkali wa vikosi vya Muungano na vya vikosi mbali mbali vya usalama vya Zanzibar hali iliyowatisha wananchi.<sup>165</sup> Hata hivyo zimekuwepo taarifa kuwa mazingira ya kisiasa yaliendelea kuwa tulivu kwa sababu ya chama cha CUF kuwataka wanachama wake kuwa watulivu kila wakati.<sup>166</sup>

161 Ibid., uk.264-265

162 EU EOM, op. cit., uk.43

163 Ibid., uk. 41

164 Kombo, op. cit., uk.254

165 Ibid., uk.256; angalia vile vile Lowry Willy, 'Zanzibar bombings may be related to a disputed election', *The New York Times*, 1 November 2015, imepatikana katika [www.nytimes.com/2015/11/02/world/africa/zanzibar](http://www.nytimes.com/2015/11/02/world/africa/zanzibar)

166 EU EOM Report, op. cit., uk.42

## **Matokeo ya kiuchumi**

Kufutwa kwa uchaguzi kuliwafanya wafadhili wazuie ufadhili wao kwa Tanzania. Marekani iliyokiita kitendi hicho kuwa si cha halali, ilizuia ruzuku katika akaunti ya Changamoto za Milenia iliyokuwa na thamani ya mamilioni ya dola kwa madhumuni ya miradi ya maendeleo. Hii ilizidisha mfumko wa bei kwa Zanzibar, kutoka asilimia 8.7% hadi asilimia 10.9% katika miezi ya Oktoba hadi Novemba 2015. Mfumko wa bei ulisababisha kupanda kwa bei za vyakula kwa kiasi cha asilimia 4%, na kuathiri vibaya ustawi wa wananchi.<sup>167</sup>

## **Maoni Kuhusu Uchaguzi wa 2015/16**

Matukio yaliyouzunguka uchaguzi wa 2015/16 na athari za baadaye za kufutwa kwake yalielezwa zaidi wakati tume ikiwa kazini kama ifuatavyo:

### **Uchaguzi wa 2015**

Walioulizwa wengi walithibitisha kuwa uchaguzi wa 2015, tofauti na uchaguzi uliopita, ulikwenda vizuri mpaka pale ulipofutwa, maelezo ambayo yanafanana kwa kiasi kikubwa na yale maelezo mengine ya kitaaluma yaliyoelezwa hapo juu.

Tume ilielezwa kuwa wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi, vyama vya kiraia na asasi za kidini waliendesha programu kubwa ya kitaifa ya elimu kwa raia kwa madhumuni ya kuwepo kwa uchaguzi ulio halali na wa amani. Programu hiyo vile vile iliwataka wananchi kuheshimu mahitaji ya uchaguzi na kuheshimu sheria na kanuni. Mashehe wa Kiisilamu waliwaleta mashehe wenzao kutoka Angola, Rwanda, Malawi, Msumbiji na Zambia ili kubadilishana mawazo kuhusu athari za fujo wakati wa uchaguzi na kuhubiri dhidi ya fujo hizo. Kusema kweli, wengi walithibitisha juu ya uchaguzi kuwa huru na kuwepo ushiriki mkubwa wa wananchi katika uchaguzi. Wananchi

---

167 Kombo, *ibid.*, uk.257

walikubaliana kuwa uchaguzi ulifanyika kwa amani. Asasi za hapa nchini zilizofuatilia uchaguzi huo zilithibitisha juu ya kutokuwepo kwa taarifa zozote za matukio makubwa ya vurugu au makosa ya kuhusiana na uchaguzi. Waliohojiwa wengi walinukuu maeleza yaliyotolewa na watazamaji wa uchaguzi wa kimataifa yaliyothibitisha kuwa uchaguzi ulikuwa huru na wa haki. Yaliyobainika kuhusu uchaguzi wa 2015 ni kuwa *uchaguzi huo ulikuwa waizi kabisa na tulivu ukilinganisha na chaguzi nyengine za 1995, 2000 na 2005*. Kwa hivyo, kufutwa kwa uchaguzi kumetokea kuwa ni mshangao mkubwa kwa waliohojiwa wengi.

### ***Kufutwa Uchaguzi***

Waliohojiwa waliarifu tume kuwa kabla ya kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar alitwa nje ya kituo cha kuhesabu kura na kuondolewa na maafisa wa usalama mpaka pale alipoonekana tena saa kadha baadaye katika kipindi kilichorekodiwa kabla cha vyombo vya habari akitangaza kufutwa kwa matokeo. Kwa maoni ya muhojiwa mmoja, *kwa mara ya kwanza, jeshi lilishiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi*. Wakati huo huo, makamo mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na wajumbe wengine wa tume walibakia na kuendelea na kuhesabu kura. Hata hivyo, waliohojiwa walibainisha kuwa baadaye, makamo mwenyekiti naye alitwa nje ya kituo na maafisa wa usalama na kupelekwa mahali pasipojulikana. Palikuwepo na tuhuma kuwa aliteswa. Magwiji walieleza kuwa kutolewa nje kwa makamo mwenyekiti kulifanyika ili kuondoa uwezekano wa makamo mwenyekiti huyo kutangaza matokea yaliyo sahihi kwa kuwa alikuwa na madaraka ya kisheria ya kufanya hivyo pale mwenyekiti anapokuwa hayupo. Kwa hivyo, kutokuwepo kwake kumefanya asiwepo mtu yeyote aliyekuwa na uwezo wa kisheria wa kutangaza matokeo ya mwisho yaliyo sahihi.

Matukio yasiyo ya kawaida yaliyouzunguka uchaguzi wa 2015 na hasa ile namna uchaguzi ulivyofutwa, yalilaaniwa kwa nguvu na waliohojiwa wengi. Kufutwa kwa matokeo yote, pamoja na yale ya

Wabunge kuliwashangaza wengi. Zaidi ya hayo, tangazo la kuufuta uchaguzi lilitolewa baada ya kumalizika uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na matokeo kutangazwa. Siku tatu zilipita tokea kufanyika kwa uchaguzi wa wabunge, washindi walikwishapata vyeti vyao wakisubiri kuapishwa tu. Zaidi ya hayo, ijapokuwa mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Bwana Jecha, ameeleza kuwa udanganyifu katika uchaguzi na kupiga kura mara mbili huko Pemba kuwa ndiyo sababu za kuyafuta matokeo, sababu hizi zilipingwa kwa nguvu wakati tume ikiwa kazini. Uamuzi wa mtu mmoja wa kuyafuta matokea uliofanywa na mwenyekiti ulikosolewa na kuonekana kuwa ni uamuzi wake mwenyewe binafsi. Tume ilibaini kuwa wajumbe wengine wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar walimpinga hadharani yeye na vitendo vyake. Katika taarifa yake iliyotolewa kwa vyombo vya habari, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) ililaani na kupinga hatua ya kufuta uchaguzi. Ilikeza kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa mujibu wa sheria, haikuwa na madaraka ya kufuta uchaguzi na kueleza kuwa, kwa lolote lile, sheria inatoa suluhishi kwa kila dosari ya uchaguzi. Ilizidi kuelezwa kuwa hapajakuwepo na sababu za kisheria za kufuta uchaguzi wote. *Unaweza kuabirisha uchaguzi wa jimbo, na siyo uchaguzi wote.* Na kwa tukio kama hili sheria haimpi madaraka mwenyekiti kuchukua hatua kwa niaba ya tume yote. Ilikezwa kuwa Jecha hakuwa na madaraka ya kufuta uchaguzi.

Waliohojiwa waliielezea hatua ya kufuta uchaguzi kwa namna mbali mbali:

Kwa wengi kufutwa kwa uchaguzi kulielezwa kuwa ni *dosari kubwa, ukiukwaji mkubwa wa taratibu, ubalifu, si halali kabisa* na wengine wamesema *ni kinyume na katiba.*

Mhojiwa mwingine aliiambia tume:

Seif kutangaza matokea yake haukuwa uhalifu wala si kinyume na sheria.

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilifanya makosa kufuta uchaguzi. Huko Pemba watu walilia kwa sababu hiyo.

Ukizihesabu kura, mgombea wa CUF alikuwa na kura 20,000 zaidi kuliko mgombea wa urais wa CCM, tofauti iliyo kubwa kuliko ile ya kawaida ya kura 2,000. Kwa hivyo Seif anatakiwa awe rais.

Akifanya majumuisho ya hali ilivyokuwa, mhojiwa mmoja alieleza: ‘Uamuzi wa wananchi haukuheshimiwa.’

Tume ilibaini pia hali ya kukata tamaa iliyolizunguka tukio la kufuta uchaguzi. Mhojiwa mmoja, katika hali ya kuvunjia moya alisema:

Seif alishinda. Lakini amri ya kufuta matokeo ilikuja kutoka juu – kutoka Bara. Zanzibar hatuna *jesbi*, wala polisi. Wananchi hawakuweza kufanya lolote. Wangeliuliwa.

Ni wachache tu ndio waliounga mkono kitendo cha kufuta uchaguzi. Mmoja wao alikuwa na maoni haya:

Seif amejitangaza kuwa mshindi. Zilikuwepo kura zaidi katika majimbo huko Pemba kuliko ilivyotarajiwa; vilikuwepo vitisho.

Kwa wengi, kufutwa kwa uchaguzi limebakia kuwa ni suala la wasiwasi mkubwa na chanzo cha hali ya kutoridhika. Wengi miongoni mwa waliohojiwa waliambia tume kuwa Wazanzibari wengi wamefadhaishwa na kufutwa kwa uchaguzi wote wa Zanzibar. Waliuliza kwa nini uchaguzi wa Rais wa Muungano na ule wa Wabunge wa Bunge la Muungano ambao ulifanyika sambamba na ule wa Rais wa Zanzibar na wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar haukuathirika kabisa. La kushangaza ni kuwa, tume ilithibitisha kuwa uchaguzi uliofanywa baadaye kuhusu tuhuma za udanganyifu wa uchaguzi umebainisha kuwa malamiko hayo hayakuwa na msingi. Mahojiano na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yalifafanua kuhusu malamiko ya kupiga kura mara mbili huko Pemba na kueleza kuwa hilo lilikuwa ni pale mpiga kura, kwa makosa alipopewa karatasi mbili za kupigia kura. Tuhumu ya

sanduku la kura kutolewa nje ya kituo cha kupigia kura kinyume na sheria nayo pia ilikataliwa kwa kuwa hilo lilitokea pale wawakilishi wa wagombea wote katika kituo fulani cha kupigia kura walipokubaliana kwa kauli moja kuhesabu kura mahali pengine penye nafasi kubwa zaidi.

### ***Sababu za kufuta uchaguzi***

Yamekuwepo maoni na maelezo tofauti kutoka kwa waliohojiwa juu ya kwa nini uchaguzi ulifutwa. Hoja kubwa ilikuwa ni kwa sababu chama cha CCM kilishindwa. Kwa mujibu wa maoni haya, wakati uchaguzi ukifutwa, chama cha CCM kilikuwa kimeshashindwa Unguja, ngome yake. Ushindi wa CUF, kwa mujibu wa maelezo ya baadhi ya waliohojiwa, ulipatikana juu ya kuwepo kwa hila za kugawa majimbo kwa kukipendelea chama tawala. Kwa mujibu wa hoja hizi, kwa mara ya kwanza chama cha CUF kilishinda majimbo tisa, Unguja, ukiongeza majimbo 18 Pemba, kwa jumla wakiwa na majimbo 27 kati ya majimbo 54 kwa Zanzibar yote kwa Baraza la Wawakilishi. Zaidi ya hayo, ushindi wa 50 kwa 50 kati ya CCM na CUF kwa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi ulikwishatangazwa. Kikiwa hakina tamaa ya kupata ushindi, ilisemekana kuwa chama cha CCM hakikuwa na jengine la kufanya isipokuwa kuyafuta matokeo ya uchaguzi. Zaidi ya hilo, kutangazwa matokeo ya uchaguzi wa Unguja, ngome maarufu ya CCM kabla ya kutangazwa yale ya Pemba, ngome ya chama cha CUF kulionekana kuwa ni kosa kubwa kwa upande wa CCM. Ilizidi kuelezwa kuwa, wakati CUF kikiongoza Unguja, ushindi wa kura kwa CUF huko Pemba ulikuwa ni wa wazi. Kusema kweli, kama ilivyoelezwa wakati tume ikiwa kazini, hadi wakati huo CUF haikujua chochote kuhusu matokeo ya Pemba.

Wakitilia mkazo kwa nini CCM isingelikuwa tayari kuukubali ushindi wa CUF, baadhi ya waliohojiwa walieleza kuwa serikali ya Zanzibar itakayoongozwa na CUF isingelikubalika ndani ya Muungano. Mhojiwa mmoja alieleza kuwa ‘Serikali ya Umoja wa Kitafa ni nzuri pale CCM inapokuwa madarakani tu.’ Hoja

nyengine iliyotolewa ni kuwa serikali inayoongozwa na upinzani, upande wowote ule wa Muungano iisingelikuwa na maslahi chini ya mfumo wa hivi sasa wa kisiasa. Mfuasi mmoja wa CCM alikiri waziwazi wakati tume ikiwa kazini kuwa ‘ukiitoa serikali kwa vyama vya CHADEMA na CUF Muungano utavunjika.’ Zaidi ya hayo kumekuwa na imani kuwa kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi, upinzani umeshinda mara mbili. Umeshinda katika kura za rais wa Muungano Zanzibar, pamoja na kura za rais wa Zanzibar. Mgombea wa upinzani Lowassa inasemekana kuwa alipata kura nyingi zaidi Zanzibar kwa nafasi ya rais wa Muungano na Seif Hamad kwa nafasi ya rais wa Zanzibar.

Tume imeelezwa vile vile, kuwa chama cha CUF kabla ya uchaguzi, kiliruhusiwa kufuatilia na kuhesabu kura za matokeo ya uchaguzi. Baadhi ya waliohojiwa walithibitisha kuwa, siku ya kupiga kura, chama cha CUF kimekuwa na watu waliokuwa wakiranda kutoka kituo kimoja cha kupigia kura kwenda katika kituo kingine, wakikusanya matokeo ya mwisho ya uchaguzi na nakala za fomu za matokeo ya mwisho ya uchaguzi zilizotiwa saini. Kusema kweli, CUF chenyewe kilijigamba kuwa kilikuwa na utaratibu madhubuti wa kufuatilia uchaguzi na kwa sababu hiyo ndiyo maana kilijitangaza kuwa mshindi. CUF kilikiri vile vile kuwa kutokuwepo namna yoyote ile ya kuthibitisha ushindi wake kwa miaka yote iliyopita kimelezimika kuwa na mfumo madhubuti wa kufuatilia uchaguzi. Chama hiki kilithibitisha kuwa kilipata msaada kutoka Umoja wa Kimataifa wa Kidemokrasia ambao umekiwezesha kujiandaa vizuri, kutoa mafunzo kwa watumishi wake na kutengeneza mfumo utakaowawezesha kufuatilia kwa makini upigaji kura ili kuepukana na udangayifu katika kupiga kura. Muhojiwa mmoja alithibitisha hilo:

Mkakati huo ulikuwa rahisi lakini wa siri. Ulikuwa ni pamoja na kukusanya matokea kutoka sanduku moja moja. Na ilipofika saa 5 usiku, tarehe 26 Oktoba 2015, Hamad, akiwa na matokeo, alivita vyombo vya habari na kujitangaza kuwa mshindi.

Zaidi ya hilo, ilielezwa kuwa ushindi wa CUF usingeliweza kufichika kwa kuwa matokeo ya mwisho yalikuwa tayari yanajulikana na wananchi. Maelezo ya waliohojiwa mbali mbali yalieleza kuwa matokeo ya uchaguzi yalisambaa kwa urahisi Siku ya Uchaguzi. Wengi walithibitisha kuwa matokeo ya mwisho ya uchaguzi yalioneshwa waziwazi katika vituo mbali mbali vya kupigia kura. Kama ilivyoelezwa:

Matokeo yalijulikana na yalitangazwa. Kila mgombea aliweza kujua matokea yake. Yalikuwa wazi.

Ilielezwa vile vile:

Kila wakala katika kila kituo cha kupigia kura alipata matokeo ya mwisho ya uchaguzi kabla ya saa sita usiku ya siku ya kupiga kura. Matokeo ya mwisho yalibandikwa ukutani. Mawakala walitia saini.

Kwa upande mwingine, kuna wale walioamini kuwa hata bila ya kuwepo mfumo 'usio na shaka'wa CUF wa kufuatilia uchaguzi na kuhesabu kura, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ingelimtangaza rasmi mshindi halai kama matokeo yasingelifutwa kwa kuwa Tume hiyo ilikusanya na kuhesabu kura za matokeo ya mwisho ya uchaguzi kwa utaratibu mzuri na kwa namna iliyokuwa wazi.

Wakati baadhi ya waliohojiwa waliilaumu Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Muungano kwa kufutwa kwa uchaguzi, nani hasa aliyehusika moja kwa moja bado ni kitendawili. Baadhi ya waliohojiwa, kama ilivyoelezwa hapo awali, walimpongeza Kikwete kwa kusababisha kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, wachache walimlaumu kwa kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi:

Kila Mzanzibari anajua kuwa uchaguzi haukuwa na udanganyifu lakini ulifutwa kwa amri ya Kikwete.

Walipeleka jeshi katika hoteli ambayo mchakato wote wa kufuta uchaguzi ulifanyika. Sisi ni kolini ya Tanganyika; viongozi wa hapa ni vibaraka wa Tanganyika. Magufuli amerithi donda la kisiasa lililosababishwa na Kikwete.

### ***Athari za kufuta uchaguzi***

Sehemu hii anaeleza maoni yaliyotolewa juu ya athari za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizojitokeza mara baada ya kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa 2015.

Baadhi ya watu walieleza kwa tume maoni yao juu ya athari zilizojitokeza mara baada ya kufutwa kwa uchaguzi. Yalikuwepo maoni kuwa haki ya vyombo vya habari na haki ya kupata habari zilikiukwa. Maoni haya yamefikiwa kutokana na ukweli kuwa pale Maalim Seif alipotangaza matokei yake, hakuna lolote lililomtokea *lakini kituo cha radio kilichotoa taarifa hiyo kilifungwa kwa muda wa miezi mitatu.*

Mawazo madhubuti yameeleza kuwa kufutwa kwa uchaguzi hakukuwa na mantiki yoyote. Kumelezwa kuwa hakukuwa suluhisho kwa suala la Zanzibar au kwa namna yoyote ile la kuudhofisha upinzani na badala yake limeuimarisha upinzani huo:

Kufuta uchaguzi si suluhishi. Hakutoirekebisha hali ya Zanzibar. Kunaifanya hali iwe mbaya zaidi. Upinzani bado upo pale pale. Kufuta uchaguzi kunaufanya upinzani ufanye kazi zaidi na kuzidi kuwa na nguvu. Huwezi kuuzuia au kuuu upinzani. Zanzibar ina upinzani ulio imara zaidi katika Afrika ya Mashariki.

Jambo ambalo tume imeliona linakera ni kule kutokuwepo kwa upinzani wowote dhidi ya uchaguzi wa 2015. Ni wazi kuwa hakuna hatua yoyote ya kisheria iliyochukuliwa kupinga kufutwa kwa uchaguzi wa 2015 au kuweka hali ya mambo sawa. Zimetolewa sababu chache wakati tume ikiwa kazini za kuelezea hali hii. Ya kwanza ni kutokuwepo kwa mahakama ya katiba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati mahakama hiyo inatajwa katika katiba haikupata kuanzishwa. Katika hali hiyo, hakuna namna yoyote ya kisheria ya kushughulikia masuala ya kikatiba kama yale yaliyojitokeza kutokana na uchaguzi wa 2015/16. La pili ni kutokuwepo kwa msingi wa kisheria wa kupinga matokea ya uchaguzi wa rais nchini Tanzania. Hoja iliyopo ni kuwa, tofauti na majirani zake Kenya na Uganda,

mfumo wa sheria wa Tanzania hautoi fursa ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais. Tume imebaini kuwa katiba zote mbili, ya Muungano na ya Zanzibar hazina vipengele kama hivyo. Kwa hali ya Zanzibar, walinukuu Ibara ya 119 (13) ya Katiba ya Zanzibar inayoeleza kuwa:

Hakuna mahakama itakayokuwa na uwezo wa kisheria wa kuhoji kitu chochote kitakachanywa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar wakati ikifanya shughuli zake kwa mujibu wa Katiba hii.

Kwa hivyo, bila ya uhalali wa kisheria (*locus standi*), matokea ya uchaguzi wa rais, yakishatangazwa, huo ndio mwisho. Baadhi ya watazamaji wa uchaguzi wameiona dosari hii na kutoa pendekezo la kuirekebisha hali hiyo.<sup>168</sup>

Mwisho, watu wengi wameeleza juu ya kutokuwa na imani na mahakama kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya ushabiki wake wa kisiasa. Wamelalamika kuwa mahakama ya Zanzibar inatumikia maslahi ya chama tawala na serikali. Kwa mantiki hii waliohojiwa wengi waliambia tume wasingelitegemea kuwa mahakama kutengua uamuzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Jambo moja lilikuwa wazi: *Mahakama zinapendelea - CCM na zisingelijali kutetea maslahi ya umma kwa kupinga matokeo ya uchaguzi.* Kwa kutetea hofu hii tume mara kwa mara ilielezwa kuhusu tukio ambalo, baada ya kufutwa kwa matokeo ya uhaguzi, kiongozi mmoja mkuu wa mahakama alieleza hadharani kuwa hakuna lolote lililo chanya litakaloweza kutokea kutokana hatua yoyote ya mahakama kuhusiana na uchaguzi. Kwa maneno ya muhojiwa mmoja: 'Inakuwaje afisa wa mahakama azungumze kama kwamba yeye ni mwanasiasa? Utategemeaje kesi ya haki na kuwa na imani na mahakama?'

Muhojiwa mwengine hakuzungumzia suala la ushabiki wa kisiasa tu bali alizungumzia pia masuala nyeti ya uwezo yanayoihusu mahakama ya Zanzibar. Kwa maoni yake, majaji hawaimudu kazi yao na kwa baadhi ya mashauri hawatoi haki ipasavyo. Akitilia

168 Angalia EAC Observer Report, uk.38; the EU EOM Observer Report, uk.47-48

mkazo hili, alitoa mfano wa tukio la mwaka 2001 pale Chama cha Wanasheria cha Zanzibar kilipohoji ubora wa majaji wanaoteuliwa na rais kuhusiana na kutokuwa na sifa zinazotakiwa na uwezo wao.

## **Uchaguzi wa marudio wa 2016**

Tume imebaini kuwa matukio yanayohusiana na uchaguzi wa marudio wa mwaka 2016 yameelezwa katika ripoti mbali mbali.

Kufuatia kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi, serikali ilitangaza kurudiwa kwa uchaguzi, ambao ulifanyika tarehe 20 Machi 2016. Uchaguzi huo uligomewa na vyama tisa kati ya vyama vya siasa 14 vilivyoshiriki katika uchaguzi wa rais wa mwezi Oktoba. Vyama hivyo vilikuwa ni pamoja na chama kikubwa cha upinzani - CUF.<sup>169</sup> Chama cha CUF katika mkutano wa nne wa majadiliano na CCM uliofanyika tarehe 24 Novemba, kilitoa mapendekezo mawili ya kuituliza hali ya Zanzibar. La kwanza lilikuwa ni kwamba pindi chaguzi zote tatu za Zanzibar zikirudiwa, uchaguzi wa rais, wa Baraza la Wawakilishi na wa ngazi ya serikali za mitaa, chama cha CUF kitashiriki tu kama chaguzi hizo zitaendeshwa na Tume Huru itakayoongozwa na Umoja wa Mataifa. Pendekezo la pili lilikuwa ni kuwa irudiwe sehemu ya uchaguzi wa rais katika majimbo 14 ya Pemba yalipokuwepo madai ya kujitokeza dosari. Hata hivyo, CCM ililikataa pendekezo la awali kwa sababu ya kutokuwepo hoja za kisheria kwa tume itakayoongozwa na Umoja wa Mataifa, na hakikulizangatia pendekezo la pili.<sup>170</sup>

Juu ya kuwa vyama viliwasiliana kwa maandishi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar juu ya kukataa kwao kushiriki, tume haikuyaondoa majina ya wagombea waliogoma au vyama vyao kutoka kwenye karatasi za kupigia kura, na vyama vya siasa vilivyoshiriki havikuruhusiwa kufanya kampeni kabla ya marudio ya uchaguzi.<sup>171</sup> Matokea ya uchaguzi wa marudio yalikuwa ni ushindi wa

<sup>169</sup> EU EOM Report, *op. cit.*, uk.9& uk.45

<sup>170</sup> *Ibid.*, uk.43

<sup>171</sup> *Ibid.*, uk.45

asilimia 91.4 % kwa chama tawala cha CCM na kutangazwa rais aliye madarakani Dk. Ali Mohamed Shein, kuwa mshindi.

Zaidi ya taarifa kutoka katika maandishi yalioletajwa hapo juu, tume ilisikia maoni mbali mbali juu ya uchaguzi wa marudio wa 2016 ikiwa ni pamoja na maelezo ya CUF juu ya kwa nini chama hicho kilikataa kushiriki katika uchaguzi wa marudio.

Wengi miongoni mwa wale waliozungumza na tume waliulaani uchaguzi wa marudio na kusema kuwa ulikuwa ni aibu, siyo kwa namna ya ushindani ulivyokuwa ambapo matokea ya 2015 yalifutwa lakini pia kwa sababu chama cha CUF kilikataa kushiriki. Muhojiwa mmoja alisema: ‘Uchaguzi wa 2016 ulishirikisha kundi la wahuni waliojidai kuwa kuna uchaguzi uliokuwa ukiendelea.’

Waliohojiwa walithibitisha pia juu ya idadi ndogo ya wapiga kura waliojitokeza kwenye uchaguzi wa marudio. Tume ilielezwa kuwa huko Pemba, ngome ya wapinzani, hawakupiga kura kabisa, isipokuwa kwa wafuasi wachache wa CCM. Kwa mujibu wa muhojiwa mmoja, *wapiga kura waliokuwepo wakati wa uchaguzi wa marudio walikuwa chini ya asilimia 20%*. Maoni yanayohusiana na hayo yameeleza kuwa katika baadhi ya majimbo huko Pemba, baadhi ya wabunge walitangazwa kuwa washindi bila ya kupigiwa kura.

Chama cha CUF kilifafanua sababu zilizokifanya kisusie marudio ya uchaguzi. Sababu kubwa ni ukiukwaji wa katiba katika kufuta uchaguzi. Kwa maoni yao, kushiriki katika marudio ya uchaguzi kungelikinzana na msimamo wao juu ya ukiukwaji wa katiba na ubatili wa kufuta uchaguzi na kutangaza uchaguzi wa marudio. Walitoa hoja kuwa hakuna kipengele katika Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar au sheria nyengine yoyote ile kinachompa madaraka mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kufuta uchaguzi. Wenye madaraka hayo ni wasimamizi wa uchaguzi tu tena kwa uchaguzi katika majimbo na mnamo siku tatu za uchaguzi.

Hoja yao ya pili ilikuwa ya kisiasa. Walidai kuwa, ni kwa sababu CCM kilishindwa katika uchaguzi ndiyo maana waliufuta uchaguzi

huo, na kusambaza vikosi vya usalama kwa wingi siku ya uchaguzi, hizo zilikuwa ni dalili za wazi za nia ya CCM kutaka kuchukua madaraka kwa namna yoyote ile na kwa hivyo kushiriki kwa CUF katika uchaguzi wa marudio kungelikua ni kitendo kisichokuwa na maana yoyote. Pia, waliamini kwa dhati kuwa kama CUF kingelishiriki, yangelitokea machafuko makubwa dhidi ya upinzani. Maoni haya yaliungwa mkono na muhojiwa mmoja wakati tume ikiwa kazini:

Upinzani haukushiriki katika marudio ya uchaguzi kwa sababu mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar aliufuta uchaguzi kwa sababu tu upinzani ulishinda. Walikuwa na shaka kama wangelishiriki uchaguzi huo ungelikuwa kweli ni huru na wa haki. Pia waliususia kwa sababu upinzani uliogopa kuwa wangeliteswa, wangelitishwa au hata wangeliuliwa na wanajeshi kwa sababu wanajeshi wengi waliwekwa ili 'kuulinda' uchaguzi.

Kwa maoni ya muhojiwa mwingine, kutokuwepo kwa fujo wakati wa uchaguzi wa marudio, bila ya kujali kususiwa kwa uchaguzi huo, kulitokana na kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Fujo ingeliweza kutokea kutokana na mchakato wa kususia uchaguzi.

## Hali ya Baada ya Mwaka 2016

---

Kuilewa vizuri hali hiyo, tume ilitafuta maoni ya Wazanzibari juu ya hali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi visiwani Zanzibar baada ya uchaguzi wa 2016. Maoni yao yanaelezwa katika sura hii.

Yamekuwepo maoni mchanganyiko kuhusiana na hali ya Zanzibar. Ni watu wachache tu wanaoonekana kuridhishwa na serikali ya hivi sasa na hali ya mambo ilivyo. Kwa waliohojiwa wengi, tume ilibaini kuwepo hali ya kuvunjika moyo na wasiwasi kuhusiana na mustakibali wao. Tume imebaini vile vile kuwepo hali ya huzini kwa kusambaratika kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kama ilivyobainika: *Tumechoka kuwapoteza wapendwa wetu; tunawatazama tu [akikusudia wale walio madarakani].*

### Aina/Tabia ya Serikali ya Baada 2016

Baada ya uchaguzi wa marudio, chama kikuu cha upinzani, CUF, kilijitenga na serikali na Baraza la Wawakilishi.

Rais Shein aliteua wanachama watatu wa vyama vidogo vya upinzani kuwa mawaziri. Ukiwaacha hawa watatu, mawaziri wengine wote ni wanachama wa chama tawala cha CCM. Kwa kuwa CUF hakikushiriki katika uchaguzi wa marudio wa 2016 hivi sasa hakina wajumbe katika Baraza la Wawakilishi kwa hivyo ni wazi kuwa hakuna mwanachama wa CUF aliye waziri kwa sababu mawaziri

lazima wawe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hivi sasa Baraza la Wawakilishi linadhibitiwa na CCM ambao ndio wengi.

Mawaziri watatu kutoka katika vyama vidogo vya siasa ni Bwana Hamad Rashid wa Alliance for Democratic Change (ADC), ambaye ni Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wakati Bwana Juma Ali Khatib kutoka African Democratic Alliance (ADA-TADEA) na Bwana Said Soud Said kutoka Alliance for Farmers Party (AFP) wote wameteuliwa kuwa mawaziri wasiokuwa na wizara maalum. Hao wawili wa mwisho ni sura mpya katika baraza la mawaziri. Hata hivyo, Bwana Rashid, ni mwanasiasa mzoefu ambaye aliwahi kuwa waziri katika serikali ya kwanza ya Muungano chini ya Mwalimu Julius Nyerere, lakini baadaye alifukuzwa kutoka CCM na kujiunga na CUF hadi mwaka 2015, ambako pia alifukuzwa na kujiunga na ADC.

Katika vyama vitatu hivyo ADA-TADEA ndiyo kikongwe kikiwa kimeanzishwa mwaka 1990 lakini kusajiliwa kikamilifu na kutambuliwa rasmi mwaka 1992, na hivi sasa kinaongozwa na John D. Lifa Chipaka. Cha pili kwa ukongwe ni AFP kilichoanzishwa 2009 na kuongozwa na Said Soud Said. Kipya kabisa na ambacho Rais Shein ameteua waziri ni ADC, kilichoanzishwa mwaka 2012 na Said Miraji Abdallah, aliyekuwa mwanachama wa CUF na mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hakuna hata kimoja katika vyama vitatu hivi kilichowahi kupata kiti katika Baraza la Wawakilishi hapo kabla.

Tume ilikusanya maoni mbali mbali juu ya serikali ya Zanzibar ya hivi sasa. Kwa jumla, ni watu wachache tu walioielezea serikali ya hivi sasa kuwa ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wale walioifananiwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya 2010 ni kwa sababu ya kuwaingiza wajumbe wa vyama vya upinzani tu. Wengine ambao walikuwa na mawazo kama hayo wameielezea serikali ya hivi sasa kuwa ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa yenye nguvu zaidi kwa sababu ya kuvishirikisha vyama vitatu vya upinzani tofauti na ile iliyopita iliyokishirikisha kimoja tu.

Hata hivyo, maoni ya wengi yalikuwa kinyume ya hivyo. Wakichukizwa na serikali ya hivi sasa, waliohojiwa wengi walikiri waziwazi kuwa wasingeliweza kuielezea sawasawa tabia ya serikali ya Zanzibar ya baada ya mwaka 2016 kwa kuwa haiko kama vile Serikali ya Umoja wa Kitafa inavyoelezwa katika katiba ambayo inaitaka serikali hiyo iwe na chama kilichoshinda na chama cha pili kilichopata asilimia 10% ya kura pamoja na wajumbe waliochaguliwa wa Baraza la Wawakilishi. Wengine walikataa kabisa kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Muhojiwa mmoja alisema. ‘Mantiki ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa haipo’. Hoja kubwa inayotolewa na wale wenye msimamo huu inatokana na uhalali wa kikatiba wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya hivi sasa. Hoja nyengine ni kuwa mdhamini mkubwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kutambulika kwake kikatiba ambayo itahakikisha kuwepo kwake bila ya kujali ni chama gani kilichoshinda. Hata hivyo, udhamini huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ulisita pamoja na uchaguzi wa 2016; kwa hivyo, ndiyo maana waliohojiwa wengi wameieleza serikali ya Zanzibar ya hivi sasa kuwa ni batili na ipo kinyume na katiba.

Hili limedhoofisha ari na kufuta maana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya asili, ya mwaka 2010 iliyokuwa na nia ya kuvisuluhisha vyama vikubwa viwili – CCM na CUF.

Kiongozi wa CUF anaieleza hali hiyo:

Chama cha CUF kinatafuta amani ya kweli na umoja kwa misingi ya chama na sera zake lakini hivi sasa tunakabiliwa na serikali haramu, iliyopo kinyume na katiba. Katiba ya Zanzibar haifuatwi. Serikali ipo kinyume na katiba, haikuchaguliwa, si Serikali ya Umoja wa Kitafa. Tumerudi katika hali ya ushabiki wa vyama iliyokuwepo kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa - bila ya uweledi.

Wakati tume hii ikiwa kazini, nafasi ya makamo wa kwanza wa rais, iliyokuwa imeshikiliwa na Seif Hamad, ilibaki wazi. Hata hivyo, kwa kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imo ndani ya katiba na sheria za nchi, maoni mengi yaliyotolewa wakati tume ikiwa kazini ni kuwa

serikali ya hivi sasa ni serikali ya chama kimoja inayoongozwa na CCM.

Kwa ufasaha zaidi, imeelezwa kuwa serikali ya hivi sasa haiendani na ufafanuzi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ulivyo katika katiba unaoelezea kuwepo kwa makamo wawili wa rais, kwa sababu serikali ya hivi sasa ina makamo wa pili wa rais tu na haina makamo wa kwanza wa rais. Limetajwa vile vile suala la kipengele cha katiba kinachosema kuwa ili chama kiwe na sifa ya kuwemo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa lazima kiwe kimeshika nafasi ya pili wakati wa uchaguzi na kiwe kimepata zaidi ya asilimi 10% ya kura ili kuwa na sifa ya kuwa sehemu ya baraza la mawazri kizingiti kinachovizua vyama vitatu vya upinzani ambavyo hivi sasa ni sehemu ya serikali kwa kuwa havikuweza kuwa na sifa hiyo. Kwa maneno ya mhojiwa mmoja. 'Vyama vitatu hivyo havikushinda hata kiti cha kata.' Wengine wamevieleza hivyo vyama vitatu vya watu wachache viliomo ndani ya serikali kuwa ni 'vibaraka' wa CCM. Hoja nyengine ya msingi ni kuwa bila ya CUF, chama ambacho kina wafuasi wengi katika nchi, kwa serikali, serikali ya hivi sasa haikidhi hata kidogo ufafanuzi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ulivyo ndani ya Katiba ya Zanzibar.

Kwa hivyo, zaidi ya kuwa imekuwa serikali ya chama kimoja, limeibuka pia suala la ubatili wake na kuwa kwake kinyume na katiba. Muhojiwa mmoja alieleza kuwa :

Imeundwa serikali ya chama kimoja kwa sababu hapajakuwepo chama cha upinzani kilichopata kiti katika Baraza la Wawakilishi. Upinzani umeipinga serikali kama hiyo na kusema kuwa ni batili na umeigomea serikali. Kuna dosari – kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa kisheria lakini si kiuhalisia. Hali kama hii inajenga uadui.

## Haki za Binadamu na Hali ya Kisiasa

Pamekuwepo na wasiwasi mkubwa kuhusiana na hali ya haki za binadamu baada ya uchaguzi wa marudio wa 2016 . Tume imebaini kuwa tokea kurudiwa kwa uchaguzi huo:

Baadhi ya wafuasi wa CUF wamedhalilishwa na kupigwa, milango imevunjwa pale mtu alipokataa kufungua. Wake za watu walibakwa na waume zao kupigwa, wengine hadi kufa na wengine wamefanywa vilema. Yote haya yamenakiliwa. Baadhi ya viongozi wamekamatwa. Wale walioshinda uchaguzi wamekamatwa, wameteswa, wamepigwa mateke na kupigwa. Tunasikia kuna maagizo kutoka Bara kusitisha hayo.

Unguja, imechorwa taswira ya hali ya hofu kubwa na wasiwasi miongoni mwa Wazanzibari. Hofu hiyo ilihusishwa na hali ya kisiasa iliyokuwepo ambayo waliohojiwa walidai kuwa iliwanyima watu haki ya kusema kwa uhuru juu ya masuala yanayohusu hali ya kisiasa. Mahojiano ya tume yalibaini kuwepo kwa ongezeko la matukio ya mateso, ya kupotea na mauaji ambayo yalikusishwa na serikali. Kuzagaa na kuzidi hali ya vitisho miongoni mwa wananchi lilikuwa ni jambo la kawaida. Ijapokuwa serikali ilikanusha. Limetajwa pia suala la mazezeta, kundi la kikatili lililojulikani kwa ukatili wake wa kukamata, kutesa na baadhi ya wakati kuua, kwa yeyote yule aliyesema chochote kuipinga serikali. Tukio la kifo cha katibu wa uwenzezi wa CUF mwezi Oktoba 2017 ikituhumiwa kuwa aliuliwa na Mazezeta lilitajwa mara kwa mara. Taarifa zilidai kuwa alikufa baada ya kupigwa sana na kuachwa afe kufuatia tuhuma za uhaini dhidi yake.

Huko Pemba, tume ilielezwa juu ya tukio ambalo mtu mmoja alichukuliwa kutoka nyumbani kwake na watu wasiojulikana wanaoaminika kuwa ni watumishi wa usalama na kupelekwa Unguja. Tukio hili lilihusishwa na mtu huyo kwa sababu ya kutoa matamshi ya kuipinga serikali. Palikuwa na wasiwasi kuwa hiyo ilikuwa ni kazi ya Mazezeta. Ni wazi kuwa watu wengi wa Zanzibar wana hofu kubwa kwa usalama wao binafsi na familia zao. Jumuiya za Kiraia

nazo pia zinawaogopa Mazezeta. Kama ilivyoelezwa, *Jumuiya nyingi za Kiraia haziwazi kusema kitu kwa hofu ya kuambwa kuwa ni wapinzani wa serikali, kukamatwa na serikali na kukabiliana na balaa la Mazezeta wanaoweza kukupiga, kukuua au kukuchomea moto nyumba yako.*

Baadhi ya wanawake waliohojiwa waliarifu tume kuwa kusambaratika kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hali ya wasiwasi ya baadaye imesababisha hali ya kukata tamaa ya kuwepo kwa amani na utulivu kwa wanawake. Hili limesababisha kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, kama vile kuvunjiwa nyumba, jambo linalowaathiri wanawake kwa namna ya pekee. Walilalamika juu ya namna ya wale waliowatuhumu kuharibu mali, kama vile maafisa wa usalama, watumishi wa serikali za mitaa na Mazezeta, namna walivyowanyanyasa na kukiuka haki za wanawake. Walielezea vile vile shida inayowapata kutokana na kukosa makazi – ikiwa ni pamoja na kulazimika kutafuta makazi kwenye nyumba za mabinti wao –, jambo la kudhalilisha kwa wanawake watu wazima wenye familia zao. Wale wenye mawazo haya wanaamini kwa dhati kuwa serikali inaunga mkono shida ya watu kukosa makazi badala ya kuwasaidia wale waliokosa makazi makwao.

Zaidi ya hayo, hasa kuhusiana na uchaguzi wa marudio, kuna maoni ya jumla kuwa wale walio madarakani hawakuwajali au wamewajali kidogo wananchi wa kawaida. Pamekuwepo na malalamiko kuwa maamuzi na sera zinatungwa na watu wachache walio juu bila ya kuwashauri wale walio chini au kupata ushiriki wao. Matokeo yake ni kuwa, mahitaji ya jamii hayakuzingatiwa. Kadhalika, wananchi wanapewa ahadi za maneno matupu, hasa wakati wa kampeni, ahadi ambazo hazitekelezwi mpaka kumalizika kwa awamu ya kisiasa, na mwanasiasa huyo huyo hurudi tena kwa jamii wakati wa uchaguzi mwingine. Matokeo yake ni kuwa jamii nyingi za vijijini wanakosa mahitaji ya msingi ya kijamii. Wanaoathiriwa zaidi ni wanawake ambao katika hali ya umasikini mkubwa inawabidi wabebe mzigo

mzito wa kuwalea watoto na kuangalia nyumba kwa kuwa tabia ya kuwa na wake wengi imeenea Zanzibar.

Tume imepata habari vile vile kuwa serikali inawazuia watu wasijieleze kwa uhuru juu ya yale yaliyotokea baada ya uchaguzi wa mwaka 2015 na upungufu wa serikali ya hivi sasa. Zimetolewa taarifa za mashtaka ya kubuni dhidi ya wale wanaoikosoa serikali ya hivi sasa au kuubeza uchaguzi wa 2016. Kwa sababu ya hofu hii, Jumuiya za Kiraia za Zanzibar zimekuwa na hofu kiasi kwamba zimeshindwa hata kusema juu ya mwenendo wa kisiasa wa hivi sasa. Mwanachama mmoja wa jumuiya ya kiraia amekiri wazi kwa tume hii kuwa Jumuiya za Kiraia Zanzibar hazikuwa na ujasiri hata wa kufanya utetezi juu ya masuala muhimu kama vile kufufua mchakato wa kuipitia upya katiba nchini Zanzibar. Walikuwa na hofu kuwa kwa kufanyya hivyo wangelikuwa wanakwenda kinyume na serikali ya Zanzibar, ambayo inaaminika kuwa inaunga mkono mfumo wa serikali mbili, na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa Rais Magufuli, ambaye anaona mchakato wa kuipitia upya katiba si muhimu. Kwa baadhi ya watu, vitendo visivyo halali vinavyoendelea hivi sasa pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu vinawakumbusha siku za kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na wengi wamevihusishavitendo hivyo na kutokuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maelezo ya muhojiwa mmoja yanaeleza jinsi hali ilivyokuwa mbaya: 'Ni jambo linaloumiza kichwa kufikiri nini kitakachotokea bila ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hali ni mbaya na ijapokuwa watu wamenyamaza kimya, wanatokwa damu ndani kwa ndani.' Waliohojiwa wengi wameeleza hofu yao vile vile kuwa watu wenye hasira zilizofungwa kizibo ni bomu la mtego ambalo litaripuka wakati wowote ule, sasa hivi au halafu.

Wengine wanaamini kuwa hali iliyoelezwa hapo juu imechochewa na ukimya wa upinzani. Zaidi ya salamu za matumaini ambazo CUF imezitoa kwa wananchi pamoja na kuwataka kutulia na kuwa wavumilivu, pamekuwepo na wasi wasi kuwa kwa jumla CUF

imefumbwa mdomo kuhusu yale yanayoendelea hivi sasa na hatua gani nyengine ya kuchukua. Hilo limesababisha wasiwasi mkubwa kwa baadhi ya Wazanzibari ambao hawana hakika nini kingine CUF kitafanya. Kwa baadhi ya watu hawana hakika kama CUF itashiriki katika uchaguzi wa 2020.

Hili limeelezwa kwa ufasaha wakati wa mahojiano na muhojiwa mmoja:

Ukweli kuwa wanajaribu kuwapa matumaini wafuasi wao bila ya kuwepo kwa muda maalum umeleta wasiwasi, na bila ya kuwepo majibu madhubuti kutoka CUF juu ya nini kingine kitafanya, hili limeusababishia uongozi wa chama hicho kupata sinikizo kubwa.

Hali hii, kwa mujibu wa habari zilizopatikana, inazidi kuchochewa na ukweli kuwa chama cha CUF lazima kiwashughulikie wanachama wake waliokasirika sana, hasa vijana, kwa sababu ya kufutwa kwa uchaguzi – kundi la watu wasiokuwa na ajira si rahisi kulidhibiti na hawa ndio wenye mategemeo ya mustakibali mzuri. Wakati wa majadiliano, imeonekana dhahiri kuwa kuwatuliza wafuasi, hasa vijana ilikuwa ni shida. *Wanataka mabadiliko, maisha bora, ajira. Wanataka kujua nini kitatokea baada ya uchaguzi uliopita.*

Kiongozi mmoja wa upinza amekiri kuhusu ukweli huu, na kuseme hili kuhusu vijana: ‘Umetwambia tusubiri kwa miaka miwili. Nini kingine?’

Kuna hofu ya vijana kufanywa wawe na siasa kali, hasa ukiangalia kuzidi kwa dalili za ugaidi katika Afrika ya Mashariki. Wengine walitahadharisha juu ya gharama ya ugaidi Zanzibar kuhusiana na maisha ya watu, ukichukulia idadi yake ndogo ya watu ambapo kuuwa watu 100 itakuwa balaa.

Zaidi ya hayo yaliyoelezwa hapo juu, kurudi katika hali ya nchi yenye ushindani mkali wa kisiasa imekuwa ni jambo la wasiwasi mkubwa kwa waliohojiwa wengi. Tume ilielezwa kuwa mpasuko wa kisiasa na mvutano kati ya wafuasi wa CCM na CUF umeibuka upya. Baadhi ya vijana ambao tume imezungumza nao wamekiri

kuwa mgawanyiko wa kisiasa miongoni mwa Wazanzibari umeibuka upya, hata miongoni mwa weledi, tena kwa misingi ya kikanda kati ya Pemba na Unguja.

Kuibuka upya kwa hali ya uhasama ulikuwepo huko nyuma na mgawanyiko miongoni mwa wananchi umeelezwa kama ifuatavyo:

Kila siku zinavyokwenda, hali inazidi kuwa mbaya. Sasa nyumba za watu zinavunjwa. Watu hawendi mazikoni kwa sababu ya mgawanyiko wa kisiasa; baadhi ya ndugu hawasalimiani kwa sababu ya siasa; watu wanasafiri kwa vyombo tofauti kwa sababu ya siasa. Hali ya uhasama imerudi. Watu wanashughulika na mambo yao wenyewe kwa sababu wamekata tama kwa kuwa wanapopiga kura hawapati kile wanachokitaka.

Vile vile pamekuwepo na vitisho vya kuitenga Pemba baada ya 2016. Muhojiwa mmoja ameeleza: ‘Mara baada ya uchaguzi wa 2016, serikali ya chama kimoja ilianza kuwapuuzwa watu wa Pemba nao wanalipiza kwa kusema “mkitutenga tutakutengeni vile vile”.’

Hali ya kutokuwepo na usawa imeelezwa kuwa imejitokeza tena makazini. Vijana wengi ambao tume ilikutana nao wamethibitisha kuwepo kwa uchunguzi mkubwa kwa vijana kwa sababu ya imani za kisiasa na usuli wa kikanda kwa ajili ya kupata kazi. Waliuita *Ndugunisation* katika kazi. Kwa mujibu wa maelezo ya kijana mmoja, mchakato wa kupata kazi serikalini umekuwa wa kisiasa na wa kibaguzi. Wameeleza wazi kuwa, kama ilivyokuwa kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hivi sasa, wafuasi wa CUF au wale wanaohusika vyovyote na chama hicho hawawezi kuajiriwa serikalini. Wakieleza juu ya kukata kwao tamaa, vijana wengi kutoka upande wa upinzani waliambia tume kuwa hawapati kazi hata kama wanazo sifa zinazohitajika. Matokeo yake ni kuwa wahitimu wengi wa vyuo vikuu hawana ajira. Walilalamika kuhusu maisha magumu yanayowakabili. Kama muhojiwa mmoja alivyoeleza: ‘Ni shida kuwa mkuu wa shule kama wewe ni mfuasi wa upinzani. Nilipata matatizo nilipotaka kuanzisha chama kisichokuwa cha kiserikali cha mazingira. Nilikuwa nikiulizwa: Wewe ni nani?’

Vijana wengi wameuelezea mchakato wa kuchunguzwa wakati wa kutafuta ajira na kueleza kuwa Afisa wa Idara ya Usalama anakuwa na jukumu kubwa katika mchakato huo. Wameueleza mchakato huo kuwa ni wa hatua mbili za mahojiano: Kwanza ni mahojiano ya ana kwa ana na afisa mahasusi wa usalama kutoka Ofisi ya Usalama; halafu afisa wa kutoka ofisi hiyo anatuma eneo la kwenu ili kuwahoji viongozi wa hapo na kupata maelezo kuhusu wazazi wa anayeomba kazi, uwanachama wao wa kisiasa na maelezo mengine. Katika hali kama hiyo, baadhi ya vijana wameamua kuchukua kadi za uanachama za CCM ili kupata kazi serikalini.

Haya ni maelezo ya kijana mmoja:

Afisa wa Ofisi ya Usalama anakuuliza wewe ni mwanachama wa chama gani. Kama wewe ni mwanachama wa CUF basi hakuna kazi, kwa hivyo watu sasa wanajibu kuwa wao ni wanachama wa CCM lakini baadaye Afisa wa Usalama anakwenda kwenye jamii ya mwombaji kazi ili kuthibitisha jibu hilo. Wanasema kuwa kuna sababu kubwa ya kuwachunguza watu kwa sababu CUF hakiitambui serikali. Kwa hivyo, baadhi ya vijana wanajaribu kupata kadi za CCM ili kupata kazi lakini serikali inajaribu pia kuchimba mizizi ya ukoo wa mwombaji pamoja na uanachama wa kisiasa.

Kijana huyo ameeleza utaratibu huo kuwa si wa kidemokrasia na kutaka iwepo Zanzibar iliyo ya kidemokrasia zaidi na yawepo mabadiliko ya mfumo wa utawala Zanzibar:

Kwa Zanzibar, demokrasia ni ndoto ya mchana. Kama Uganda, CCM imekuwepo milele. Vijana wengi wanaielewa hali hii na hawataki serikali ya chama kimoja iendelee milele.

Hata hivyo, muhojiwa mmoja ametetea hatua ya kuutenga upinzani katika ajira serikalini na namna ya kuajiri. Kwa mujibu wa muhojiwa huyo:

Kwa nini mfuasi wa upinzani apewe kazi ikiwa wataiteka nyara serikali, watatoa siri na kwenda kinyume na kanuni za utumishi serikalini?

Hali hiyo imehusishwa na hali ya kisiasa Tanzania Bara. Wanaamini kuwa hali ya haki za binadamu iliopo Bara inaathiri yale yanayotokea Zanzibar. Kwa mujibu wa maoni ya muhojiwa mmoja:

Ni mikutano ya ndani tu ndiyo inayoruhusiwa kwa vyama vya upinzani. Matangazo ya moja kwa moja ya mijadala ya bungeni yamepigwa marufuku. Kumkosea Magufuli katika mitandao ya kijamii kutakutia matatani. Watu wengi wameuliwa Kibiti; mwandishi wa habari anayechunguza habari hiyo amepotea.

Akizungumza juu ya hali ya kisiasa ya hivi sasa, mtu mwingine ameeleza kuwa ijapokuwa *mambo yapo kimya, na hakuna mikutano ya kisiasa inayofanyika, bado watu wana basira za ndani kwa ndani.*

Watu wengi ambao tume ilifanya mazungumzo nao kote, Unguja na Pemba wanaielezea hali ya kisiasa ya Zanzibar hivi sasa kuwa inatengenezwa na Serikali ya Muungano – kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa 2015, uchaguzi wa marudio wa 2016 na hata aina ya serikali iliyopo Zanzibar hivi sasa. Kwa wale wenye maoni haya, watu wa Zanzibar walipiga hatua kubwa na ya kijasiri ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2010 na walikuwa wazi juu ya namna ya serikali waliyoitaka lakini kwa sababu ya kuingiliwa na serikali ya Muungano, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilisambaratishwa.

## Hali ya Kiuchumi

Kuna viashirio vichache vinavyoonesha kuendelea kwa uchumi baada ya uchaguzi wa 2016. Mfano mmoja ni kuwa Rais Shein alipandisha bei ya karafuu kutoka TSh. 3500 hadi TSh. 14,000, na baadaye hadi TSh. 16,000, kwa kilo na matokeo yake ni kuwa usafirishaji wa karafuu kwa magendo kupitia Mombasa umepungua. Hiki ni kiashirio kuwa uchumi umeboreka baada ya uchaguzi wa 2016. Maoni mengine ni kuwa maendeleo makubwa ya miundo mbinu yamefanyika Pemba wakati wa serikali ya Rais Shein lakini hili halikuwapendeza wale watu wenye mawazo hasi, *ambao fikera zao zimeganda kule kwenye mawazo ya kizamani ya kuendeleza ubaguzi dbidi ya watu wa Pemba chini ya serikali za utawala wa CCM.*

Mawazo ya jumla ni kuwa nchi, juu ya athari hasi za uchumi zilizosababishwa na wafadhili wa nchi za magharibi kusimamisha misaada yao baada ya uchaguzi wa 2016, baadhi ya wahojiwa wanadhani kuwa kurudiwa kwa uchaguzi wa 2016 kumesababisha kuvurugika kwa bajeti ya nchi na kuuharibu uchumi kwa sababu ya gharama za juu za kuendesha uchaguzi, hasa kwa kuwa uchaguzi huo lilikuwa ni tukio lisilotarajiwa. Inasemekana kuwa ni kwa sababu ya uchumi mbaya ndiyo maana serikali imetoa ardhi kwa Azam (kampuni ya mtu binafsi ambayo kwa mujibu wa baadhi ya wahojiwa, inaonekana kupatiwa fursa nyingi za kibiashara Zanzibar na Bara) ili kulipa deni ambalo wahojiwa wanadai kuwa kampuni hiyo iliikopesha serikali kwa ajili ya kulipa mishahara.

Kwa watu wengi ambao tume ilikutana nao Pemba, kwa jumla hali visiwani imebaki kuwa mbaya. Tume ilielezwa kuwa hapajakuwepo na maendeleo yoyote ya kiuchumi yenye maana huko Pemba kwa siku za hivi karibuni. Watu wengi wamelalamika kuwa miradi mingi ya maendeleo inakwenda Tanzania Bara. Wameendelea kulalamika kuwa, hata huko Pemba miradi mingi inayofadhiliwa inakwenda kwa wafuasi wa CCM. Visiwa vinakabiliwa na hali ngumu ya kiuchumi, kiasi kikubwa cha ukosefu wa ajira, gharama za maisha zilizo juu, kodi zilizo juu lakini mishahara ni midogo na fursa chache za kiuchumi. Wameeleza pia juu ya kutokuwepo na ajira katika sekta ya Vyama Visivyokuwa vya Kiserikali. Tume imabaini kuwa miradi ya kilimo kama vile ufugaji wa wanyama na kuku, ambao ndio muhimili wa uchumi wa Pemba inaendelea kuporomoka. Pia yametolewa malalamiko juu ya kutokuwepo kwa malighafi za kutosha na rahisi kwa ajili ya viwanda na kutokuwepo miundo mbinu ya msingi kama vile viwanda vya kutengeneza chakula cha mifugo. Matokeo yake ni kuwa kwa watu wengi mazao ya mifugo na kuku yamekuwa ghali mno na kwao yanaonekana kuwa ni anasa.

Hali ya vijana huko Pemba imeelezwa kuwa ni mbaya zaidi ukiilinganisha na ya Unguja. Umekuwepo ushahidi wa kuwepo

umasikini wa hali ya juu, hali ya kuwa hatarini, uhalifu na hali ya kukata tamaa kwa vijana. Uzururaji, kuongezeka kwa mimba za utotoni na vijana kudanganywa na wanasiasa kumeongezeka. Pamekuwepo na wasiwasi mkubwa kuhusu vijana wa Pemba kuvutiwa na siasa kali. Wakati vijana wa Pemba wana hamu kubwa ya kuendeleza maisha yao na kufanyakazi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na kujifunza kutokana uzoefu wa nchi mbalimbali, hayo, kwa mujibu wa vyanzo vya habari vya Pemba yanakatishwa tamaa kwa ukosefu wa fedha na usimamizi mzuri. Zaidi ya hayo, juhudu za hivi sasa zenye madhumuni ya kuboresha maisha ya vijana kwa kupitia jumuiya za vijana, kama zile za kuendeleza upandaji wa miti na matunda na ufugaji wa wanyama, inadhaniwa kuwa zinawanufaisha zaidi vijana kutoka chama tawala kuliko wenzao kutoka upande wa upinzani. Kijana mmoja ameeleza kuwa ili kunufaika kwa miradi kama hiyo, vijana kutoka upande wa upinzami inawabidi wafiche uwanachama wao wa kisiasa. Hata hivyo, tume imebaini kuwa miradi kama hiyo ni michache na iko mbali.

Katika kuwatathmini baadhi ya waliohojiwa huko Pemba, ni hali ya kusikitisha ya huko Pemba ndiyo inayowafanya Wapemba wengi, pamoja na wale walio wasomi na wenye ujuzi na wale walio Ughaibuni – duniani kote Ulaya, Mashariki ya Kati, Amerika na Japan – kuwa hawana mori wa kurudi visiwani kuishi na kufanyakazi huko juu ya uzuri wake wa ajabu na wingi wa maliasili. Ni kwa sababu hiyo hiyo ndiyo maana Wapemba walio Ughaibuni ambao wangeliyaunga mkono maendeleo ya visiwani hawakufanya hivyo. Kwa bahati mbaya, kwa maoni ya waliohojiwa wengi Pemba, hali mbaya ya kiuchumi na kijamii, na hasa mazingira yenye vikwazo ya kisiasa visiwani, hayana tamaa ya kubadilika hivi karibuni.

Kufuatia hali ya kiuchumi, inasemekana kuwa CUF imechukua hatua mbali mbali. Chama hicho kiliandaa programu ya kuendeleza ujuzi katika ujasiri amali ambayo ilikuwa ikitoa mafunzo kwa vijana. Pesa zilikusanywa kutoka kwa vijana ili kuanzisha mfuko unaozunguka

ili kuwawezesha kujiajiri. Miradi mingine iliyoanzishwa ilikuwa ni pamoja na kilimo, uvuvi, utengenezaji wa mashua, utengenezaji wa nyavu za kuvulia na kutengeneza chumvi. Hata hivyo, programu hizo zimekuwa na upungufu kwa uhaba wa rasilimali.

## Hali ya Kijamii

Tume ilielezwa kuhusu baadhi ya matukio chanya ya maisha ya kijamii ya Zanzibar. Lililotiliwa mkazo ilikuwa ni programu ya serikali ya elimu ya msingi bure na ada hafifu kwa elimu ya sekondari jambo linaloifanya elimu kupatikana kwa wote. Zaidi ya hayo, mahusiano ya kifamilia Zanzibar bado yana nguvu kwa hivyo utamaduni wa kusaidiana bado ungalipo.

Kwa upande mwingine, tume imebaini kuwa Wazanzibari wengi hawapati huduma za kijamii za msingi. Huduma za matibabu ni mbaya. Watumishi wa huduma za afya na dawa hazitoshi jambo lililosababisha kuongezeka kwa vifo vya watoto. Wanawake wameeleza kuwa *watoto wanakufa kila siku*. Hali hii inazidishwa na kiwango kikubwa cha umasikini, kwani wengi hawadiriki hata kupata dola mbili kwa siku na hawawezi kupata milo mitatu kwa siku.

Tume imeelezwa kuwa ni wale walio serikalini na katika chama tawala tu ndio wenye uwezo wa kiuchumi wa kuzifikia huduma za msingi za kijamii: *Ni viongozi wa serikali na wa chama tawala tu ndio wenye hali nzuri*. Tume ilielezwa kuwa kwa sababu ya hali ya kijamii na kiuchumi iliopo hivi sasa, watoto wengi wa vijijini huvutiwa na tasnia ya utalii na uvuvi, na wengine huenda shule ili kuwafurahisha wazazi wao tu. Kwa maneno mengine, kwa baadhi ya watoto mategemeo ya kubariki kwa kupitia elimu yamedidimia. Kama muhojiwa mmoja alivyosema: 'Kwa nini niende shule wakati hatimaye mtu hawezi kupata kazi?'

## Uchaguzi wa 2020

### Utangulizi

Uchaguzi mkuu mwingine wa Tanzania unatarajiwa kufanyika mwaka 2020. Wapiga kura wa Zanzibar wanashiriki katika chaguzi tano: Uchaguzi wa rais wa Jamhuri ya Muungano, wabunge wa Bunge la Muungano, rais wa Zanzibar, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani wa Serikali za Mitaa. Chaguzi mbili za kwanza ambazo zinahusiana na Muungano zinaendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na chaguzi tatu za mwisho zinaendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Aina mbili hizi za uchaguzi zinatarajiwa kufanyika katika siku tofauti baada ya wiki moja baina yao zikianza zile zinazohusiana na Zanzibar.<sup>172</sup>

Inatarajiwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ingelikuwepo Zanzibar kikamilifu ili kuandaa na kuendesha chaguzi za Muungano, haifanyi hivyo. Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Ibara ya 12 A ya Sheria ya Uchaguzi ya 1985 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inakasimu madaraka yake yote kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar<sup>173</sup> na kiuhalisia mambo yote yanayohusiana na aina mbili hizo za uchaguzi yanashughulikiwa na Tume ya Uchaguzi ya

<sup>172</sup> Hamad & Peter, op. cit., uk.148. Angalia pia Peter, 'Recent developments in Zanzibar', op. cit., uk.182.

<sup>173</sup> Peter, ibid., uk.206 & uk.214

Zanzibar na katika hilo zina uhusiano wa ‘uwakala’.<sup>174</sup> Hii ni pamoja na uandikishaji na matumizi ya daftari la kudumu la wapiga kura la Zanzibar na kanuni za kufanya kampeni kwa aina zote mbili za uchaguzi. Hili lina matatizo yake. Kwa mfano, mtu akinyimwa haki ya kupiga kura na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika uchaguzi wa Zanzibar kwa sababu yoyote ile mtu huyo moja kwa moja anapoteza haki ya kupiga kura kwa rais wa Muungano na wabunge wa Bunge la Muungano. Kadhalika, siku za nyuma Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikiyafuata maamuzi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa suala la ugawaji wa majimbo ya uchaguzi.<sup>175</sup> Kwa mfano, mwaka 2010, wagombea wa Zanzibar wa uchaguzi wa Bunge la Muungano walianza kampeni yao wiki mbili baada ya wenzao wa Bara kwa sababu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilifupisha muda wa kampeni visiwani.<sup>176</sup> La kushangaza ni kuwa, ushirikiano huu kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar hautambuliwi na sheria za Zanzibar.<sup>177</sup>

## Kuelekea Uchaguzi wa 2020

### **Hisia ja jumla**

Watu wengi ambao tume ilikutana nao hawakuwa na hakika nini kitatokea mwaka 2020. Kwa wengi wao mustakbali hauna matumaini. Wengi walieleza juu ya kukata tamaa kuhusiana na hali ya mambo ilivyo na itakavyokuwa hapo baadaye. Hawakuwa na matumaini makubwa ya uchaguzi wa 2020. Hata hivyo, wengi walitilia mkazo juu ya haja ya mabadiliko ya serikali baada ya miaka 50 kwa kutegemea kuwa upinzani utaruhusuiwa kutawala. Ni wachache tu ndio waliokuwa na matumaini kuwa kitafanyika kitu ili kurekebisha hali ya kisiasa ya hivi sasa. Kuna wachache walioamini kuwa wakati

---

174 Ibid., uk.214

175 Ibid., uk.207

176 Ibid., uk.214

177 Ibid.

hakuna kinachofanyika hivi sasa, kwa kuwepo nia njema na ujasiri karibu zitachukuliwa hatua madhubuti za kushughulikia mgogoro wa kisiasa. Umetolewa wito wa kuwa na uchaguzi wa 2020 usiokuwa na vurugu ili kuepuka kujitokeza tena hali ya 2015/16 kwa sababu kwa jumla chaguzi ni ghali kuziendesha na zinaathiri uchumi kwa namna mbaya. Kwa sababu hiyo, baadhi ya watu wanataka suala hili waachiwe wanasiasa ili walitatie. Kauli hii inalingana na ule usemi: *Serikali inaendelea. Nchi imo mikononi mwa wanasiasa.*

Hisia za jumla ni zile za kukata tamaa, kukosa imani na hali ya kusubiri majaliwa. Watu wengi hawaoni maana ya kuwa na uchaguzi. Wengine wameeleza kuhusu hali ya kukosa imani kwa wanasiasa na siasa zenyewe. Wakiwa hawana imani na hali ya udanganyifu ya demokrasia katika Afrika kwa jumla na hasa Zanzibar, zimetolewa kauli kama vile, ‘Tanzania, siasa ni mchezo mchafu’ na ‘Zanzibar siasa ni jinamizi’. Wengine wameeleza juu ya utovu wa uaminifu na ubinafsi wa wanasiasa kama ifuatavyo: ‘Wanasiasa Zanzibar, wakiwa katika chama tawala au upinzani, wanajiingiza katika siasa ikiwa ni biashara na hufanya hivyo kwa maslahi yao binafsi’; ‘Hawautumikii umaa’; ‘Wote CCM na CUF wanaweza kufanya udanganyifu wakati wa uchaguzi’; ‘Baadhi ya watu wanatafuta kivuno kutoka CCM. Hujiunga ili kupata vyeo’.

### **Wasifu wa Seif Sharif Hamad**

Watu wengi walimwamini sana na kuwa na mategemeo makubwa kwa Seif Hamad akiwa mtu binafsi. Waliridhika na kuwa na matumaini kwa ujumbe wake wa mara kwa mara kuwa nchi inabidi itulie kwanza ili kila mmoja aweze kushiriki katika maendeleo na demokrasia yake. Watu walipata matumaini makubwa kutokana na maneno ya Seif kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakuwa ndiyo kitu cha kwanza atakachokifanya kwa serikali yoyote ambayo ataiunda siku za mbele. Palikuwa na imani pia kuwa ujumbe wa Seif umesaidia sana watu ambao walikuwa hawakutulia kisiasa. Kusema kweli, watu wengi walimwona kuwa ni mwanasiasa wa kuaminika ukimlinganisha na

baadhi ya wenzake na wafuasi wa chama. Yalikuwepo malalamiko kuwa baadhi ya wafuasi wake wamekosa uvumilivu na wangelipenda kutaka fidia kutoka CCM. Tume imeelezwa vile vile kuwa imani kubwa waliyonayo baadhi ya wafuasi wa CUF kwa Seif imewafanya waamini kuwa atakuwa rais kabla ya 2020. Baadhi ya kauli zilizotolewa ni kama zifuatazo: ‘Watu wanampenda Maalim Seif’; ‘Watu barabarani wanaamini Maalim atakuwa rais kabla ya mwaka 2020. Tunawataka watu wawe na matumaini hayo’.

Hata hivyo, yamekuwepo mawazo pia kuwa kama Seif hatokabidhiwa madaraka kabla ya 2020, hatagombea urais.

Kuna wengi wanaoamini kuwa hapatakuwepo kiwanja kilicho sawa mwaka 2020 bila ya kuwepo kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya Zanzibar. Wanaamini kuwa hivi sasa CCM inaudhibiti mchakato wa uchaguzi na kuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar haiko huru – imeshirikishwa na CCM. Kwa maoni yao, ni kwa kuwepo mabadiliko makubwa tu juu ya namna Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inavyoundwa na kuruhusiwa ifanyekazi kwa uhuru ndipo yanapoweza kupatikana matumaini.

Kwa upande mwingine, kuna wale walioeleza kuwa hali tete ya kisiasa Zanzibar imepungua kwa kiasi fulani kwa sababu ya hatua zinazochukuliwa na Rais Magufuli za kupambana na ufasidi, ikiwa ni pamoja na kupungua kwa matumizi mabaya ya fedha za umma na kuongezeka kwa makusanyo ya kodi na hivyo uchumi kuboreka na kuleta matumaini kwa wananchi.

### **Fujo au amani?**

Kuhusiana na amani na utulivu, ni watu wachache waliotabiri kuwepo amani na utulivu mwaka 2020. Baadhi ya wale wanaoamini kuwa hapatakuwepo na fujo wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi wa 2020 wanaamini kuwa serikali iliyopo itaendelea kubaki madarakani. Wanaamini kuwa kuwepo madarakani kwa CCM kutaiwezesha serikali ya hivi sasa kuzuia fujo yoyote ya upinzani na/

au wananchi. Kwa kutilia mkazo hili, muhojiwa mmoja ameeleza kuwa mlinganisho wa uwezo Zanzibar haujawahi kuwa upande wa CUF – hata wakati wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Alieleza kuwa: ‘Serikali ya Umoja wa Kitaifa haikubadili lolote – zilikuwa ni dhana tu. Kusema kweli mlinganisho wa madaraka haukubadilika.’ Wale wanaokubaliana na mawazo haya wameeleza kujiamini kwao kuwa hivi sasa serikali iliyo madarakani ipo katika njia sahihi – ikiwa na maana kuwa haitoyumba. Maoni mengine yaliyotolewa kulingana na haya ni kuwa sheria ya uchaguzi imeshabadilishwa ili kukiruhusu CCM kufanyakazi pamoja na vyama vidogo vya upinzani na kuwa *kama CUF kinafanya kazi kwa dbati kwa maslabi ya umma, basi kijiunge na serikali ya CCM. Kama si hivyo, basi vyama vidogo vitaendelea kufanyakazi na CCM. Wakijitenga, basi itabidi wakubali lolote lile.* Hii ina maana kuwa CCM kitaendelea kuwa juu zaidi.

Kinyume chake, watu wengi wanatabiri fujo wakati wa uchaguzi wa 2020. Wengine wanatoa hoja kwa nguvu kuwa, ukiangali utaratibu wa upigaji kura Zanzibar, CCM hakina dalili ya kushinda katika uchaguzi wa 2020 kwa namna iliyo huru na ya haki, na ikiwa hivyo basi kinaweza kutumia nguvu kubwa ili kubaki madarakani. Wengine wameeleza kuwa, kama ilivyokuwa hapo zamani, serikali ya Muungano itaingilia kati ili kuhakikisha kuwa CCM kinashinda kwa namna yoyote ile. Zaidi ya hayo, pamekuwa na wasiwasi kuwa kama Seif hakuwa rais kabla ya uchaguzi wa mwaka 2020, kama baadhi ya watu wanavyoamini kuwa ndivyo itakavyokuwa, fujo itatokea. Yalikuwepo maoni vile vile kuwa uchaguzi wa 2020 utakuwa na fujo kama CUF kitashiriki.

Tume inaona kuwa tabia ya serikali ya hivi sasa ya kuzima upinzani, hasa kwa kutumia vikosi vya usalama, itasababisha vurugu na kurudia yale yaliyotokea wakati wa chaguzi zilizopita. Zanzibar inahitaji kujizuia kutumia nguvu ya jeshi kwa kuwa ikitumika njia hiyo ni tabu kuirekebisha hali inayojitokeza. Haya yameonekana kwa kuchukua mfano wa Uganda na nchi nyengine katika kanda hii.

## CUF kugomea uchaguzi wa 2020

Jambo jengine ni kuwa hali ya kutojali ya wafuasi wa CUF, hali iliyojikusanya baada kupiga kura katika chaguzi nne – mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 na 2015 – bila ya kushinda, itawafanya waache kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2020. Baadhi ya wale wenye maoni haya wameyahusisha na ukweli kuwa uchaguzi Zanzibar haukuwa chombo cha demokrasia wala cha kutaka amani. Kama muhojiwa mmoja alivyoeleza, ‘Watu wengi hawatashiriki katika uchaguzi wa 2020 kwa sababu kile tunachokichagua sicho tunachokipata. Tutabaki nyumbani; hatutafanya maandamano kwa sababu tunataka amani.’

Maoni ya wengine yameeleza kuwepo kwa tishio kwa amani au kutokea vurugu: ‘Wafuasi wa upinzani “watawaua” viongozi wao kama watawataka wakajiandikishe na kushiriki katika uchaguzi wa 2020’; ‘Mustakibali ni mbaya na umejaa kiza’; ‘CCM itayaona matokeo; sote tutateseka’; ‘Amani tuliyoifurahia Zanzibar itatoweka’. Kwa kauli kama hiyo ya kukata tamaa muhojiwa mwengine aliiambia tume kuwa hakuna namna yoyote ya kuwambia watu kushiriki katika uchaguzi wa 2020. Alieleza kuwa baadhi ya vijana wametishia kuwa : *Mkitambia kushiriki katika uchaguzi wa 2020 tutakushughulikieni.*

Kutokana na maelezo ya hapo juu, ni wazi kuwa kwa namna yoyote ile, maoni ya wananchi hayalingani na yale ya viongozi wao, na madai yao vile vile hayalingani na yale ya viongozi. Katika hali hii, wananchi wanaonekana kuwa wako mbele zaidi kuliko viongozi wao. Wasiwasi ulioelezwa na viongozi katika maoni ya hapo juu yanaweza kuwa ni dalili kwamba viongozi wanaweza kushindwa kuwadhibiti wafuasi wao.

## Juu ya mustakibala wa CUF

Wahojiwa wachache wanatazamia kuwepo kwa upinzani imara zaidi – yaani CUF iliyo imara zaidi kwa siku za mbele. Wanaamini kuwa watu wa Pemba wana uwezo mkubwa wa kubadili hali ya idadi ya

watu kwa uchaguzi wa Zanzibar kwa sababu ya uwezo wao mkubwa wa kuzaa sana. Vile vile, wameeleza juu ya kubadili hali ya idadi ya watu kwa watu kuhama kutoka Pemba kuja Unguja kwa sababu ya shida za kiuchumi. Uhamiaji huo utauwezesha upinzani kupata viti vingi hata Unguja kama utafanyika uchaguzi ulio huru na wa haki. Wakitilia mkazo hili, wamesema kuwa imebainika kwamba *Zanzibar hivi sasa imezungukwa na Wapemba walio katika upinzani*. Mwaka 2015, upinzani ulipata viti vinane Unguja na CCM haikupata hata kiti kimoja Pemba. Kusema kweli, viti vingi vitachukuliwa na CUF katika uchaguzi wa 2020. Hii itakifanya CUF kuwa ndiyo chama kikuu chenye wafuasi wengi baada ya muda. Hoja hii inabidi ilinganishwe na madai kuwa CCM nayo inawaruhusu wahamiaji kutoka Bara ili kuzidisha idadi yao vile vile.

Kwa upande mwingine, kwa baadhi ya wahojiwa, njia ya kuelekea uchaguzi wa 2020 haikunyooka sawa kwa CUF. Umekuwepo wasiwasi kuhusu kuwepo kwa vikwazo vingi vya kisheria na kisiasa vyenye nia ya kukidhoofisha chama hicho. Pamekuwepo na hofu kuwa, zaidi ya agizo la serikali ya Muungano kuuzuia upinzani kutoendesha shughuli za vyama vya siasa hadi wakati wa kipindi cha uchaguzi, mabadiliko ya mwenendo wa uchaguzi Zanzibar baada ya uchaguzi wa -2016 yanakipendelea chama tawala na kudhoofisha utendaji mzuri wa CUF.

La kutia wasiwasi zaidi ni changamoto ambazo zinaikabili CUF hivi sasa kikiwa chama. Tume imebaini kuwa CUF imegawika makundi mawili – kundi moja likiongozwa na aliyekuwa mwenyekiti wake, Prof. Ibrahim Lipumba upande wa Bara, na kundi jingine likiongozwa na katibu mkuu, Maalim Seif Hamad kwa Zanzibar. Kwa baadhi ya wahojiwa, chama kimo katika mtihani. Pamekuwepo na wasiwasi vile vile kuwa migogoro ya ndani ya CUF imekuwa ni tishio la kuwepo kwake kama chama na katika kushiriki kwake kwenye uchaguzi wa 2020. Hata hivyo, juu ya kupoteza kwake mwelekeo na uhai wake uliojengeka kwa miaka kadha, pamekuwepo na wasiwasi

kuhusu shida za kuandikisha chama kipya. Inasemekana kuwa zoezi la kufanya hivyo ni refu na la kuchokesha. Mchakato huo si kama unahitaji taratibu fulani Bara na Zanzibar ; kinachotia wasiwasi zaidi ni ukweli kuwa juhudi kama hiyo itawekewa vipingamizi na serikali, ukichukulia kuwa CUF ni chama cha upinzani na zaidi ni kuwa kina nguvu Zanzibar. Zaidi ya hayo, bila ya jina hilo, CUF kinaweza kupoteza wanachama wake wengi – ambao utiifu wao ni rasilimali kubwa na ni sababu ya ‘ushindi wa mfululizo’ wa chama hicho.

Pamoja na hayo yaliyoelezwa hapo juu, kundi la Zanzibar la CUF linakabiliwa na changamoto kubwa za kifedha baada ya kundi linaloongozwa na Lipumba kutoa TSh. Milioni 369 kutoka katika ruzuku ya chama kutoka serikalini. Hali ni ya changamoto zaidi ukichukulia kuwepo kwa kesi ambazo zipo mahakamani hivi sasa (zinakisiwa kuwa karibu 14) zinazohusiana na mgawanyiko wa chama na dhidi ya kundi lililojitenga linaloongozwa na Lipumba hii ikionyesha gharama zilizo juu kuhusiana na muda na fedha. Linalokera zaidi ni hali ya kutokuwepo utulivu iliyoelezwa na baadhi ya wahojiwa kuhusiana na msaada ambao kundi la Lipumba linaupata kutoka serikalini na chama tawala, chama cha CCM. Dalili za msaada huu zimeonekana kwa kile kilichoelezwa kutambuliwa kusiko kwa kawaida na serikali kwa Lipumba pale Lipumba aliporudi na kufuta kauli yake ya kujiuzulu kuwa mwenyekiti wa CUF. Insemekana kuwa Mrajisi wa Vyama vya Siasa alilikubali hili juu ya kuwepo hali ambayo ilidhaniwa kuwa si ya kawaida. Maoni haya yamefafanuliwa na baadhi ya waliohojiwa.

Kwa mujibu wa uongozi wa CUF, katiba ya chama ina taratibu zilizowazi za kujiuzulu kwa viongozi wake wa juu. Kiongozi anatakiwa awasilishe maombi ya kujiuzulu kwenye mkutano mkuu wa chama wa taifa. Prof. Lipumba alijiuzulu kuwa mwenyekiti wa taifa wa CUF tarehe 5Agosti 2015 kwa madai kuwa hakukubaliana na uteuzi wa Lowassa kuwa mgombea wa upinzani wa UKAWA kwa sababu hakuionga mkono rasimu ya katiba. Hata hivyo, alieleza kuwa ataendelea kuwa

mwanachama wa chama hicho. Tume ilielezwa kuwa baada ya kujiuzulu katikati ya kipindi cha uchaguzi, hapajakuwepo fedha za kuitisha mkutano mkuu wa taifa kuidhinisha kujiuzulu kwake. Takriban mwaka mmoja baadaye, mwezi Juni 2016, Prof. Lipumba alimwandikia katibu mkuu wa CUF ili kufuta kujiuzulu kwake na kueleza kuwa ameshika tena nafasi yake ya mwenyekiti wa taifa wa chama. Mkutano mkuu wa taifa usio wa kawaida wa CUF ulifanyika tarehe 21 Agosti 2016 baada ya Prof. Lipumba kuibuka tena na kuthibitisha kujiuzulu kwake. Wiki mbali baadaye baraza kuu la utawala la CUF liliamua kumsimamisha kwa muda kutoka kwenye chama, Lipumba pamoja na wanachama wengine 10 ambao wawili walikuwa Wabunge. Hata hivyo, Lipumba alikataa kufukuzwa na kulipeleka shauri hilo kwa Mrajis wa Vyama vya Siasa kwa uamuzi. Mrajis alithibitisha kuwa Prof. Lipumba bado alikuwa mwenyekiti wa chama baada ya kufuta kujiuzulu kwake. Mrajisi alizidi kueleza kuwa mkutano mkuu wa taifa wa mwezi Agosti na mikutano iliyofuatia ili kujadiliana suala hilo ilikuwa ni batili kwa sababu Lipumba alikwishafuta kujiuzulu kwake. CUF kiliuona uamuzi wa mrajis kuwa si wa halali na kilikwenda mahakamani kuupinga. Kulingana na uamuzi uliopita wa Mahakama Kuu, CUF kilieleza kuwa Mrajis wa Vyama vya Siasa hakuwa na uwezo kuhusiana maamuzi ya ndani ya kisiasa.

Haraka iliyofanywa kuwaondoa bungeni wawakilishi wanawake wanane wa CUF mwezi Julai 2017 na nafasi zao kuchukuliwa kwa haraka na walioteuliwa wa Lipumba ni suala la kuangaliwa. Maelezo ya tukio hili kwa tume yalikuwa wazi: *Ilichukua siku mbili tu kwa Mrajis wa Vyama vya Siasa kuidhinisha kuondolewa wanawake wawakilishi wanane wa CUF kutoka Bungeni, kwa kawaida jambo linalofanywa na mahakama; siku mbili kwa Kamati ya Utekelezaji EC kutena wawakilishi mbadala; na wiki moja kuapishwa na Bunge wawakilishi wanawake wapya.*

Matukio yaliyotajwa hapo juu yamesababisha kuwepo kwa kesi nyingi mahakamani tokea wakati huo.

Muhojiwa mwengine akielezea wasiwasi wake kuhusu hali hii, alieleza kuwa: 'Mwenyekiti amejuzulu lakini sasa amekidai tena kiti,

na anasaidiwa na serikali, polisi na mrajis wa vyama vya siasa. Kuna kesi 22 kuhusiana na mgogoro huu.’

Suala jingine ni tukio linalotarajiwa la kubadili sheria, ambazo zinaweza kuwa na athari za ukandamizaji kwa upinzani. Watu wanaamini kuwa badiliko la hivi karibuni la Sheria ya Uchaguzi kuikabidhi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar madaraka ya kufuta uchaguzi inaonesha uwezekano wa serikali kupitia upya na kubadili sheria mbali mbali kwa nia ya kuukandamiza upinzani. Watu wengine walikuwa na mawazo kuwa ingelikuwa haikuhitajika kura ya maoni, Serikali ya Umoja wa Kitaifa nayo pia ingelifutwa katika katiba. Wengine walikuwa na mawazo kuwa yalitarajiwa kufanywa mabadiliko ya sheria ya kumzuia au kumtoa mgombea yeyote yule ambaye huko nyuma aligombea katika uchaguzi wa rais akashindwa. Huu ulitafsiriwa kuwa ni mpango unaomlenga mahasusi mgombea urais mara nne na kiongozi wa CUF, Maalim Seif Hamad, na wenye nia ya kumkatisha tama katika kugombea uchaguzi wa rais mwaka 2020. Palikuwa na hofu kuwa bila ya Hamad, CUF itadhoofika. *CUF itakufa*, ndivyo muhojiwa mmoja alivyosema.

Swali linalotia wasiwasi ni kuhusiana na mustakbali wa jina la chama na hadhi yake ya kisheria, kuendelea kwake kuwepo na hasa kushiriki kwake katika uchaguzi wa 2020, pamoja na ukimya wa chama hicho kuhusu hatua yake nyengine. Haya yamekuwa ni chanzo kikubwa cha , wasiwasi kwa wengi wakati tume ikiwa kazini.

Kwa jumla, namna ambayo Rais Magufuli amekuwa akiutendea upinzani Tanzania imewalazimisha baadhi ya wahojiwa kudhani kuwa hautokuwepo upinzani wowote mwaka 2020. Wanaamini kuwa Rais Magufuli anauchukia upinzani. Ilidhaniwa kuwa ‘anataka ukanyagwekanyagwe ili pasiwepo na changamoto mwaka 2020’. Pamoja na hayo, ni mawazo kuwa vyama vya upinzani viwili vyenye nguvu vimekuwa na changamoto kubwa: *CHADEMA ina matatizo yake na CUF nayo vile vile.*

## Hitimisho na Mapendekezo

---

Haja ya kuirekebisha hali ya Zanzibar ni kubwa sana. Kwa maoni ya tume, palikuwepo na viashirio vya dhahiri kuwa waliohojiwa wengi wanataka hali ya Zanzibar irekebishwe kwa haraka, kabla ya mwaka 2020. Kwa maoni ya tume kutokuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ilivyoelezwa kwenye katiba ni upungufu mkubwa kwa suluhisho la watu wenyewe la vurugu za uchaguzi zisizokwisha katika jamii iliyogawika katikati kwa sababu za kikabila, kitabaka, kijamii na kisiasa. Tume inaamini kwa dhati kuwa machafuko yanaweza kuzidi kwa kiwango kisichotarajiwa ukifika mwaka 2020, ukiichukulia hali ya Zanzibar yenye historia ya chaguzi za vurugu. Ni vyema kama litatafutwa suluhisho mapema kabla ya hapo.

### Aina za Uingiliaji Kati

Tume inapendekeza uingiliaji kati ufuatao ili kurekebisha hali ya hivi sasa ya Zanzibar:

1. Kurejeshwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa
2. Majadiliano kati ya CUF na CCM na wadau wengine katika mjadala wa kitaifa wa Zanzibar
3. Kutilia maanani maslahi ya umma
4. Marekebisho ya Katiba
5. Serikali ya muda
6. Marekebisho ya uchaguzi

## **Wahusika Mbali Mbali**

Wakati tume inapendekeza hatua za hapo juu, jukumu la kwanza na la mwisho la kusuluhisha matatizo ya Zanzibar ni la watu wa Zanzibar wenyewe. Wahusika wengine wanaweza kuwa na jukumu la uwezesaji.

### **Jamii ya kimataifa**

Wakati ni wahojiwa wachache tu ndio waliokuwa na imani na uingiliaji kati wa Umoja wa Mataifa katika kusuluhisha matatizo ya Zanzibar, wengi wanahisi kuwa suluhisho halimo mikononi mwa wageni nje ya bara hili: ‘Hatuwezi kuitegemea jamii ya kimataifa – wageni hawawezi kusuluhisha matatizo ya Zanzibar’. Baadhi yao wameeleza kukatishwa tamaa na jamii ya kimataifa kwa kuitelekeza Zanzibar baada ya kufutwa kwa uchaguzi wa 2015 na marudio ya uchaguzi wa 2016. Hakuna wasiwasi kuwa jamii ya kimataifa ina rasilimali za kidiplomasia wanazoweza kuzitumia katika kusuluhisha hali kama ile ya Zanzibar. Hata hivyo, hilo linahitaji fedha lakini na fimbo mkononi.

Na hatua hizo za fedha na fimbo mkononi zina kiwango chake pamoja na kuwekewa vikwazo. Baadhi ya wakati uingiliaji kati wa kimataifa unakuwa na masharti. Kusema kweli, suala la wageni watatetea maslahi ya nani kama itawabidi waingilie kati kwa hali ya Zanzibar lilijitokeza sana wakati tume ikiwa kazini. Zaidi ya hayo, kuna changamoto ya kuweka na kuendeleza vikwazo kwa muda fulani au hata kufikia uamuzi wa pamoja kwa nchi zote zinazohusika kwa kuwa hatua za ‘fimbo mkononi’ zinataka mtazamo wa kijumuiya. Lakini la muhimu zaidi ni kuwa hatua kama hizi hazifai kwa kuwa kwa kawaida waathiriwa wanakuwa ni watu wa kawaida wanaopata shida za kiuchumi na vurugu ya kijamii kwa sababu ya vikwazo vya kiuchumi. Pale inapokuwa hilo ndilo suluhisho pekee lililobaki, ushawishi na kuzileta pamoja mezani pande husika liwe ndiyo jambo la kwanza.

Kwa hali ya Zanzibar, hatua ya ‘fimbo mkononi’ ilichukuliwa pale fedha za Tanzania zilipozuiliwa baada ya marudio ya uchaguzi wa 2016 na kufuatia hilo wananchi wa kawaida walipambana na mfumko wa bei uliokuwa ukipanda na bei za juu za vyakula. Vyenginevyo, baada ya uchaguzi wa marudio wa 2016, tume za hapa nchini na za kimataifa zilizokuwepo Tanzania katika taarifa yao ya mwisho ya pamoja waliipunguza uzito hali ya Zanzibar na kutaka yawepo masikilizano kati ya wahusika wakuu. Hakuna uingiliaji kati wa moja kwa moja uliofanyika tokea wakati huo. Kampeni ya kimataifa ya CUF iliyokuwa na nia ya kuuzindua Umoja wa Taifa na nchi kubwa za magharibi haikuzaa matunda mengi. Hivi sasa, nchi za magharibi zinaangalia ndani mwao na zimeshughulika na changamoto zao zaidi na kuingilia kati katika mambo ya Afrika na sehemu nyengine ni mambo yasiyowashughulisha. Tume inakumbuka vile vile, kuwa moja ya mambo yaliyosababisha kutofanikiwa kwa *Muafaka I*, ni shaka ya Wazanzibari na hata CCM na CUF kuhusu jukumu la upatanishi wa jumuiya ya Madola ambao ndio uliosababisha upatanishi wa ndani wa *Muafaka II*.

Zaidi ya hayo, mara nyingi, uingiliaji kati wa kimataifa unakataliwa kwa sababu ya kuingilia kati mambo ya nchi zinazojitawala.

Ijapokuwa hatua chanya za kidiplomasia inabidi zichukuliwe pale inapowezekana ili kusuluhisha hali ya Zanzibar, lazima itiliwe maanani kuwa hatua hizi zinaangaliwa kwa wasiwasi na kuwa ni uingiliaji kati ulio hasi katika kutafuta maelewano. Tume inatilia mkazo kuwa wahusika wakuu lazima wawe wananchi wa Zanzibar.

## **Vyama vya kanda**

Tume inauamini kwa dhati uingiliaji kati wa Bara la Afrika kwa kuwa uingiliaji kati huo utakuwa ni msaada wa kindugu na hautokuwa na nia ya kukandamiza. Tume inabaini vile vile, kuwa kutokana na historia ya Zanzibar, uingiliaji kati wa kuleta usuluhishi kutoka Bara la Afrika, na hasa Afrika ya Mashariki, si jambo jipya. *Muafaka* wa kwanza wa 1958 ulitiwa saina Ghana, na wa 1963 kwenye mkutano

mkuu wa Mbale, Uganda na iliungwa mkono na PAFMEACA, ikijaribu kuvipatanisha vyama vilivyokuwa vikivutana vya Zanzibar.

Hata hivyo, ijapokuwa Umoja wa Afrika (AU) , Jumuiya ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) waliangalia uchaguzi wa Zanzibar wa 2015 na kutoa ripoti zilizopongezwa na Wazanzibari kwa kuuita uchaguzi huo kuwa ulikuwa huru na wa haki, ripoti hizo, kama zilivyokuwa ripoti nyengine zilizotolewa na vikundi vya watazamaji uchaguzi wa kigeni, zilihusu uchaguzi tu na mapendekezo yao yalikusiana na mchakato wa uchaguzi tu. Hakuna hata moja katika ripoti hizo iliyoelezea kuhusu masuala muhimu ya msingi ambayo ndiyo sababu ya hali ya sasa ya kisiasa ya Zanzibar. La muhimu zaidi, na kama ilivyoelezwa kwa uwazi wakati tume ikiwa kazini, hakuna uingiliaji kati wowote uliofanywa kuhusiana na hali ya Zanzibar baada ya hapo, kutoka chama chochote kile cha kanda.

Wakati Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hivi karibuni imekuwa ikipeleka watazamaji wa uchaguzi katika Nchi Wanachama wakati wa uchaguzi, kutojihusisha kwake kwa makusudi katika kusuluhisha hali ya Zanzibar kumbainika wakati tume ikiwa kazini. Wazanzibari wamekata tamaa kuwa hata chombo chao wenyewe cha kanda kimejitoa kutoka katika jukumu hili adhimu. Mwisho wa mchakato wa uchaguzi wa 2015, taarifa iliyotolewa na Tume ya Waangalizi wa Uchaguzi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki juu ya hali ya Zanzibar ya baada ya uchaguzi kufuatia kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa rais imewataka wadau wa kisiasa kusuluhisha mgogoro huo kwa maelewano.<sup>178</sup> Kama walivyofanya wengine, hakuna hatua za uingiliaji kati chanya zilizochukuliwa tokea wakati huo.

Hali hii yakukata tamaa imeelezewa kwa ufasaha wakati tume ikiwa kazini: *Huwezi kuilinganisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Magharibi kuhusiana na usuluhishi*

---

178 Ripoti ya Watazamaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, op. cit., uk.38

*wa kikanda. Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni klubu ya madikteta; na SADC vile vile (wakati Mugabe na Zuma wakiva humo).*

Hata hivyo, Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki uko wazi kuhusu majukumu yake kwa Nchi Wanachama katika kuhakikisha kuwepo kwa amani na utawala bora katika kanda. Katika kanuni zake za uendeshaji na za msingi hautili mkazo kuheshimu utawala bora tu; bali unatambua vile vile kuwa amani na usalama kuwa ni mahitaji ya kwanza katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ndani ya jumuiya na kueleza kuwa jumuiya itahakikisha uendelezaji wa amani, usalama na utulivu ndani ya jumuiya na ujirani mwema kati ya Nchi Wanachama. Kadhalika, mkataba huo unazitaka Nchi Wanachama kulinda amani na kuimarisha usalama wa kimataifa miongoni mwao chini ya sera ya namna moja ya nchi za nje na ya amani.<sup>179</sup>

Tume inaamini kuwa vipemgele hivi vinaitaka Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kufuatilia migogoro kama ule wa Zanzibar badala ya kuishia kutazama uchaguzi tu. Mafunzo yaliyopatikana kutoka Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Magharibi yako wazi na yanapinga ile hoja iliyozeleka ya kutoingilia utawala wa kitaifa.

Lakini vyovyote itakavyokuwa, tume imeona namna bora ambayo Umoja wa Afrika unaweza kutoa mchango mkubwa na muhimu huko Zanzibar kuliko Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Ijapokuwa uingiliaji kati wa Umoja wa Afrika haukusuluhisha machafuko ya Burundi, Baraza la Amani na Usalama la Umoja huo limetoa kauli kadha kuhusu hali katika nchi hiyo tarehe 17 Oktoba, 13 Novemba na tarehe 17 Disemba 2015. Zaidi ya hayo, katika juhudi za kuhakikisha ustawi wa wananchi, Umoja wa Afrika ulipeleka Burundi ujumbe mzito kuzungumza juu ya kupeleka kikosi cha kujihami na cha ulinzi cha Umoja wa Afrika.<sup>180</sup> Kwa mujibu wa Ibara ya 4(h) ya Sheria

179 Angalia Ibara ya 5 (3) (f); 6; 123 (3) (d), & 124 (1)

180 Angalia 'EALA concerned about Republic of Burundi', inapatikana katika <https://www.eac.int/press-releases/356-387-916-eala-concerned-about-republic-of-burundi>; na 'EALA to hold public hearing workshop on Republic of Burundi', inapatikana katika

yake, Umoja wa Afrika ulibadili msimamo kutoka *kutoingilia* na kuwa *kutojali* kuhusiana na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na kuchukua madaraka kinyume na katiba katika nchi mwanachama yoyote. Mwezi Julai 2013, Umoja wa Afrika uliisimamisha uanachama Misri pale jeshi lilipoipindua serikali iliyochaguliwa ya Rais Mohamed Morsi El Ayat. Mwezi Machi mwaka huo huo Umoja wa Afrika uliisimamisha uanachama Jamhuri ya Afrika ya Kati baada ya waasi kuchukua madaraka ya serikali kwa nguvu. Baadhi ya Jumuiya za Kanda zimefanikiwa kuwazuia viongozi wapinzani wa demokrasia waliotaka kuongeza muda wao wa kukaa madarakani. Kwa mfano Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Magharibi kwa kukitumia kikosi chake cha kijeshi kilichopewa jina la ‘Operesheni Ruridisha Demokrasia’, kwa mafanikio, ilimlazimisha kuondoka madarakani Yahya Jame Rais wa Gambia pale alipojaribu kung’ang’ania madaraka baada ya kushindwa uchaguzi.

Ilivyo, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ingeliweza kuchukua hatua. Hata kwa maslahi yake yenyewe, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ingeliweza kuchukua hatua ya kutafuta suluhisho kwa mgogoro wa Zanzibar ili kuepukana na uwezekano wa kuibuka ugaidi ambao umeanza kuonesha sura yake mbaya kwa miripuko katika takriban Nchi zote Wanachama – Tanzania yenyewe, Kenya, Uganda, Burundi, Somalia nchi jirani na hivi karibuni, Mozambique –, hii ni kwa sababu ya hofu kuwa Zanzibar inaweza kuwa ni mahali mwafaka pa kuibuka siasa kali kwa sababu ya kuwepo idadi kubwa ya vijana, wasiokuwa na kazi na wenye chuki za kisiasa.

Hata hivyo, kuna nyumba nyingi za vioo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Nchi zote zinahusika na vitendo vya kupinga demokrasia na kuvunja katiba na zina changamoto zinazofanana na zile za Zanzibar, kama vile udanganyifu katika uchaguzi, vurugu, hali ya kukosa uvumilivu, migogoro ya kikabila na utaweala mbaya.

Kuingilia kati mgogoro wa Zanzibar, viongozi wa Afrika ya Mashariki wataweza kuona kuwa ni sawa na kufungua kisanduku cha pandora. Kwa hivyo, haiwezekani kuwa suala la Zanzibar lipelekwe katika ngazi ya kikao cha wakuu wa nchi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa sababu viongozi wa hivi sasa katika kanda hii hawana sifa za kuwa wasuluhishi kwa mgogoro kama huo. Huko Uganda na Kenya, chaguzi za rais zimepingwa mara kwa mara. Wakati serikali na viongozi katika kanda wanakabiliwa na masuala kama hayo ya kukosa sifa, nchi zao zikiwa na migogoro ya kidemokresia na uhalali, kanda hii kama ilivyo hivi sasa haiwezi kuwa na msaada wowote.

Labda Bunge la Afrika ya Mashariki (EALA), chombo cha kutunga sheria cha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambacho wajumbe wake si wa kutoka vyama tawala pekee, linaweza kuingilia kati katika suala la Zanzibar ikiwa ni katika kutimiza jukumu lake la uwakilishi na mawasiliano. Ijapokuwa halikufanikiwa kikamilifu, Bunge la Afrika ya Mashariki liliingilia kati katika mgogoro wa kisiasa na wa kibinaadamu wa Burundi. Kuanzia tarehe 14 hadi 15 Januari 2016, Kamati ya Mambo ya Kikanda na Usuluhishi wa Migogoro ya Bunge la Afrika ya Mashariki ilifanya warsha ya hadhara mjini Arusha kuhusu mgogoro wa ubinaadamu nchini Burundi. Warsha hii ilifuatiwa na ombi lililowasilishwa kwa Spika wa Bunge la Afrika ya Mashariki na Chama cha Wanasheria wa Bara la Afrika (PAULA) na Jumuiya za Kiraia nne ambazo ni Jukwaa la Jumuiya za Kiraia za Afrika ya Mashariki, Chama Kinachoangalia Udhalilishaji cha Afrika, Kituo cha Ushiriki wa Wananchi katika Umoja wa Afrika, Chama cha Wanasheria cha Afrika ya Mashariki na Kituo cha Katiba, tarehe 16 November 2015, wakilitaka Bunge la Afrika Mashariki kuingilia kati haraka katika mgogoro wa Burundi. Waliopeleka ombi hilo walilitaka Bunge la Afrika ya Mashariki kuuomba Umoja wa Afrika kuingilia katika katika mgogoro wa kisiasa na wa kibinadamu wa Burundi, na vile vile wamelitaka Bunge hilo kupeleka maazimio madhubuti kwenye Mkutano wa Kilele wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

wasiiruhusu nchi hiyo kuchukua nafasi ya uwenyekiti wa mzunguko wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mpaka hapo itakaposuluhisha migogorio ya kisiasa, haki za binadamu na hali ya ubinadamu katika nchi hiyo. Kamati hiyo ilikutana pia na wadau kutoka Burundi tarehe 15 Januari 2016 na ujumbe wa ngazi ya juu kutoka katika Serikali ya Burundi ulitoa maelezo yake kwa kamati hiyo tarehe 25 Januari 2016. Ripoti ya kamati ilijadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lote na baada ya hapo, Bunge liliutaka Mkutano wa Kilele wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kutilia mkazo jukumu lake la kuwalinda na kuwahami wananchi wa Burundi dhidi ya fujo na kuwahakikishia usalama wao.<sup>181</sup>

Wazo la kulitumia Bunge la Afrika ya Mashariki inabidi lifuatiliwe kwa nguvu na kwa haraka.

### **Viongozi wa kanda**

Tume imetilia maanani jukumu la viongozi waliopita, kama vile marehemu Mwalimu Nyerere na marehemu Nelson Mandela, wakati wa machafuko ya Burundi na Rwanda katikati ya miaka ya 1990 na mazungumzo juu ya Burundi yaliyofanyika Arusha, na kuyahusisha mafanikio ya mikutano hiyo na heshima na busara zao. Ijapokuwa baadhi ya wahojiwa wameeleza wasiwasi wa kuweza kupatikana watu wenye uwezo na ujuzi wa usuluhishi katika kanda kwa hali kama ya Zanzibar, mawazo ya tume ni kinyume na hayo. Hivi karibuni, viongozi kutoka katika kanda hii, kama vile Rais Mkapu, waliungana na viongozi wengine wa bara hili wakiongozwa na Kofi Anan kusuluhisha mgogoro wa baada ya uchaguzi wa 2007 nchini Kenya. Ijapokuwa kuna uhaba wa viongozi wa zamani nje ya Tanzania na Kenya, tunaweza kuangalia kwengine katika bara hili kwa watu kama aliyekuwa rais wa Msumbiji, Joachim Chissano, aliyehusika katika kusuluhisha mgogoro wa Sudan ya Kusini, na viongozi wengine kama hao. Uingiliaji kati wa viongozi kama hao kwa hali ya

---

181 Ibid.

Zanzibar inabidi utafutwe kwa juhudi. Juhudi kama hizo hazihitaji kusababisha vifo na mateso. Historia ya machafuko ya uchaguzi Zanzibar imekuwa ni ya mfululizo kiasi cha kumfanya mtu atabiri hatari na kuchukua hatua madhubuti za kuzuia hatari hiyo.

Mahakama ya Afrika ya Mashariki inaweza kutoa mchango. Mahakama hiyo ya kanda imeamua masuala kadha yanayohusiana na utawala na katiba kutoka kwenye Nchi Wanachama. Miongoni mwa masuala hayo ni mashauri yanayohusiana na muundo wa Bunge la Afrika ya Mashariki lenyewe, migogoro ya uchaguzi na ukiukwaji wa haki za binadamu, bila ya kutaja mgogoro mmoja uliowasilishwa na Wazanzibari hivi karibuni: *Rashid Salum Adiy & wengine dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Tanzania*,<sup>182</sup> ambapo Adiy na raia wengine wa Zanzibar 39,999 wameiomba Mahakama ya Afrika ya Mashariki kupinga uhalali wa Muungano wa Tanzania.<sup>183</sup>

## **Jukumu la Wazanzibari**

Wakati majukumu mengine yanaweza kukabidhiwa kwa wahusika wa kanda hii, jukumu kubwa la kusuluhisha mgogoro wa hivi sasa limo mikononi mwa watu wa Zanzibar. Juhudi nyengine zote zinaweza kuwa ni za kusaidia tu. Kusema kweli, kwa watu wa Zanzibar kuweza kufikia *Miafaka* mbali mbali na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, wamedhihirisha wazi uwezo wao wa kutatua matatizo yao wao wenyewe.

## **Vyama vya Siasa**

Tume inaamini kuwa, kikiwa ni chama tawala, CCM Zanzibar kina haja ya kufikiria utaratibu wa kugawana madaraka utakaotilia maanani maoni ya watu wa Zanzibar.

182 Mahakama ya Afrika ya Mashariki Ombi Na.07 la 2017, limeamuliwa na mahakama tarehe 8 Mchi 2018

183 Mahakama imelikataa ombi kwa sababu wakala aliyeteuliwa na Mlalamikaji hana *ubalali wa kisheria* kwa sababu ya madaraka ya kisheria yenye kasoro

CCM Zanzibar, kama ilivyokuwa katika *Maridhiano*, lazima ichukue hatua hii ya kijasiri kwa maslahi ya taifa. CCM lazima ioneshe tawi la mzaituni kwa CUF na CUF nayo ipatane na chama tawala kwa maslahi ya nchi.

### ***Viongozi wa Vyama***

Walio muhimu katika mchakato huu ni viongozi wa vyama. Viongozi wa vyama vya CCM na CUF wana jukumu maalum katika kumaliza mgogoro huu. Ni maoni ya tume kuwa usuluhishi unawezekana kwa kuwa ulikwishapatikana hapo kabla – pale ilipopatika *Miafaka* na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Maalim Seif na aliyekuwa Rais Karume waliposahau tofauti zao na kukubali kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa maslahi ya Zanzibar ya amani, yenye utulivu na iliyoendelea. Bila ya kujali wasiwasi waliokuwa nao baadhi ya waliohojiwa, kwa jumla wanakubaliana kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ingelikuwepo mapema wakati Karume akiwa rais, serikali hiyo ingelikuwa na msingi madhubuti zaidi. Hivi sasa haijulikani Karume ana jukumu gani, akiwa ni mmojawapo wa waasisi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Haijulikani amekabidhiwa jukumu gani na Serikali ya Zanzibar na/au ya Muungano, katika hali ngumu inayoikabili Zanzibatr. Utafutaji wa suluhisho la hapa nyumbani unaweza kufanikiwa kutokana na mtu mwenye hadhi kama yake ambaye hawezi kugombea nafasi ya kisiasa na anaweza kuwa na muda wa kutosha wa kushughulikia hali ya migogoro tokea alipoacha madaraka.

Jukumu la Maalim Seif wakati huu ni muhimu sana. Siyo kwa sababu ya wafuasi wengi alioweza kuwakusanya kwa muda wote tu lakini pia kwa sababu ya wasifu wake ambao umesaidia katika kuwatuliza wafuasi waliokasirika na waliokata tamaa wa CUF, hasa vijana. Kusema kweli, kama msomi mmoja alivyoeleza: ‘Si jambo linalotiwa chumvi kusema kuwa Seif ni mtu muhimu katika visiwa hivi na Tanzania kwa jumla. Anaheshimiwa na kuungwa mkono na

mamia ya maelfu ya Wazanzibari?<sup>184</sup> Zaidi ya hayo, kama mfuasi mmoja wa CCM alivyokiri kuhusiana na kuwa kwake na wafuasi wengi sana huko Pemba: ‘Ni shida kuwapata watu wa Pemba ila kama maalim Seif amefariki!’

Ushupavu wa Maalim unaweza kuivuruga au kuijenga Zanzibar katika kipindi hiki kigumu.

Tume inaamini kuwa watu binafsi watakaokubalika pande zote mbili kutoka CCM Tanzania Bara wanaweza kuhitajika. Ukiiangalia hali ya Muungano, ushirikishwaji wa CCM Bara unaweza kuwa ni lazima. Hata hivyo, hili liwe baada wa Wazanzibari kukubaliana. CCM inaweza kuwaainisha watu hao kwa kushauriana na watu wa Zanzibar.

Kwa maslahi ya ushirikishwaji na kama ilivyoenezwa wakati tume ikiwa kazini, siasa za Zanzibar lazima ziache kuwa ni za vyama viwili – za CCM na CUF tu. Ijapokuwa inaeleweka kuwa CCM na CUF zina dhamana kubwa katika kusuluhisha mgogoro wa Zanzibar, juhudi za vyama vyote viwili lazima zijumuishe na za vyama vingine. Vyama vidogo na viongozi wao lazima vishirikishwe. Hata hivyo, lazima ichukuliwe tahadhari ili kuhakikisha kuwa ni vyama vyenye sifa tu ndivyo vinavyoshirikishwa katika majadiliano kati ya vyama mbali mbali.

### ***Watu binafsi wa kushirikishwa***

Katika mahojiano yetu na wahojiwa wakati tume ikiwakazini, waliainishwa watu binafsi kwa kuzingatia imani za kisiasa ambao wanaweza kutoa mchango katika majadiliano kati ya viongozi wa CCM na CUF. Watu hao itabidi wakubaliwe na pande zote mbili zinazopingana. Tume inawapa changamoto wazanzibari, kujiangalia na bila ya kuchelewa, kuainisha watu hao. Kuwaainisha na kuwaleta watu hao pamoja unaweza kuwa ni mwanzo mzuri.

184 Angalia Othman, Haroub Miraji: Mapitio ya kitabu, Burgess, Gut Thomas (ed.) ‘Race, revolution and the struggles for human rights in Zanzibar: Maelezo ya Ali Sultan Issa na Seif Sharif Hamad’, katika *Zanzibar Yearbook of Law*, Juzuu ya 1, 2011, op. cit., uk.388

Lililo muhimu ni kuwa ule utamadunu wa kuficha na kuufanya mchakato wa upatanishi kuwa siri kama ilivyokuwa katika upatanishi uliopita itabidi uachwe. Ili kuondoa hali ya kutiliana shaka na kuwepo uwajibikaji, mchakato wa upatanishi wa siku za mbele itabidi uwe wazi na wananchi wapatiwe habari muhimu kuhusiana na mchakato huo. Haya ni kwa upinzani vile vile. Hii haina maana kuwa hatua zote na mwenendo wa mchakato huo zifanyike hadharani. Ukutilia maanani kiwango cha juu cha ushabiki wa kisiasa na majadiliano ambayo ni sehemu ya utamaduni wa Zanzibar, majadiliano ya wazi juu ya masuala muhimu kama haya kutaongeza heshima ya vyama vyote viwili CCM na CUF kwa wafuasi wao na kwa wananchi kwa jumla.

### ***Jumuiya za kiraia***

#### **■ *Viongozi wa dini***

Ijapokuwa inasemekana kuwa viongozi wa dini wanalipwa na serikali na wengi kuamini kuwa wanatumikia maslahi ya chama tawala cha CCM, tume inaamini kuwa wanaweza kuwa na mchango muhimu katika kuwaandaa watu ili waungane na kuwa na mshikamano wa kijamii kwa kuwa Wazanzibari wengi ni Waisilamu na Uisilamu ni mtindo wa maisha. Ni kweli kuwa viongozi wa dini walitoa mchango mkubwa katika kuwaandaa wananchi kuikubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kupiga kura katika kura ya maoni. Wameshiriki vile vile katika programu za kumaliza fujo Zanzibar, kama ilivyokuwa wakati wa kampeni yao ya kuzuia mashabulizi ya tindikali. Zaidi ya hayo, kama ilivyoelezwa wakati tume ikiwa kazini, Wazanzibari, bila ya kujali uanachama wao katika vyama vya siasa, wanaswali pamoja. Tume imeelezwa vile vile juu ya kuwepo kwa jukwaa la waumini wa dini mbalimbali ambalo linawajumuisha Wakiristo na Wahindu walio wachache katika kutafuta suluhisho la changamoto za kisiasa na kijamii Zanzibar.

### ■ *Vyama Visivyo vya Kiserikali*

Tume imebaini kuwa, bila ya kujali kukamatwa na vitisho kutoka serikalini kwa shughuli zao, vyama visivyo vya kiserikali na vyama vya kijamii vinavyowaleta pamoja vijana, wanawake na mahitaji maalum kama vile haki za binadamu, utawala na masuala ya mazingira vipo Zanzibar. Kama walivyo viongozi wa dini, Vyama Visivyo vya Kiserikali vinaweza kuendesha shughuli za utetezi kwa madhumuni ya kuleta mshikamano na umoja, na kuandaa wananchi katika kuyafikia malengo hayo. Ijapokuwa tume imebaini kuwepo kwa uhaba mkubwa wa kesi za utetezi wa maslahi ya wananchi Zanzibar, bila ya kujali majina yao, Chama Kisicho cha Kiserikali kama vile Chama cha Wanasheria cha Zanzibar, kinachoshughulikia masuala ya utawala kinaweza kushughulikia utetezi wa maslahi ya wananchi kwa mambo muhimu yanayohusiana na uchaguzi wa 2015/16 na masuala ya katiba. Hii ni sawa kabisa kwa Chama cha Wanasheria wa Zanzibar ambacho kisheria kina madaraka ya kushughulikia maslahi ya wananchi.

Tume inatambua hatua chanya iliyochukuliwa kwa kutetea maslahi ya wananchi katika shauri la hivi karibuni la *Rashid Salum Adiy*.<sup>185</sup> Ni juhudi nzuri na ya kutia moyo ambayo imekwenda nje ya mipaka ya kitaifa na kufikia kuwa mchakato wa kusuluhisha mgogoro wa kikanda, ijapokuwa shauri hilo lilitupiliwa mbali kwa sababu za kiufundi.

Wakati tume inatambua hali ya kisiasa inayotisha ambayo inakizuia Chama cha Wanasheria na Jumuiya za Kiraia kama Chama cha Wanasheria Zanzibar zishughulikia utetezi wa maslahi ya wananchi kuhusiana na masuala ya katiba yanayotokana na hali ya Zanzibar ya 2015/16, na suala la uwezo linalovisumbua vyama hivyo, tume inakitaka hasa Chama cha Wanasheria cha Zanzibar, kutimiza wajibu wake wa kisheria wa kuendeleza utawala bora na kuheshimu katiba Zanzibar kwa namna ya kuchukua hadhari kabla

---

185 Op. cit.

ya athari. Kwa sababu hiyo, Chama cha Wanasheria inabidi kijitahidi kujenga uwezo wake katika uwanja huu kwa kujifunza kutoka katika utendaji bora katika kanda hii. Chama cha Wanasheria cha Zanzibar inabidi kichote kutoka katika rasilimali za kiuledi ziliopo katika kanda, hasa Chama cha Wanasheria cha Afrika ya Mashariki, katika kutetea maslahi ya wananchi na katika kuitumia ofisi yake adhimu kuwasuluhisha Wazanzibari.

Rasilimali za vyama vya kanda kama vile Chama cha Wanasheria cha Afrika ya Mashariki na KcK zinaweza kuwa na faida katika kuufanya usuluhishi kuwa ni tukio halisi kwa kuainisha viongozi na watu binafsui wenye sifa katika kanda ili kuendeleza na kuzidisha kasi ya mchakato wa kuleta usuluhishi. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Jumuiya za Kiraia za Kanda zililiomba Bunge la Afrika ya Mashariki kuingilia kati katika mgogoro wa Burundi.

### ***Sekta binafsi***

Tunaamini kuwa, ukiangalia mchango mkubwa ambao sekta binafsi inatoa au inabidi itoe Zanzibar katika kuzalisha ajira na kushirikiana na serikali katika kutoa huduma za jamii, sekta hii inaweza vile vile kushughulikia masuala kadha ambayo yamesababisha hali ya kutoridhika miongoni mwa vijana na wananchi kwa jumla. Kuna uwezo mkubwa wa kibiashara katika visiwa vyote viwili, uwezo ambao unaweza kustawi kwa kuwepo mazingira ya siasa ya amani na utulivu.

### **Kuipitia tena Katiba**

Kama KcK kilivyobaini katika tume zake zilizopita na kusema kweli kama habari nyingi zinazohusiana na Muungano wa Tanzania zinavyoonesha, utawala bora na masuala ya katiba ya Zanzibar ni suala la muungano. Ni kweli kuwa tume imepokea maoni juu ya Muungano na juu ya athari za kukwama kwa mchakato wa kuipitia tena katiba visiwani. Hatimae, ni wazi kuwa usuluhishi ambao hauzingatii muundo wa Muungano ni usuluhishi usiotimia. Kuahirisha azimio

hili la kuipitia tena katiba kunazidi kuipa nguvu imani ya Wazanzibari wengi kuwa ni Bara tu ndiyo inayonufaika na Muungano wakati wao, Wazanzibari wanakandamizwa ndani ya Muungano huo. Wengi wao wanaamini kuwa Muungano uliojengeka na kusimamiwa vyema utakuwa na maslahi kwa wote Visiwani na Bara. Kwa hivyo, tume inapendekeza kuwa mchakato wa kuipitia tena katiba ya Muungano ufufuliwe na hasa kuhusiana na yale yaliyobainika, na wakati huo huo tume iliyopita ya KcK inapendekeza kuwepo kwa Muungano wa serikali tatu kama ilivyopendekezwa na Tume ya Warioba.

Tume inapendekeza vile vile kupitiwa tena katiba ya Zanzibar. Hii inaweza kutanguliwa na kuipitia tena katiba ya Muungano. Mchakato huu utaiwezesha Zanzibar kushughulikia na kusuluhisha masuala ya katiba ambayo ni ya namna ya pekee Zanzibar, kama vile Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Masuala mengine ambayo yanaweza kushughulikiwa ni pamoja na kuimarisha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na mahakama. Ni muhimu sana kuifanya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuwa ni tume huru isiyopendelea upande wowote. Katika hali hiyo hiyo, na mahakama nayo iwe huru na isitegemee mihimili mingine ya dola. Na kuhusiana na uchaguzi, mahaka ipewe uwezo wa kusikiliza maombi yanayopinga matokeo ya uchaguzi wa rais.

## **Usuluhishi Uliokubaliwa**

Tume imebaini kuwa Wazanzibari wanajivunia sana Serikali ya Umoja wa Kitaifa, siyo kwa sababu ni chimbuko la hapohapo nyumbani tu bali kwa sababu kwa mara ya kwanza masuala ya kutengana na ubaguzi katika serikali na katika jamii yalishughulikiwa ipasavyo na vyama vyote viwili, chama tawala na chama kikuu cha upinzani. Hali ya kukata tamaa inayoonekana sasa miongoni mwa Wazanzibari inadhihirisha hali ya kuvunjika moyo kuwa umoja wao na ustahamilivu ulioletwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa imewaponyoka haraka na inaonekana kupotea na kusahauliwa. Ni

maoni ya tume kuwa masuala yote ya hapo juu yanahitaji usuluhishi wa majadiliano na juhudi madhubuti za wahusika wote waliotajwa hapo juu. Tume imebaini juu ya umuhimu wa kuwepo mjadala wa kitaifa ili kutatua suala la mvutano wa kihistoria wa Zanzibar. Tume inatilia mkazo kuwa mabadiliko ya kiuchaguzi na chaguzi zenyewe hayatoshi katika kutatua tatizo la Zanzibar ukichukulia mgawanyiko wa kisiasa uliopo, hata kama chaguzi zitakuwa huru na za haki. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar lazima ifanyiwe mabadiliko lakini hiyo si sababu ya kutosha ya kuhakikisha kuwepo kwa amani. Pamoja na wazo la kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, masuala kama vile vipi serikali hiyo inatiririka hadi kufikia ngazi za chini za serikali pamoja na kuwa na rais wa mzunguko, yanahitaji kujadiliwa. Katika ngazi ya uchaguzi, utaratibu wa uwakilishi wa uiano ukiwa ni pamoja na kujumuisha makundi yaliyotengwa unaweza ukafikiriwa vile vile. Zaidi ya hayo, ijapokuwa mpasuko wa katikati wa jamii ya Wazanzibari unaojionesha wakati wa uchaguzi umekuwepo kabla ya Muungano, muungano huo tokea kuundwa kwake umechangia sana katika matatizo yaliyopo Zanzibar hivi sasa. Kwa hivyo, usuluhishi wa suala la Muungano ni sehemu ya usuluhishi wa suala la Zanzibar vile vile.

Mjadala huo lazima uhakikishe ushirikishwaji wa watu wa Zanzibar, pamoja na vyama vya siasa, Jumiya za Kiraia, Vyama Visivyokuwa vya Kiserikali, Vyama vya Kiuledi, Vyama vya Wafanyakazi, sekta binafsi, viongoi wa dini na wazee. Mjadala wa kitaifa itabidi utengeneze utaratibu wa kuleta maelewano katika ngazi zote kuanzia ngazi za chini kabisa, ili kuhakikisha kuwepo kwa hali ya kuishi pamoja na kuvumiliana katika ngazi zote – bila ya kujali ikiwa haya yamo au hayamo katika katiba na sheria. Inategemewa kuwa mjadala kama huo utafikia kwenye usuluhishi uliokubaliwa.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na *Miafaka* yalikuwa ni usuluhishi uliokubaliwa na kupatikana maelewano katika hali ya hivi sasa kunawezekana; hilo

ndilo Wazanzibari wanalolitaka. Usuluhishi uliokubaliwa ni chaguo lisiloepukika kwa hali ya historia ya Zanzibar na siasa zake ilivyo, na hasa mpasuko wa katikati kati ya wafuasi wa vyama vikubwa viwili – CCM na CUF. Zaidi ya hayo, usuluhishi uliokubaliwa lazima ushughulikie kwa makini suala la mgawanyo wa madaraka. Kutokana na yale ambayo tume imeyaona ni wazi kuwa suala kubwa la Zanzibar ni uraisi. Kadhalika, la msingi katika majadiliano hayo ni masuala kama vile namna gani kuifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ifanyekazi, na hasa urais wa mzunguko, tofautu na ule wa rais anayechaguliwa, na madara ya makamo wa rais wawili katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa utaratibu huu inachukuliwa kuwa uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi utaendelea kuwepo.

Kwa maoni ya tume, ikiwa suala la madaraka katika ngazi ya urais litasuluhishwa, mambo madogomadogo mengi yatasuluhishwa kwa urahisi. Wazo la kuifanyia marekebisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili itiririke kufikia kwenye serikali za mitaa au kwa wateuliwa wasiokuwa wa kisiasa kama vile katika utumishi wa serikali, kama ilivyopendekezwa na baadhi ya wahojiwa wakati tume ikiwa kazini, halitakuwa jambo la lazima. Pendekezo la kuitiririsha Serikali ya Umoja wa Kitaifa hadi kufikia kwenye utumishi wa serikali, uliopo kwa misingi ya utumishi wa serikali unaoegemea upande wa chama tawala linaweza kushughulikiwa kwa kurekebisha na kuweka mchakato wa kuajiri usiokuwa na ushabiki wa vyama na ulio wazi ili kuthibitisha ushirikishwaji na upendeleo kwa wale waliotengwa. Zaidi ya hayo, ari ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa inaweza kuhitaji uingiliaji kati wa haraka ili kuurekebisha utumishi wa umma ili uwe ni wa pande zote chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Ni muhimu kutambua kuwa, wakati tume inaridhika kuwa muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa umejengwa kwa misingi ya historia ya Zanzibar, Serikali ya Umoja wa Kitaifa inahitaji kuingiza masuala yanayoweza kujitokeza baadaye. Inahitaji kuangalia mbali

zaidi kuliko CCM na CUF, kwa kuwa mambo mapya ya kisiasa yanaweza yakajitokeza siku za usoni.

Tume inatilia mkazo kuwa uamuzi wa mwisho juu ya mustakibali wa Zanzibar ni wa Wazanzibari. Kwa hivyo, mapendekezo ya tume hii yako wazi kwa mjadala zaidi na uchambuzi wa Wazanzibari. Baadhi ya mapendekezo au mapendekezo yote yanaweza kutekelezwa, lakini usuluhishi uliokubaliwa unabakia kuwa ndiyo msingi wa mustakibali wa Zanzibar, kisiasa na kikatiba.

# Orodha ya Watu Waliohojiwa

---

## **Dar es Salaam**

Deus Kibamba Dk. Helen Kijo Bisimba	Mwenyekiti, Jukwaa la Katiba Mkurugenzi Mtendaji, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)
Harold Sungusia	Mwanaharakati wa haki za binadamu, mshauri, Sung Consultants
Mhe. Bahame Tom Nyanduga	Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)
Mhe. Ibrahim Lipumpa	Mwenyekiti, Chama cha Wananchi (CUF)
Mhe. J.S. Warioba	Aliyekuwa Mwenyekiti, Tume ya Kuipitia Upya Katiba, Tanzania (CRC)
Mhe. Pole Humphrey	Katibu Mtendaji wa Taifa wa Itikadi na Utangazaji, Chama cha Mapinduzi (CCM)
Prof. Chris Maina Peter Prof. Mwesiga Baregu	Profesa wa Sheria ya Katiba Profesa wa Sayansi ya Siasa

## **Zanzibar**

Abeid Abdullah	Mkurugenzi Mtendaji, Vijana wa Zanzibar dhidi ya Changamoto za Vijana
----------------	-----------------------------------------------------------------------------

Asha About	Umoja wa Vyama Visivyo vya Kiserikali Zanzibar (ANGOZA)
Awadh Ali Said	Alikuwa mjumbe wa Tume ya Kuipitia Upya Katiba na mwanasheria
Commissioner Mohamed Khamis	Tume ya Haki za Binadamu na UtawalaBora CHRAGG, Zanzibar
Dk. Abdulla Mohammed Juma	Mwanahabari, Shirika la Utangazaji Zanzibar
Dk. Mzuri Issa Ali	Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) na mratibu ZANGG
Dk. Yahya Khamis Hamad	Mnasihi Mkuu wa Kisheria , Zanzibar, Tume ya Kuzipitia Upya Sheria
Dk. Moh'd Makame Haji	Chuo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Zanzibar
Hassan Ali Mzee	Mjumbe wa Bodi, Chama cha Wafanya Biashara, Viwanda na Kilimo cha Zanzibar na Mweyekiti Chama cha Waendeshaki Biashara ya Utalii Zanzibar (ZATO)
Mhe. Ali Mzee	Mwanachama wa CCM na mjumbe wa Kamati ya Watu Sita
Mhe. Ally Saleh	Mwanahabari, alikuwa mjumbe wa Tume ya Kuipitia Upya Katiba na Mbunge wa Bunge la Muungano
Mhe. Bakary Khamis Abubaker	Jaji, alikuwa MwanasheriaMkuu, alikuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, mjumbe wa Kamati

	ya Watu Sita ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa
Mhe. Fatuma Fereji	Mwenyekiti, Umoja wa Wanawake wa CUF
Mhe. Himid Yusuf	Alikuwa waziri na mjumbe wa Kamati ya Watu Sita ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa
Mhe. Ismail Jussa	Mkurugenzi wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa wa CUF, alikuwa mjumbe wa Kamati ya Watu Sita ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na alikuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi
Mhe. Maalim Seif Hamad Sharif	Katibu Mkuu, Chama cha Wananchi (CUF)
Mhe. Mohammad Yussuf	Alikuwa mjumbe wa Tume ya Kuipitia Upya Katiba na Mkurugenzi Mtendaji, Taasisi ya Zanzibar ya Utafiti na Sera za Umma
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Naibu Katibu Mkuu, CUF
Mhe. Nassor Mohammed	Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, alikuwa mjumbe wa Tume ya Kuipitia Upya Katiba na mwanasheria
Mhe. Othman Masoud Othman	Alikuwa Mwanasheria Mkuu
Mhe. Simai	Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Tunguu
Jamila Juma	Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA)
Jaji Msibe	Mwenyekiti, Tume ya Kuzipitia Upya Sheria Zanzibar
Lulu Abdallah Omar	Marafiki wa Zanzibar

Lusungu Leonard Mbilinyi	Kituo cha waumini wa dini mbali mbali Zanzibar
Musa Omar Tafurwa	Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC)
Mustafa Sherif	Mjumbe, Kamati ya Utendaji ya Vijana wa Zanzibar dhidi ya Changamoto za Vijana
Nik Bredholt	Mratibu, Kituo cha Waumini wa Dini Mbali mbali, Zanzibar
Omar Said Shaaban	Chama cha Wanasheria cha Zanzibar (ZLS)
Prof. Abdul Sherif Saida Abdallah	Profesa wa Historia Kaimu Mkurugenzi Mtendaji , Kituo cha Huduma za Sheria, Zanzibar Legal Service (ZLSC)
Sheikh Soraga	Ofisi ya Imam

## **Pemba**

Abubakar M. Ali	Mkurugenzi Mtendaji , Chama cha Wakulima wa Karafuu Zanzibar
Ali Mohammed Ali Feisal Abdalla Saidi	Emir, Chama cha Maimam Mwenyekiti/mwana elimu, Chama cha Kutoa Huduma kwa Wafugaji (LIFSOPE)
Haji Dawa Haji	Cha cha Kuendeleza Wavuvi Mwambe
Kassim Khamis Rashid	Mwenyekiti, Chama cha Wakulima wa Karafuu Zanzibar
Kombo Ahmed Issa	Kijana

Mohamed Ali Masoud	Daktari wa Mifugo/Afisa Mipango, Chama cha kuhudumia wafugaji
Nassor Haji Nassor Rahim Simai Makame	Chama cha Kuendeleza Wavuvi Mwambe
Said Bakar Hamza	Katibu, Chama cha Wakulima cha Mtakata (MCCOS)
Saleh Abdalla Mohammed Suleiman Said Mohammed	Kijana Naibu mwenyekiti Wakulima wa Mtakata
Sumaya Othman Ibrahim Yusuf Abdalla Ramadhan	Kijana JUMAZA, Chama cha Maimam Zanzibar

## **Makundi yaliyolengwa**

### ***Vijana (Vijijini)***

Haji Ussi Pandu  
Kazija Ali Shauri  
Maryaam Abdi  
Rabia Fadhi  
Raya Ali Nyange  
Sheha Ali Khamis  
Suleiman Habib  
Zubeir Daud

### ***Vijana (Mjini)***

Aysha Juma Mussa  
George Mkwaya  
Iddi Haji  
Lailat Abed  
Mohammed Ibrahim  
Saadat Soud  
Seif Gharib  
Shadida Omar Ali

### ***Wanawake (Vijijini)***

Amne Khamis  
Arafa Hamad Mwinyi  
Maryam Jafar Said  
Maryam Khamis Ngwali  
Miza Foum Mwadini  
Nuru Nyange Makame  
Rusina Salum Ali  
Ummulkultum Ambar Ujud

### ***Wanawake (Mjini)***

Amne Khamis Ahmada  
Badria Salim  
Barke  
Hanifa Sali  
Khadija  
Khayrat Zahor  
Rusan Salum Ali  
Safia  
Shemsa Salahdin  
Ummul Kultham Ambar  
Zaituni

# Rejea

- Ali Uki, 'Maridhiano and the Government of National Unity, its impact on elections and constitutionalism in Tanzania', katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), in *Zanzibar, The Development of the Constitution*, 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3
- Bakari Kombo Mussa, 'The state of constitutionalism in Zanzibar 2015', katika Mwesiga Baregu, *Annual State of Constitutionalism in East Africa 2015*, 2016, Kampala, Fountain Publishers
- Bakary Khamis Abubaker, katika *Zanzibar YearBook of Law*, Vol., 1, 2011
- 'Election Observation Mission to the 20th March 2016 Re-Run General Elections in Zanzibar Statement, Zanzibar 21st March, 2016', imeambatanishwa katika *Report of the EAC Observer Mission to the 2015 Tanzania General Elections, 18-25 October 2015*
- European Union Election Observation Mission, United Republic of Tanzania, Final Report, General Elections 2015*
- Glassman, Jonathan, *War of Words, War of Stones: Racial Thought and Violence in Colonial Zanzibar*, 2011, Indiana: Indiana University Press
- Hamad Khamis Mohamed, 'The state of constitutionalism in Zanzibar 2011', katika Makulilo B. Alexander (ed), *Annual State of Constitutionalism in East Africa 2011*, Kampala, Uganda, Fountain Publishers, 2013
- Hamad Khamis Yahya & Peter Maina Chris, 'Elections in Zanzibar and their consequences: ZEMOG na Miafaka', katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), in *Zanzibar, The Development of the Constitution*, 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3
- <https://eisa.org.za/wep/zan2000election2.htm>
- Jjuuko Frederick & Muriuki Godfrey, *Federation within Federation, The Tanzania Union Experience and the East African Integration Process*, Ripoti ya Kituo cha Katiba Tume ya Kutafuta Ukweli wa Mambo Tanzania

- Lowry Willy, 'Zanzibar bombings may be related to a disputed election', *The New York Times*, 1 November 2015, imepatikana katika [www.nytimes.com/2015/11/02/world/africa/zanzibar](http://www.nytimes.com/2015/11/02/world/africa/zanzibar)
- Oloka Onyango Joe na Nassali Maria, *Constitutionalism and Political Stability in Zanzibar: The Search for a New Vision*, Ripoti ya Tume ya Kutafuta Ukweli wa Mambo iliyotumwa na Kituo cha Katiba, Oktoba 2003
- Othman Haroub, Yes, in *My Lifetime: Selected Works of Haroub Othman*, Saidha Yahya-Othman (ed), 2014, Mkuki na Nyota
- Othman, Haroub Miraji: Book reviews, Burgess, Gut Thomas (ed) 'Race, revolution and the struggles for human rights in Zanzibar: Memoirs of Ali Sultan Issa and Seif Sharif Hamad', katika *Zanzibar YearBook of Law*, Vol.1, 2011
- Peter Maina Chris, 'Recent developments in Zanzibar: From Miafaka to Maridhiano and Government of National Unity', katika *Zanzibar, The Development of the Constitution*; 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3
- Ripoti ya Tume ya Kutazama Uchaguzi wa 2015 Tanzania ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, 18-29 Oktoba 2015. EAC Secretariat, Tanzania, 18 January 2016
- The *Election Observation Mission, Zanzibar 2015*, Friedrich Nauman Stiftung, amepatikana katika <http://www.scribd.com/document/289609067/Report-Zanzibar-2015>
- Throup David W, 'Commentary: The political crisis in Zanzibar', March 2016, imepatikana katika <http://www.csis.org/analysis/political-crisis-zanzibar>
- UNPO news reports, inapatikana katika <http://www.unpo.org/article/15390>
- Yahya Khamis Hamad, 'The constitutional premises of the GNU in Zanzibar', katika Chris Maina Peter & Immi Sikand (eds), katika *Zanzibar, The Development of the Constitution*; 2011, Zanzibar, Zanzibar Legal Services Centre, Publication Series Book No.3

Yusuf Issa, 'Tanzania: Concerns over Zanzibar's Govt of National Unity', *Tanzania Daily News*, 31 October, 2012, imepatikana katika <http://allafrica.com/stories/201210310157.html>

'Zanzibar: Power-sharing mechanism proves successful', *The Citizen*, 21 January 2013, imepatikana katika <http://unpo.org/article/15390>

## **Kesi**

*Rashid Salum Adiy & wengine dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Tanzania*, EACJ Application No.07 of 2017